Kikao cha Nne - Tarehe 16 Machi, 2015

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

Hati za Kuwasilisha Mezani:

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano Na. 1 ya 1999 na kutunga Sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha mashirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuweka mezani maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano Na. 1 ya 1999 na kutunga sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendeleza mashirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 1

Eneo la Muyuni Kikatini Kutumiwa na KVZ

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu angalau kwa dakika moja kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhana Wataallah* aliyeniwezesha hapa kusimama ikiwa huu si ujanja wangu wala maarifa, akili au uwezo wangu, hizi ni pumzi tu za muda nilizoazimwa tu, sijui saa ngapi, dakika ngapi, mwaka gani, sekunde gani nitahitajika.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri ambaye hivi alikuwa ajibu swali hili kwa jitihada zake alizochukua kukaa na wananchi wa Jimbo la Muyuni na kulipatia mwelekeo wa ufumbuzi hili. Hili suala ni la muda mrefu limekuja Baraza la Wawakilishi karibu vikao vitatu lakini kwa bahati limekuja ilikuwa niliondoshe kabla ya kuja humu ndani. Kwa hivyo, naomba swali kuliondosha sasa lisipate majibu na juhudi za Mhe. Waziri aendelee nazo kama alivyozianza, isije ikawa mbio za sakafuni. Baada ya maeleo hayo naomba kuliondosha swali langu.

(Mhe. Mjumbe ameliondoa swali lake)

Nam. 20

Upatikanaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Wanawake

Mhe. Panya Ali Abdalla - Aliuliza:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi kubwa za kuhakikisha wananchi wake wanapata elimu ikiwa ni miongoni mwa haki ya msingi. Kwa kuwa wanawake ni miongoni mwa wananchi wanaopaswa kupatiwa elimu hiyo sawa na wanaume.

a) Je, ni kwa kiasi gani Serikali imezingatia kuwapatia mikopo ya elimu ya juu wanawake.

b) Kila kipindi inapotoka mikopo hiyo ni asilimia ngapi wanapatiwa wanawake na asilimia ngapi wanaume.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 20 ambalo lina (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar imekuwa ikipokea maombi ya mikopo ya masomo katika Taasisi ya Elimu ya Juu kutoka kwa wanafunzi waliohitimu kidato cha sita na wafanyakazi wa Serikali. Idadi ya waombaji wa mikopo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, katika mwaka 2011/2012 idadi ya vijana walioomba mikopo ya elimu ya juu walikuwa ni 1,900 ukilinganisha na maombi 5,200 yaliyopokelewa kwa mwaka 2014/2015.

Utaratibu wa utoaji wa mikopo unazingatia sifa za masomo za maombi na fani ya masomo za kipaumbele kama vile udaktari, uhandisi, ufamasia, walimu wa sayansi, uchumi na fani nyengine. Pia waombaji wenye ulemavu wanapewa kipaumbele kama wametimiza sifa za kujiunga na vyuo. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

a) Bodi ya Mikopo imezingatia kuwapatia mikopo waombaji wanawake. Kwa mfano katika kipindi cha 2012/2013 hadi 2014/2015 idadi ya waombaji wanawake waliopatiwa mikopo ya kusoma shahada ya mwanzo ni 1,793 ukilinganisha na waombaji wanaume ambao ni 1,636 kama ifuatavyo:-

Mwaka	**Wanaume**	**Wanawake**
2012/2013	384	507
2013/2014	564	638
2014/2015	688	648

	1,636	**1,793**

b) Kwa kipindi cha 2012/2013 hadi 2014/2015 wastani wa asilimia ya wanawake waliopata mikopo ya kusoma shahada ya kwanza ni 52.3 ukilinganisha na asilimia 47.7 ya wanaume. Kwa uchambuzi huo Mhe. Naibu Spika, wanawake ndiyo wanaongoza katika kupata mkopo wa masomo ya elimu ya juu.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na pia nitoe shukurani zangu kwa Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake. Kwa sababu nikiwa kama mwanamke nina haki ya kujua wanawake wangapi ni kwa kiasi wamezingatiwa katika upatikanaji huu wa elimu, ikiwa ni haki yao ya msingi hata kidini imeelezwa kutafuta elimu ni faradhi kwa mwanamke na mwanamme.

Sasa nilitaka kujua tu juu ya mikopo ni vipi munawazingatia wale watu ambao wapo wanyonge zaidi ambao wazazi wao ni wanyonge hawana fursa ya kuwasomesha watoto ili na wao wakaweza kuendelea kupata fursa hii ya elimu, vipi munawazingatia hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Katika jibu langu la msingi Mhe. Naibu Spika, nilijibu kama mikopo hii inazingatia vipaumbele. Moja ya vipaumbele ni yale mahitaji ya nchi lakini pia nilizungumza kwa walemavu.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, wakati muombaji anaomba hii mikopo huwa kuna fomu maalum ambayo anajaza. Fomu hii inazingatia mambo mengi lakini moja ya kipengele ambacho kilichomo katika fomu hii ni kutizama uwezo wa yule muombaji na wale ambao tunaona uwezo wao ni mdogo sana na wana sifa za kupata mikopo hiyo Mhe. Naibu Spika, huwa tunawapa kipaumbele cha kwanza.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba na ndiyo utaratibu wa mataifa mbali mbali kwamba mikopo ya elimu ya juu hutolewa kwa mujibu wa vipaumbele vya nchi, na kwa kuwa sasa hivi ulimwengu mzima vile vile una-*advocate gender equality,* na kwa kuwa wanawake wengi inawezekana wengi wanaomba lakini masomo wanayoyataka pengine ni nje ya vipaumbele vya nchi na huku tunataka tu-*balance gender* katika elimu za juu na hatimaye hawa akina mama waweze kuingia katika vyombo vikubwa kama hivi asilimia 50 kwa 50.

Je, ni kwa kiasi gani na kwa sababu hakuna mtu anaweza kupita njia mbili kwa wakati mmoja kuweza ku-*balance gender* pamoja na kuangalia na vipaumbele vya nchi. Je, ni kwa kiasi gani Wizara yake ya Elimu ina-*maintain* hivi vipaumbele vya nchi wakati huo huo wakiwawezesha akinamama na wao pamoja na kwamba wanaomba ni nje ya vipaumbele, muna-*balance* vipi huku katika kutoa mikopo hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini naomba kumjibu swali la nyongeza Mhe. Saleh Nassor Juma kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama ambavyo nilivyozungumza mwanzo kama moja ya sifa za mikopo ni kuzingatia vipaumbele vya nchi, lakini Mhe. Saleh kama alikuwa ananifuatilia sawa sawa kaona ni namna wanawake ambavyo wanaweza kuingia katika fani mbali mbali. Na siyo kama tunawapa mikopo ni kwa sababu ya wanawake tu, ni kwa sababu wanatimiza yale masharti ya kupewa mikopo.

Na nilizungumza hapa wanawake ambao wamepewa mikopo ni asilimia 52.3. Ni kuonesha dhahiri kama uwezo wao wa kuogelea katika fani mbali mbali zinazosomeshwa ndani ya nchi hii ni mkubwa mno.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi ninashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kila mwaka mahitaji ya wakopaji wa elimu ya juu inaongezeka, na kwa kuwa Wizara ya Elimu haina uwezo wa kukidhi haja ya wakopaji wote wanaokopa.

Je, Wizara yako, ina mpango gani wa kushirikiana na Mfuko wa Uhifadhi ya Jamii (*ZSSF*) na Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) ili kuungana na Wizara kwa wasomi hawa ambao tunawategemea Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mohamed Mbwana Hamad swali lake la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, alililozungumza ni kweli kama mahitaji ya wanafunzi katika nchi yanaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mwaka huu wanafunzi ambao walioomba ni karibu wanafunzi elfu tano na zaidi, lakini uwezo wa kuwapatia mikopo tumewapatia karibu wanafunzi elfu tatu mia nne.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia ikumbukwe kama tulipitisha sheria ya Bodi ya Mikopo. Na Baraza hili hili ndiyo ambalo lilipitisha sheria ya Bodi ya Mikopo, na katika kipengele kimoja cha sheria ile inairuhusu Bodi kutafuta *funds* kwa njia yoyote ile. Mojawapo ni hii ambayo umeizungumza Mhe. Mwakilishi ya mikopo ya hifadhi. Kwa hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo tutakaa pamoja tuone kama kipengele hichi kinafanyiwa kazi kama ambavyo sheria ile inavyoruhusu.

Nam. 35

Kuadimika kwa Vifaa vya Uchunguzi wa Homa ya Matumbo Micheweni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Mnamo tarehe 25/8/2014 kumekuwa na taarifa ya vyombo vya habari kuhusu kuadimika kwa vifaa vya uchunguzi wa homa ya matumbo katika Hospitali ya Micheweni na kuathiri wananchi wanyonge wanaofuata tiba katika hospitali hiyo.

a) Sababu za msingi zimepelekea hadi vifaa hivyo kuadimika na wananchi kulazimika kununua kutoka kwa watu binafsi na wasiokuwa na uwezo kukosa huduma.

b) Kwa nini biashara ya vipimo hivyo ifanyike katika maabara ya hospitali hiyo ya Serikali huku wananchi wakiuziwa huduma hizo bila ya kupewa risiti ya malipo ya shilingi 3,000/-.

c) Wizara itachukua hatua gani kwa watendaji wanaochukua vifaa vya watu binafsi kwa kutumia Hospitali ya Serikali kuwauzia wananchi vifaa hivyo jambo ambalo halileti picha nzuri kati ya wananchi na Serikali yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wenye afya njema na uzima na kuhudhuria hapa katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Na. 35 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kulieleza Baraza lako Tukufu la Wawakilishi kuwa vifaa vya uchunguzi vya homa ya matumbo ikiwa pamoja na *reagents* zake vifaa vyake vyengine kama zile *sticks* za kupimia katika hospitali ya Micheweni pamoja na hospitali nyengine zote zipo na wananchi wenye matatizo hayo wanatibiwa na wanaendelea kupata huduma hizo. Hakuna mwananchi anayekoseshwa huduma hiyo, pale panapotokezea kuisha kwa *reagents* ama *sticks* za kupimia vipimo hivyo ambapo hutokana na sababu kuu mbili.

Aidha, kuchelewa sisi kama Wizara ya Afya kupokea kutoka kwa wale wanaotuletea vifaa hivyo ama wafanyakazi wa kituo husika kuchelea kujaza zile fomu za kuomba vifaa vya ziada viletwe, basi pale hutokea mapungufu.

b) Katika hospitali zetu za Serikali hatufanyi biashara za vipimo hususan katika maabara zetu bali wananchi huchangia pale panapokuwa na mapungufu maalum ya huduma fulani katika vituo vyetu hivyo vya afya. Mara nyingi wananchi aidha huchangia moja kwa moja na mifano mengine ipo ambapo wananchi kama vile vituo vya vijijini huchangia kupitia Kamati zao za Shehia. Mara baada ya kuchangia huwa tunawajibika kupatiwa risiti. Wizara inawaomba wananchi kudai risiti zao pahali popote wanapochangia kwa huduma yoyote, na sisi kwa upande wetu wa Wizara ya Afya tunaendelea kushajihisha katika utoaji wa risiti miongoni mwa wafanyakazi wetu wote hususan wale wanaotoa huduma za maabara.

Endapo itatokea kwa mwananchi yeyote kutopewa risiti kwenye huduma aliyochangia, mwananchi huyo anatakiwa atoe taarifa kwa uongozi wa hospitali husika ili tatizo hilo lifanyiwe kazi mara moja.

Tunaomba Mhe. Naibu Spika, mwananchi huyo anapokuwa hajapatiwa risiti yake hata baada ya vitabu vya risiti kufika basi awasilishe ushahidi mbele ya uongozi wa afya wa Wilaya ama uongozi wa *Zonal* ili hatua husika ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimjulishe Mhe. Mwakilishi kuwa tayari wafanyakazi watatu walishapewa barua za onyo kwa kutoa huduma bila ya kutoa risiti wala kurikodi huduma ile katika vitabu vinavyorikodiwa huduma.

(c)Mhe. Spika, nasikitika kusema kwamba Uongozi hauna taarifa juu ya Watendaji wa Wizara kuchukua vifaa vya watu binafsi vya nje, ili kuwauzia wananchi vifaa hivyo, lakini tunatoa wito kwa wananchi kuwa atakapobaini mfanyakazi yeyote wa Wizara ya Afya anauza vifaa vya huduma, hususan vifaa kutoka nje ya hospitali kwa wananchi hao, tunaomba atoe taarifa kwa uongozi haraka iwezekanavyo, na ikithibitika mfanyakazi huyo kuwa kweli ametenda kosa hilo, basi wizara itamchukulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizopo bila kusita.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi Wizara ya Afya pamoja na viongozi wake mbali mbali, wanapotaka kuchukua hatua ushahidi hukosekana. Baada ya mlalamikaji kusema basi hawezi kutoa ushahidi au ameshasamehe hizo fedha au kuona muhali katika kuliwasilisha lalamiko lake.

Hutokea baadhi ya wakati pale ambapo tunapokea malalamiko kama haya, na katika ufuatiliaji wake tunagundua kwamba Kamati za Shehia zimekuwa zikitoa mashirikiano yao makubwa kabisa pale panapotokea upungufu, hususan wa *reagents* au *sticks* za kupimia damu ama mkojo, au huduma za afya nyengine za maabara ambapo wafanyakazi wa maabara hukaa pamoja na uongozi wa Kituo cha Afya na Kamati za Shehia na kuwajulisha mapema kuwa siku fulani zile *sticks* zitakwisha na bado hazijapokelewa kutoka Bohari Kuu ya Madawa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nieleze kuwa vituo vingi hivi sasa vinashajihishwa na tayari vimeshashajihika kuwa ni vituo vya vijijini vya jamii moja kwa moja, badala ya kuwa kama hapo zamani kujulikana kama vituo vya Wizara ya Afya. Ni kweli vituo vya Wizara ya Afya, lakini jamii hushajihishwa zaidi kujihisi kwamba vituo vile ni vya kwao, kwa hivyo kunakuwepo na mashirikiano makubwa kati ya jamii pamoja na uongozi wa vituo katika kutoa huduma hizo moja kwa moja, ambapo kuchangia kwa huduma hizo kunapelekea mashirikiano baina ya wafanyakazi wa kituo pamoja na Kamati za Shehia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokuwa na afya kama wizara yake anayoiongoza kutokuwa na afya, namuuliza. Mimi sio mkamilifu, mkamilifu ni mmoja tu *Allah Subhanahu Wataalla*, lakini sijaribu kuuliza swali hasa la Wizara ya Afya, kama sijalifuatilia kwa umakini.

Mhe. Naibu Waziri utakuwa tayari kujiuzulu pindipo nikikukutanisha na watu waliokutana na upepo huu, harufu hii na dharuba hii; waliochukua vipimo vyao kuelekea hadi Hospitali ya Wete

kwenda kupima. Uko tayari kujiuzulu pindipo nikikukutanisha na wananchi hawa waliopata harufu hii.

Kwa kuwa Wizara ya Afya huduma zake zimekuwa kama upele wa msimu, mara moja hutokea dawa nyengine ikapatikana na nyengine haipatikani, ni sababu gani na mambo mengine hayataki hata bajeti. Juzi tumeshuhudia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwenda kuangalia usafi nayo inataka bajeti. Hamko tayari kuwatumikia wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, hapa hakuna suala la kujiuzulu au la kutokujiuzulu kutokana na mapungufu yanayotokea madogo kama hayo ya afya.

Mimi nimeeleza katika jibu langu hapo awali na ninaamini Mhe. Jaku Hashim Ayoub ufahamu wake ni mzuri sana. Nimeeleza hivi; kwamba haya mapungufu yanatokea ya vifaa vya maabara, huwa yanatokea kwa baadhi ya wakati na yanatokea kwa sababu kuu mbili.

Sababu ya kwanza ni mfanyakazi wa kituo husika kuchelewa kujaza zile fomu za kuombea dawa katika mfumo huu wa *ZILS*, hata jimboni kwako Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mhe. Naibu Spika, limeshawahi kutokezea tatizo hilo, lakini hutatuliwa ndani ya muda mfupi baada ya kugundulika tu na zile fomu kujazwa.

Sababu ya pili, katika jibu hilo hilo Mhe. Naibu Spika, hutokea wakati mwengine *sticks* zile za kupimia damu, hususan hii ya kisukari zinapungua. Panapotokezea na upungufu huo, basi wale wafanyakazi huijulisha Wizara ya Afya na kukiwa kumechelewa kutolewa huduma hiyo, basi vile vituo vya afya vinavyotoa huduma hizo za maabara, hukaa moja kwa moja na Kamati ya Shehia na wao wenyewe wanakubaliana katika kuchangia huduma hizo ili wananchi waendelee kupata huduma hizo, na mara tu vifaa hivyo vinapopatikana kutoka wizarani kupitia bohari kuu, basi vifaa hivyo vinawasilishwa. Suala la kujiuzulu hapo Mheshimiwa halipo kabisa.

Kwa upande wa pili kaeleza mfano ule wa juzi uliotokea pale kwa ile karo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kujaa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kufika pale wizarani. Naomba nieleze hivi na nitalirudia tena hili na naomba ufafanuzi huu ueleweke kwa uwazi kabisa.

Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipojengwa mnamo mwaka 1922 ilikuwa inahudumia *population* ya watu chini ya laki tatu, hospitali ile hivi sasa inahudumia karibu *population* yote ya Zanzibar ambayo ni watu milioni 1.3 ni karibu mara nne zaidi. Kwa hivyo, huduma zile huwa zinazidiwa kwa ukubwa wa zile *pipes* zinazopitisha maji machafu, kutokana na idadi ya vyoo kuongezeka ndani ya hospitali, kutokana na idadi ya majengo mbali mbali pamoja na majengo mapya yanayoendelea kujengwa. Jengo ya *neurosurgery* na majengo mengine yameongezeka na inatumia *system* ile ile ya *CUH.*Kule chini bado hakujaongezwa mtanuko wa *pipe* kusema kwamba sasa huduma hizi zilikuwa zinatolewa kwa watu 300,000 sasa milioni 1.3 kwamba zile *pipes* zimeongezeka, hapana.

Jengine kubwa zaidi, hivi sasa tayari wanamazingira wanakataza huduma zile zisiende moja kwa moja pwani kama ilivyokuwa hapo awali. Tunajua nchi yetu ina utalii na utalii unavutia zaidi kwenye hizi fukwe zetu za bahari, tunajua kwamba fukwe ya kuanzia hapa maeneo ya Mbweni

hadi Serena na kupita kwenda mbele kwenye hoteli mpya iliyofunguliwa ya Hayat, zinatumika kitalii. Kwa hivyo, huduma zile hivi sasa zinakwenda kwenye mashimo maalum ambayo mara tu yanapojaa huja kutolewa, yaani mashimo yale kutapishwa. Sasa linapotokezea tatizo lile, kwa kweli lile tatizo lilichukua masaa matatu tu, lakini ndani ya masaa matatu waandishi wa habari walifanya kazi yao vizuri wakaliripoti lile suala na ndani ya masaa matatu lilipotokezea tatizo lile basi limeweza kutatuliwa kwa kuomba gari la kuweza kuja kuchota ule uchafu.

Tatizo lililotokezea siku ile ni kwamba yale mashimo yalijaa kabla ya lile gari kuja kuchukua ule uchafu. Sasa hayo huwa yanatokezea, lakini tutajitahidi kwa upande wetu kwa wizara kwamba tatizo hilo lisitokezee kwa kujenga utaratibu maalum wa kwamba kila linapotokezea tatizo hilo, basi huduma ile ya kuja kutapisha ifanyike kabla ya yale mashimo kujaa.

Lakini pili, kwa majengo haya mapya yanayokuja ya *ORIO*, basi tutaandaa utaratibu vile viwanda vya madawa pamoja na eneo lile la Mapinduzi Mpya kuendelea huko mbele, tutaandaa utaratibu maalum wa mashimo yake kule kuwa tofauti na upande huu. Naamini *Inshaallah* tatizo hilo halitotokezea tena.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Enhe, utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha 37. Nilichomuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa nini Wizara ya Afya huduma zake zimekuwa kama upele wa msimu, dawa moja inapatikana na nyengine haipatikani, ni lini tatizo hili litamalizika. Nafikiri Mhe. Waziri anaweza kuinuka akasaidia kujibu swali hilo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri majibu, hilo ulilichacha.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, sikuliacha kwa sababu upele wa msimu mimi siujui na sikuuelezea humu, wala siufahamu upele wa msimu, labda ningepata taaluma ya upele wa msimu ningeweza kuelewa. Ila ninachotaka kusema kuhusu upande wa madawa, madawa tumehamia katika mfumo mpya na yeye Mhe. Jaku Hashim anajua, kwa sababu tulishawahi kumjulisha mfumo huo kwa vituo vyake vilivyokuwepo Muyuni, kwa sababu navyo viko katika mfumo wa *ZILS*.

Baada ya kuanzisha mfumo huo mpya wa *ZILS*, hapo awali ilikuwa madawa yanapelekwa moja kwa moja katika vituo kila yanapopatikana yanagaiwa katika vituo kutokana na idadi ya watu waliokuwepo kwenye maeneo hayo, lakini katika mfumo wa *ZILS*, unaitwa *pulling system,* vituo huandika wao hujaza zile fomu kusema wanahitaji madawa yepi. Bohari Kuu yetu sasa hivi ina vifaa vya kutosha katika ile *essential*, narudia tena katika *essential drugs*, yaani yale madawa yaliyokuwa muhimu nchini yapo pale katika bohari kuu na mimi nitamuomba kama atakuwa na muda twende pamoja tukafanye ziara pale bohari, ili ajiridhishe yeye mwenyewe na kuthibitisha kwamba dawa hizo zipo.

Pale zinapochelewa kuletwa zile fomu za *ZILS* kutoka huko vituoni, basi pale ndipo hutokea mapungufu hayo, lakini sio kwa upande wa bohari, bali ni kwa upande wa kituo kwa kupata dawa zile kwa wakati. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya maelezo marefu ya Mhe. Naibu Waziri, napenda niongeze majibu kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa upelekaji madawa katika vituo unafuata haja ya vituo wenyewe, utaratibu uliokuwa ukitumika nyuma ulikuwa madawa yanapelekwa kwa kadiri *store* ilivyo, lakini ikaonekana ni upotevu wa fedha na pia madawa yanaweza kufikia kuharibika kabla hayajatumika.

Kwa hivyo, wataalamu wameanzisha utaratibu mpya ambao vituo wenyewe ndio wanaoleta *list* ile kwenye bohari kuu kwa madawa ambayo yanatumika zaidi kwenye vituo vile. Baada ya kuleta *list* ile ndio bohari kuu inapeleka madawa kutokana na matumizi ya dawa zile, ili zisije zikaharibika au kutumika vibaya. Kwa hivyo, ikitokezea upungufu ama itakuwa dawa zile zimetumika zaidi ya kiwango au itakuwa hawakupeleka kwa taratibu maalum, lakini ukosefu wa baadhi ya nyenzo na madawa kwa ujumla, inasababishwa na bajeti ndogo ya wizara.

Kwa hivyo, kuanzia leo tunaipigia debe Wizara ya Afya kwamba wakati wa kupitisha bajeti wajue kwamba watuongezee bajeti. Hivi sasa *WHO* imetoa kiwango cha nchi zinazoendelea katika ulimwengu kuwa na bajeti isiyopungua dola 60 kwa kila mtu kwa ajili ya afya. Hivi sasa sisi tuko katika dola 29 kwa kila mtu pamoja na misaada tunayoipata. Kwa hivyo, ni karibu nusu ya fedha ambazo zinahitajika ya kiwango cha chini kilichowekwa na *WHO*. Kwa hivyo, kukosekana kwa dawa, sio tatizo tu la wizara, lakini ni tatizo vile vile la bajeti ndogo inayowekwa.

Kwa hivyo, ili kuongeza hali hiyo, tunaliomba sana Baraza litoe mapendekezo yake ya kukuza uchumi wa Zanzibar, ili na hali ya afya ikuzike. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi moja ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake marefu na mazuri yenye mashiko. Katika majibu yake alisema kwamba serikali haifanyi biashara bali wananchi huomba kuchangia huduma ambazo huwa ni bure, na mimi nakubaliana naye kwamba serikali haifanyi biashara. Katika maelezo yake amesema kwamba mwananchi anayetozwa fedha atoe taarifa

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe subiri. Mhe. Jaku Hashim na Wajumbe wenzako wakiuliza uwasikilize. Endelea.

Mhe. Nassor Salim Ali: Na katika majibu yake mengine amesema kwamba mwananchi anayetozwa fedha atoe taarifa sehemu husika. Swali langu ni kwamba katika kipindi cha mwaka 2010 mpaka mwaka 2015 matukio yapo, na kama yapo ni matukio mangapi na ni hukumu gani ambayo imetolewa kama yametokea kwa yule ambaye ameyafanya kutoza fedha kwa wananchi ambao ni walipa kodi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza kabisa nitalianza hili la pili kama kuanzia mwaka 2010 hadi leo ni wafanyakazi watano waliopewa onyo moja kwa moja, kuhusiana na masuala ya risiti, masuala ya kupokea fedha kwa huduma ya afya, masuala ya kutoa huduma kwa kupokea fedha bila ya kutoa risiti, ni wafanyakazi watano waliopewa barua za onyo na wengine kuchukuliwa hatua ya kuhamishwa kutoka kituo kimoja kwenda chengine. Baada ya kupewa barua hizo za onyo, tumeona kwamba *trend* ile wamejirekebisha tayari na hivi sasa hilo tatizo halipo.

Pili Mhe. Naibu Spika, hutokezea tatizo wakati mwengine mgonjwa akafika pale. Huu ni mfano ambao niliuona kituo kimoja cha pale Tazari Nungwi, ilikuja kesi kama hiyo kwamba mfanyakazi kaomba fedha 35,000/-, zikatolewa fedha zile mfanyakazi yule akaenda kununua *stick*. Bahati nzuri mimi nilihusika moja kwa moja, siku hiyo tulipofika kwenye ziara ndio kesi hiyo ikawepo kituoni, kwa hivyo na mimi nikashiriki kwenye kuisikiliza, kama msikilizaji tu sio mtoaji hukumu.

Katika kesi ile jambo moja nililojifunza ni kwamba yule mfanyakazi alipoona zile *sticks* za kupimia damu za kisukari hazipo, ambapo damu ya kisukari hupimwa kwa wazee na wale wagonjwa waliokuwa na maradhi ya kisukari, lakini pia *sticks* hizo huwa zinatumika kwa mama wajawazito kwa sababu sukari zao huwa zinapanda na kushuka, hususan wanapopata matatizo ya *pressure* na kuvimba miguu wakati wa ujauzito.

Sasa kesi ile ilipokuwa ikiendelea pale, yule mfanyakazi akajitetea, akasema mimi ni bora kujibu kwamba huduma hiyo haipo au kujibu kwamba *sticks* zimetuishia au kutafuta mbinu ya kupata kununua zile *sticks*, baada ya watu kuchangia kumrudishia mwenyewe fedha hizo. Sasa hapo mfanyakazi yule ametumia ubunifu, ni katika Kituo cha Tazari alitumia ubunifu, kwamba kukusanya zile fedha zote. Kitu kilichomsaidia ni mambo matatu yafuatayo.

La kwanza kabisa, alipokwenda kununua zile *sticks* alipatiwa risiti, alikwenda kununua *Shamshu Pharmacy* akawa na risiti akaitoa pale kwamba nimenunua kwa kiasi fulani.

Pili yule aliyetoa zile huduma walikubaliana kwamba fedha zake atarudishiwa kila baada ya mtu mmoja kuchangia zile *sticks*.

La tatu, amefanya ubunifu kwamba kwa sababu zile *sticks* zimechelewa kutoka bohari kuu kuwasilishwa pale na zile *sticks* hazimo katika ile *essential drugs,* ni dawa za ziada, kwa kuwa ameona zimechelewa ili huduma nyengine za afya pale kituoni ziendelee na mtu asikose kupimwa ile damu kwa ajili ya kupatiwa matokeo, basi ameona hilo jambo lifanyike.

Sasa kwa upande wetu Wizara ya Afya hatua iliyochukuliwa ni kwamba yule mfanyakazi ametakiwa moja kwa moja azungumze na uongozi wa kile kituo cha afya, awe anarikodi zile *transaction,* yaani kwenda kununua na ile risiti na pale kipato kinachopatikana kirekodiwe ili mwenyewe aweze kulipwa na zile fedha zinazobakia ziingie serikalini. Utaratibu huu ni wa muda mpaka tatizo litakapokwisha, ulitumika hapo wakati huo kwa muda tu mpaka tatizo lilipokwisha.

Lakini kitu ambacho sisi hatukumchukulia hatua mfanyakazi yule tuliona alifanya ubunifu kwa moyo wake wa kizalendo, kwamba wagonjwa waendelee kupata huduma kwa ule ule mchango mdogo wanaoutoa waendelee kupata ile huduma.

Kwa bahati nzuri Sheha wa Shehia hiyo alikuwepo, na Kamati ya Shehia baada ya hapo iliandaa utaratibu maalum, kwa sababu kile kituo wanakihisi ni cha kwao kile cha Tazari sio cha Wizara ya Afya. Waliandaa utaratibu maalum kwamba popote panapokuwa na mapungufu, wana bajeti yao ambayo kile kituo kitaendelea kuhudumiwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kutoa pongezi kwa Wizara ya Afya kwa kutuongezea wodi za kulazwa wagonjwa kule Hospitali yetu ya Micheweni.

Kwa kuwa hospitali ya Micheweni inachukua idadi kubwa ya wananchi wanaohudumiwa na Hospitali ya Micheweni, na kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kama sababu zinazotokea za kusababisha kukosekana kwa hivi vifaa, aidha vya kuchunguzia damu ama kuchunguza hiyo homa ya matumbo kunasababishwa na mtiririko wa ugawaji wa dawa yaani mfumo uliopo wa sasa hivi, sasa mimi kwanza napongeza mfumo huo uliopo.

Lakini namuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa kituo kile kinahudumia watu wanaotoka sehemu mbali, na kwa kuwa rufaa yetu sisi ni mbali kufuata hospitali Wete, Chake na Mkoani na vile watu ni wengi. Je, haoni kama kuna haja ya kuunda kamati ya kuchunguza huo mtiririko wa madawa ikajua hapa kama dawa zimeshapungua ziongezwe, kuliko kuacha mpaka dawa zikakosekana ikabidi wananchi wakose huduma na wafuate mbali, kama hivyo ndivyo, je, ni lini ataunda kamati ya kuangalia kama dawa zimepungua pamoja na mtiririko wao walionao ili zisikosekane kabisa wananchi wakapata usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kamati huundwa pale panapokuwa na tatizo ambalo halijajulikana, ama kuna uchunguzi maalum wa tatizo lile unaendelea. Kwa kuwa Mhe. Waziri alisimama leo na kusema kwamba tatizo linajulikana, tatizo ni kwamba ile kasma ya bajeti mgonjwa mmoja kwa wastani wa kutibiwa katika nchi zinazoendelea anahitaji dola sitini amelieleza hapo Mhe. Waziri. Na hivi sasa bajeti ya Serikali *allocation* yake kwa zile bilioni 24 tunazozipata zinakuwa ni dola 28 mpaka 29 kwa mtu mmoja.

Kwa hivyo hapo kuna kasoro ya takriban ya dola 31 ambayo mwananchi anaikosa katika kupatiwa huduma za afya, kwa hivyo hilo ni tatizo la kibajeti. Kwa hivyo hakuna haja ya kuunda kamati kwa sababu tatizo tunalijua tayari kwa nini tuunde kamati wakati tatizo tunalijua, ndio maana Mhe. Waziri katika kauli yake amesisitiza leo kwamba suala la *allocation* ya bajeti katika Wizara ya Afya ni muhimu, na hata amefika kusema kwamba zile njia kuu za kuzalisha uchumi au kuingiza uchumi zifanyiwe kazi zaidi ili bajeti ya Wizara ya Afya iweze kuongezeka na wananchi wa Micheweni pamoja na wananchi wengine wote wa maeneo yote katika Kisiwa cha Pemba na Unguja waweze kupata huduma hizo za afya.

Kwa hivyo tatizo Mheshimiwa ni la kibajeti, sasa hivi zaidi upande wa bohari kuu ya madawa tayari wao wameshatia *system* mpya ya kompyuta. Bohari kuu imeshajengwa na Mungu akitujaalia hivi karibuni nyengine itaanza kujengwa kwa Pemba, kwa hivyo tatizo hilo litakuwa halipo.

Na naomba nimjulishe Mheshimiwa Hospitali ya Micheweni sasa hivi inashindana na hizo Hospitali nyengine ulizozitaja za Wete, Chake, labda hiyo Abdalla Mzee Mpya itakayojengwa labda itakuwa kubwa zaidi. Kwa hivyo madamu huduma hizo zinashindana inawezekana siku moja mtu wa Chake akaja kule Micheweni kutokana na huduma zinavyoendelea kutolewa vizuri. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Katibu kabla ya kuendelea naomba niwaarifu Waheshimiwa Wajumbe kwamba tukimaliza masuala mawili yaliyosalia Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo atafanya majumuisho ya Mswada wake na kupitisha vifungu, sasa vifungu vinapitishwa kwa *quorum* ya Baraza naona Waheshimiwa wengi wanatoka nje, kwa hivyo naomba sasa hivi chai tusinywe mpaka tupitishe vifungu halafu mtatoka taratibu kwenda kunywa chai, vyenginevyo kazi yetu tutashindwa kuifanya naomba sana.

Nam. 63

Akinamama wa Kusini Pemba Kutafutiwa Soko Nje ya Pemba

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza :-
Tumeona akinamama wa Mkoa wa Kusini Pemba wajasiriamali wamefunguliwa soko la Jumapili, pale Chake-Chake na wanatengeneza bidhaa nzuri tu, lakini soko lile halikidhi viwango vya manunuzi kwa kuwa wateja ni kidogo mno.

Je, Serikali haioni iko haja ya kuwatafutia soko jengine nje ya Pemba ili akinamama hao wafaidike na matunda ya jasho lao.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 63 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nataka nikiri kuwa jukumu la kuwatafutia masoko wajasiriamali wanaozalisha bidhaa zao hapa ni mojawapo ya majukumu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii Vijana Wanawake na Watoto, basi imeweza kuanzisha soko hilo la Jumapili ambapo lilianza rasmi tarehe 30 Novemba, 2012.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hilo Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pia huwa inaandaa na kuratibu ushiriki wa wajasiriamali wa Zanzibar katika maonesho mbali mbali ya kibisahara na matamasha ya kibiashara ndani na nje ya nchi; ikiwemo kuratibu na kuwawezesha kushiriki katika maonesho ya saba saba yanayofanyika kila mwaka pale Dar es Salaam.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Je, Mhe. Waziri, Wizara yako haioni kuwa kuna haja ya kuwapatia wataalamu kinamama hao katika suala zima la vikundi vya ushirika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ni jukumu la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuwapatia wataalamu wajasiriamali na wazalishaji wadogo wadogo na mpango huo upo katika idara husika Idara ya Viwanda kuwapatia wataalamu na kuwapatia mafunzo katika kuzalisha bidhaa zilizo bora ili ziweze kukubalika katika soko.
Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu sana, naomba nimuulize swali dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa akinamama katika Kisiwa cha Pemba wamejikita sana katika mambo ya ujasiriamali katika utengenezaji wa mambo kama vile mikoba ya ukili, kutengeneza chakne na kusindika viungo. Na kwa kuwa Pemba kwa kweli soko la mambo haya hapana, na kwa kuwa sehemu za kama kule Mayotte, Anzwani sehemu za Ungazijani kule wanapenda sana mikoba hii ya ukili katika kufanyia shughuli zao.

Na kwa kuwa sehemu kama Taj Mahal pale India wanapenda sana mambo ya viungo hivi kwa mfano achari ya ndimu, ambazo wanazalisha sana pale Pemba. Je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri katika makongamano ya nje ambayo wanasema wanakwenda kufanya makongamano ya nje, atafuatana na akina mama kutoka sehemu za Micheweni, kutoka sehemu za Ndagoni pale, Wawi pamoja na Muwambe ili kinamama wale waende kule kuona jinsi masoko yanavyokwenda, kusudi na wao waweze kupata soko la nje badala ya kuendelea kukaa pale kuuzauza katika jua kali namna ile ambayo mimi nawaonea huruma sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tunaratibu na kuwawezesha kushiriki katika maonesho na matamasha mbali mbali ya kibiashara. Wanaposhiriki katika maonesho hayo *mathalan* watakaposhiriki Dar es Salaam lakini pia katika masoko yao ya Jumapili pale Chake Chake Pemba basi wafanya biashara mbali mbali wanapovutiwa na bidhaa zao zile huwapa oda ya kuzalisha bidhaa zao, au huwaalika pia kushiriki katika maonesho nje ya nchi, na hilo limeshafanyika kwa vikundi kadhaa, wameweza kushiriki hadi katika maonesho yaliyofanyika Korea mwaka juzi.

Kwa hivyo, Wizara ya Biashara inafanya hilo na inaendelea kuwashirikisha, muhimu ni kwamba bidhaa zao ziweze kufikia viwango vinavyokubalika na wafanya biashara hao.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, ndani na *Sunday Market* yaani soko la Jumapili la Chake Chake, lakini tulikuwa na soko la Jumapili katika maeneo ya Kisonge ambapo pamejengwa mnara.

Swali langu ni kwamba baada ya kujengwa mnara ule lile soko la pale wamepelekwa wapi, na vile vile katika swali la pili ni kwamba ulimwenguni kote *Sunday Market* yaani soko la Jumapili huwa linafanyika katika sehemu ya mijini, maana katikati ya soko kule mijini.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba *Sunday Markets* hizi zinafanyika sehemu ambazo kuna biashara ili wajasiriamali wetu waweze kufanya biashara yao kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ni kweli katika siku za nyuma pale Kisonge katika Jimbo la Rahaleo palikuwa panatumika siku za Jumapili wafanyabiashara wadogo wadodo kuonesha bidhaa zao kwa ajili ya kutafuta soko na kuuza bidhaa zao.

Na ni kweli kwamba pale sasa hivi hakuna tena soko hilo la Jumapili, lakini nimtoe wasi wasi Mhe. Nassor Ali Salim, kwamba suala hili Wizara tunaendelea kulifanyia kazi kutafuta eneo zuri ambalo litakuwa kivutio, tunafahamu kwamba katika nchi zilizoendelea hata katika barabara kuu hata Dar es Salaam siku hizi huwa wanafunga barabara zile ili kuwaruhusu wafanya biashara wadogo wadogo waweze kuuza bidhaa zao kwa wakati maalum kwa siku za Jumapili.

Sasa tumelizingatia hilo na tunalifanyia kazi, tayari tumeshaanza kudhani kwamba kuna maeneo kama pale Baraza la Wawakilishi la zamani barabara ile ya Kikwajuni tunalizingatia hilo kama itawezekana, lakini na maeneo mengine ili tuweze kulifanikisha hilo kwa wazalishaji wetu wadogo wadogo Mhe. Naibu Spika.

Nam. 48

Bei Kubwa ya Kuungiwa Umeme Vijijini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub **-** Aliuliza:-

Wananchi wengi hasa wa Jimbo la Muyuni wamekuwa wakiomba kupelekewa huduma ya umeme, lakini bei wanazopewa za kuungiwa umeme huo huwa kubwa.

Je, kwa nini Serikali haipunguzi bei ya kuungiwa umeme kwa wananchi hasa wa vijijini ambao vipato vyao ni vya chini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati **–** Alijibu:

Mhe Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 48 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mwakilishi kuwa Serikali tayari imeweka mpango maalum wa kuwasaidia wananchi wake wenye kipato cha chini katika ununuzi wa umeme, bei zake ziko chini sana kulinganisha na watumiaji wenye kipato cha kawaida.

Kwa upande wa gharama za uungaji wa umeme bei zake zinatokana na utumiaji wa vifaa ambavyo vingi huagizwa na kununuliwa kutoka nje. Hata hivyo umewekwa mpango wa kuweza

kuwasaidia wananchi hasa wa vijijini ambao hawamudu kulipia kwa gharama za muombaji kwa mkupuo mmoja waweze kulipa kwa njia ya mkopo. Na utaratibu huo tayari umeanza kutumika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri ya kukatisha tamaa na kuvunja moyo, na ushahidi upo nitamthibitishia mimi kwa wananchi wangu wa Paje, wamechangishwa pesa na zimechukuliwa na washalipa, na kama yuko tayari mimi nitamthibitishia leo twende mguu kwa mguu na huduma hiyo haipatikani.

Kwa kuwa Serikali iliyopita iliahidi kutoa mkopo kwa wananchi wanyonge juu ya gharama za uungaji wa umeme Unguja na Pemba, mradi huu umedhaminiwa na Waziri dhamana wa awamu ya sita, leo umefikia wapi wananchi bado wanaendelea kuteseka, suala hili ikiwemo wananchi wangu wa Paje pesa wamechukua sijui kama zinazaa riba zile au vipi huduma hiyo haipatikani. Baada ya hapo suala la pili la ziada, kwa kuwa wananchi wengi wanashindwa kumudu, tutaupunguza vipi umasikini huo na umeme huo ukawa umebaki kwenye nguzo tu, lengo kuwafikia wananchi au kubaki kwenye nguzo za umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba Wizara yangu kupitia Shirika la umeme iko tayari kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini kwa ajili ya kuwafanyia mkopo wa kuwaunganishia umeme wananchi hao.

Sasa Mheshimiwa Mwakilishi kama wapo wa Paje ambao wamefika Wizarani na huduma hiyo bado hawajapelekewa basi namuomba Mhe. Mwakilishi aje Wizarani na tutashirikiana, tutalifuatilia suala hilo na tutahakikisha kwamba wananchi hao wanaunganishiwa huduma hiyo.

Suala la pili la kuhusu kuondoa umasikini. Ni lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha wananchi wake wote wanaishi vizuri na wanafanikiwa katika huduma zote ambazo wanazihitaji.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, hawa watu hawajaomba msaada wameshalipa pesa na muda ni mrefu, si wajibu wao au wangu mimi, ni wajibu wa Wizara yake. Lini atakwenda kuwapelekea, hawaombi msaada, washapeleka pesa zao kwenye shirika sio kama msaada huo, si wajibu wangu, majibu ya kumueleza tu hapa alifuatilie, na hizi ahadi za Wizara hizi zimekuwa ndefu hakuna utekelezaji.

Ni lini utawapelekea umeme? Nataka kusikia kauli yako Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Jaku nilivyofahamu mimi kwamba anasema pesa zishapelekwa, wewe kama kiongozi wao na watu unawajua mwende Wizarani mkashirikiane limalizwe hilo suala. Siku utakayoamua wewe kama leo, kesho, keshokutwa wao wako tayari hata leo mkitoka hapo nendeni na majina ya watu wako na fedha zilizokusanywa hilo jambo liishe, ni wewe mwenyewe kujiweka tu sasa hivi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaleta umeme kwa ajili ya kuwapunguzia usumbufu wananchi, na pia umeme unasaidia wananchi kupata kipato chao zaidi, kwa sababu umeme unasaidia mambo mengi katika nchi.
Sasa kwa kuwa huduma ya umeme imefika katika Wilaya ya Micheweni na hasa katika Jimbo la Micheweni, na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni wanafuata masafa makubwa kufuatilia ulipaji wa umeme, na kwa kuwa umeme sasa hivi ni wa tukuza.

Je, Mheshimiwa tumepeleka maombi yetu mara nyingi sana kuwa tunaomba tuwekewe kituo karibu cha kulipia umeme, mwananchi anakuwa anapoteza gharama ya pesa nyingi kuondoka kwenda kulipa umeme Chake chake au Wete.

Ni lini Wizara yake itaweka kituo katika Wilaya yetu ya Micheweni ili kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kwenda kulipa umeme Chake, kwa sababu wanalazimika kupata gharama nyengine za nauli, ni lini hasa suala hili litapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme lengo lake kuu ni kuwafanikishia wananchi na wateja wetu wote kupata huduma hiyo kwa wepesi, hususan katika suala la malipo. Na katika kulishughulikia hili tayari Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imeshirikiana na mtandao wa simu wa ZANTEL ili wananchi waweze kulipa huduma hiyo kupitia pale walipo. Na vile vile Shirika la Umeme tayari limesambaza vituo vingi vya ulipaji wa huduma hiyo katika vijiji vingi. Kwa hivyo namuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba katika eneo lake la Micheweni tunajiandaa na *Isnhallah* tukijaaliwa tutawapelekea kituo cha kulipa huduma hiyo.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni ya 2015 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa kufanya majumuisho katika Mswada wetu. Aidha nawashukuru sana Wajumbe wote wa Baraza lako kwa namna ambavyo walivyochangia Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wote waliochangia kwa hakika wamedhihirisha namna wanavyokerwa kuona kwamba mila, silka na utamaduni wetu unavyopotea. Nimefurahi kusikia kwamba Wajumbe wote wa Baraza hili ni waendelezaji wazuri wa utamaduni wetu, na kwamba wanajivunia utamaduni wetu. Jambo hili limetupa moyo sana kwa niaba ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu umechangiwa na Wajumbe 16 wa Baraza lako Tukufu na naomba niwatambue kama hivi ifuatavyo:

1) Mhe. Mlinde Mabrouk Juma

2) Mhe. Mohammed Haji Khalid
3) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4) Mhe. Wanu Hafidh Ameir
5) Mhe. Farida Amour Mohammed
6) Mhe. Raya Suleiman Hamad
7) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
8) Mhe. Panya Ali Abdalla
9) Mhe. Mgeni Hassan Juma
10) Mhe. Hija Hassan Hija
11) Mhe. Saleh Nassor Juma
12) Mhe. Ali Salum Haji; na
13) Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Waliochangia kwa maandishi ni:

14) Mhe. Asha Abdu Haji
15) Mhe. Salma Muhammed Bilal; na
16) Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru wote ambao wamechangia, na kwa kweli michango yao yote ilikuwa ni michango ya kujenga.

Mhe. Naibu Spika, silka mila na utamaduni wa nchi ndio utambulisho wa nchi. Ikiwa nchi haina utamaduni wake, nchi hiyo ni sawa sawa na haipo. Wazanzibari dunia nzima hadi leo tunatambulika kwa upole wetu, kwa heshima yetu, kwa uaminifu wetu, kwa imani zetu, kwa mavazi yetu, kwa ngoma zetu, kwa muruwa wa mazungumzo yetu, kwa ukarimu wetu na tabasamu zetu na zaidi kwa kujiamini kwetu. Huo ndio utamaduni wetu unaotutofautisha na jamii nyengine. Mambo hayo ni lazima tuyaenzi, tuyalinde maana huo ndio uzanzibari wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, katika uchangiaji wa Mswada huu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu pamoja na mambo mengine walizungumzia kwa ujumla mambo manane makubwa yafuatayo; ambayo nakuomba kwanza uniruhusu niyatolee maelezo ambayo baadaye ndiyo nimjibu Mheshimiwa mmoja mmoja.

Jambo la kwanza lililozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe kwa upana sana ni kwamba utamaduni wetu unapotea kwa nguvu. Utamaduni wa nchi ni mfumo wa maishi unaohusiana na mila, desturi na imani katika wakati maalum.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na michango ya Wajumbe ya kwamba utamaduni wetu unapotea. Kuna sababu nyingi miongoni mwao ya kwanza kubwa ni malezi yetu sisi wazazi. Hili tumelipuuzia kidogo na sasa linatugharimu. Ushauri wangu ni kwamba sisi kama wazazi sote kuhakikisha kwamba tunawalea watoto wetu katika misingi ya silka, mila na utamaduni wetu. Hili ni letu sote, na lazima kila mzazi na mlezi ahakikishe hili analifanyia kazi.

Pili ni kutokana na udhaifu wa sheria zilizopo na hii ndio sababu iliyoifanya serikali kuleta Mswada huu mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe wamelizungumza kwa upana sana, mavazi yanayovaliwa yanaharibu utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Spika, suala la mavazi limezungumzwa sana na Waheshimiwa karibu wote. Jambo hili nakubaliana Waheshimiwa Wajumbe kwamba lina mchango muhimu katika kutambulisha utamaduni wa nchi. Ni kweli mavazi yanayovaliwa yanakirihisha, yanaudhi na yanaondoa muruwa wa nchi yetu.

Katika suala la mavazi yamegawika sehemu tatu. Moja ni mavazi yanayovaliwa na wenyeji wenyewe Wazanzibari. Haya kwa kiasi bado yanaridhisha ingawa vijana wetu wameanza kuiga kwa wengine. Naomba tusaidiane wazazi kutoa zaidi taaluma kwa watoto wetu madhara ya kuiga mavazi ya watu wengine.

Pili mavazi yanayovaliwa na jirani zetu wanaohamia ama kwa kazi au kwa matembezi. Hapa napo tuna mtihani kidogo maana huvaa kama wanavyovaa katika nchi zao na maeneo yao wanayotoka ya asili. Jambo hili tunalizingatia.

Athari ya tatu ni mavazi yanayovaliwa na wageni wetu watalii. Hapa napo pana mtihani kwamba Makampuni yanayoleta watalii hawajatoa taaluma ya kutosha kwa wageni wetu kujua utamaduni wa mavazi ya nchi yetu. Watalii wakipewa taaluma nzuri huwa hawana tabu kufuata, na uuzaji wa nguo za Kizanzibari itakuwa ni moja katika shughuli muhimu za kiuchumi kwa utalii.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili tunalifanyia kazi, kuna *decree* ya mavazi ya mwaka 1971 ambayo utekelezaji wake kwa kiasi fulani umepitwa na wakati. Wizara yangu tunashirikiana na Tume ya Kubadilisha Sheria iliyopo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuangalia namna ya kurekebisha kwa kushirikiana na wahusika wote. Naomba tupewe muda zaidi wa kukamilisha kazi hiyo muhimu kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, jambo la tatu **ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wajumbe ni ghasia na ngoma zinazopigwa hadi alfajiri. Mhe. Naibu Spika, suala hili nalo limezungumzwa na Wajumbe** takriban wote waliopata nafasi ya kuzungumza. Naomba kukiri kwamba Ofisi yangu imekuwa ikipokea malalamiko ya wananchi kutoka kila pembe ya nchi yetu hasa Unguja, kwa kiasi fulani wananchi wamechoka wanaomba serikali iwahurumie. Na wao wanasema wanawake zao Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni mfano sana wa suala hili, amewahi kuja na watu wake kutoka maeneo mbali mbali ya jimbo lake, wakilalamikia kuhusu ngoma ambazo zinapigwa katika maeneo yao hadi alfajiri na kwa ghasia kubwa na kukirihisha sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe na wasaidizi wangu tumeshakagua maaeneo yote ya Unguja hii, mjini na mashamba tena usiku wa manane, kwenye kumbi za disco na ngoma, iwe Raju, iwe Entebbe na maeneo yote ya starehe na kushuhudia mambo makubwa. Mara zote nasi hujifanya kama wateja wa kawaida kuna mambo makubwa ambayo tumeyagundua ambayo kwa vyovyote lazima yadhibitiwe na ndio sababu ya serikali ya kuja na Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kasema kaitembelea Spain yote hakusikia ngoma ikipigwa. Spain katika nchi ya Ulaya ndio kwenyewe kwa starehe za muziki, lakini muziki huusikii ukitembea Spain.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Ali Salum Haji wa Jimbo la Kwahani kwamba Kumbi ziwe na *sound proof*. Hili nalo ndio dhumuni la Mswada huu katika vifungu vya Sehemu ya Sita kwenye Mswada huu na Kanuni zitakazotungwa baadae.

Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tunazungumza na wahusika mbali mbali wakati wa maandalizi ya sheria hii, suala la kuwa na *sound proof* tulizungumza na kwamba sharti hili litawahusu wamiliki wa kumbi zote; iwe raia, iwe hoteli, iwe vikosi vya ulinzi. Serikali haitoingilia uhuru wa vikosi vya ulinzi kwa kujiburudisha baada ya kazi ngumu ya ulinzi, lakini uhuru huo hauwezi ukaruhusiwa ukawaudhi wengine, haiwezekani iendelee kuruhusiwa Kambi ya Jeshi Chukwani ipige mziki wa ghasia uwaudhi watu wote wa Shehia ya Kiembesamaki. Ushauri wetu ni kwamba wajenge *sound proof hall,* baadaye wajiburudishe usiku kucha na mchana bila ya kuwaudhi wengine.

Haiwezekani pia waendelee kuwaachia Chuo cha Mafunzo au Polisi wapige mziki usiku kucha iwaudhi watu wote wa Kwahani, Kilimani, Rahaleo na Jang'ombe wakiulizwa sisi ni walinzi. Katika suala hili naomba nilipongeze sana Jeshi la Polisi Zanzibar kwa kujenga ukumbi mzuri wa kisasa wenye *sound proof* nzuri na safi pale katika mesi yao. Naomba vikosi vyengine viige mfano wao.

Mhe. Naibu Spika, jambo la nne ambalo lilizungumzwa sana ni kwamba baa zimekithiri katika maeneo ya watu. Mhe. Naibu Spika, suala hili limechangiwa na Waheshimiwa wote wa Baraza lako nakubaliana na maoni yao, maana nami pia huwa nalalamikiwa. Ninachotaka kusema ni kwamba, Wizara yangu haihusiki na utolewaji wa vibali vya kuendesha baa wala vibali vya uuzaji wa pombe. Suala hili lipo katika taasisi nyengine na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum wanalishughulikia.

Mhe. Naibu Spika, katika hizo baa kuna shughuli za upigaji ngoma kwenye kambi zao. Ninachowaahidi Wajumbe wa Baraza lako Tukufu baada ya kupitishwa sheria hizi basi wananchi sasa watapata utulivu. Na wale wananchi wa Amani ambao Mhe. Farida Amour Mohammed, amezungumzia naomba afanye subira baada ya kupitishwa sheria hizi na baada ya Mhe. Rais, kuitia saini mambo yale yatadhibitiwa.

Mhe. Naibu Spika, jambo la tano ni sifa ya Mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe wengi walizungumza sifa za mwenyekiti ni nyepesi, hazikuoneshwa vyema. Ukweli ni kwamba Mwenyekiti wa Baraza hili anatakiwa zaidi awe na mambo mawili. La kwanza awe anaumwa na utamaduni wa nchi yetu. La pili awe na kipaji kikubwa katika masuala ya mila, silka, utamaduni na heshima ya Kizanzibari. Haitoshi tu hata kidogo mtu kuwa na *master degree* au *PHD* ya *Arts* lakini suruali yake akawa anaifunga kata kei.

Tulikuwa tunafikiri mtu kama Marehemu Bakari Abeid, hakwenda Makerere, lakini kipaji chake katika mila, silka, adabu na heshima ya nchi yetu ilikuwa ni kubwa na hawa wapo wengi. Kwa hivyo tunaona kwamba tukijifunga kwa taaluma tunaweza kwa kweli tukawaacha watu muhimu

ambao tunao, ambao tukiwapa jukumu hili wanaweza wakalisimamia vizuri. Hayo ndio maoni ya Serikali na naomba Waheshimiwa wa Baraza lako Tukufu wakubaliane na sisi.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi kwamba faini ni ndogo katika makosa mbali mbali. Wajumbe wengi wamezungumza kwamba faini zilizowekwa zimetajwa zisizozidi, na hivyo kuna uwezekano wa kutoa adhabu ndogo kwa wanaokosa. Wizara imezingatia kilio hicho cha Waheshimiwa Wawakilishi, imekubali kurekebisha katika vifungu vyote vya adhabu neno isiyozidi liondoke na badala yake litumike lisilopungua.

Jambo la saba ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wawakilishi ni suala la uamuzi wa Waziri kuwa wa mwisho. Mhe. Naibu Spika, lengo la kifungu hiki ni kumpa Waziri anayeshughulikia na utamaduni mamlaka ya kiutawala wa kufanya maamuzi juu ya yaliyofanywa na Maofisa aliowapa kazi ya kusaidia kiutawala. Msimamizi Mkuu wa shughuli za utamaduni katika nchi ni Waziri wa Utamaduni, lakini kiutendaji ametoa baadhi ya mamlaka yake asaidiwe na maofisa mbali mbali wa serikali kuanzia Sheha, Mkaguzi, Mrajis, Katibu na wengine.

Mwananchi akiona hajatendewa haki ngazi ya mwisho ya utawala katika suala hili kama msimamizi amewekewa kuwa ni Waziri wa Utamaduni anayehusika, lakini hili halimnyimi nafasi mwananchi kwenda Mahakamani ambapo Kikatiba ndiko kwenye maamuzi ya mwisho. Hili si geni, mfano Katiba ya *ZFA* yenyewe imesema hasa kwamba masuala yote ya michezo hayaruhusiwi kwenda Mahakamani, lakini kwa sababu Katiba ya nchi, hivi sasa suala hili lipo Mahakamani.

Hata hivyo Mhe. Naibu Spika, ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe tumekubali kwamba mwisho wa maneno ya kifungu hicho tuongeze maneno kwamba "na mtu asiporidhika na maamuzi ya Waziri anaweza kufanyiwa mapitio uamuzi huo katika Mahakama Kuu ya Zanzibar".

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla sasa kabla ya kumalizia kifungu cha 8 naomba nimalizie vifungu ambavyo vimebakia katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe mmoja mmoja.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati, tunamshukuru, na yale yote ambayo ameyataja katika mchango wake, ushauri ambao kwanza ametupa katika Kamati, tunamshukuru sana na ushauri ambao ametupa katika mchango hapa, tunauchukua.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, mambo mengi mazito nimeshayajibu katika mambo ya jumla. Kulikuwa kuna jambo ambalo ametushauri, naomba nizungumze kwamba na hasa nimpe pole katika suala ambalo mnenguaji mmoja alitaka kumkumbatia hadharani. Nampa pole kwa hilo, baada ya kupita sheria hii masuala hayo yatakuwa hayawezekani tena.

Katika kifungu cha 47 hapakutajwa mtoto lakini kifungu cha 46 kimeeleza habari ya mtoto. Kwa hivyo vifungu vyote viwili 46 na 47 kimoja kinamuhusu mtoto na chengine kinachofuata kinamuhusu mtu wa kawaida.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk hayupo, yeye alitaka kujua vikundi vingapi vya wasanii. Katika kumbukumbu zetu kuna vikundi 73 vya maigizo vilivyosajiliwa, vikundi 40 vya ngoma ambavyo vimesajiliwa, vikundi 21 vilivyosajiliwa vya tiba za jadi vikundi 21 na *promoter* vikundi 12 vyote vimesajiliwa.

Kuhusu vikundi ambavyo vilishiriki katika onesho la Sauti ya Busara ni vitano. *Culture*, Mohammed Ilyas, Kiki *DCMA* na Shirikisho; vyote hivi vilishiriki. Kuhusiana na suala la kushughulikia mambo ya Entebbe na kwengineko, ninachomuahidi ni kwamba baada ya sheria hii kupita masuala haya yatakuwa yamedhibitiwa vizuri.

Mhe. Wanu Hafidh ninamshukuru sana kwa mchango wake; alitupa ushauri mwingi sana wenye kujenga tunakushukuru, katika masuala ya baa na pombe nimeshajibu. Katika suala la adhabu tumelizungumza, tafsiri ya kikundi tumeieleza vizuri katika sheria.

Mhe. Farida tunakushukuru sana kwa mchango wako kuhusu amani na ghasia zake tumezizungumza, kuhusu leseni kwenye nyumba za maonesho zitolewe vizuri ushauri wako tunauchukua. Kuhusu malipo mambo haya yatawekwa katika kanuni kama ambavyo sheria imetajwa.

Mhe. Bi Raya Suleiman Hamad tunakushukuru sana kwa mchango wako na hasa uliposisitiza umuhimu wa wazee kutilia maanani malezi ya watoto wetu. Mheshimiwa hili tunakushukuru na bado tunaendelea kutoa wito kwa wazee wote tushirikiane kuhakikisha kwamba tunasaidiana katika kuwalea watoto wetu katika mila, silka na utamaduni wa nchi yetu.

Kuhusu machangudoa. Sheria hii haitashughulikia mambo haya, haya yanasimamiwa katika sheria ya uzembe na uzururaji. Kuhusu wanaochaguliwa na *DC* watapatikanaje. Kifungu cha 27(1) watateuliwa na Mkuu wa Wilaya kwa kushauriana na taasisi husika.

Kuhusu walemavu na wao wawemo katika Bodi na Mabaraza. Mheshimiwa Mwakilishi nakuhakikishia kwamba ushauri huo tutauchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa wa Jimbo la Kikwajuni ninakushukuru kwa mchango mzuri kuhusu maelezo kwamba kuwapa tunza wasanii wa zamani taasisi inayohusika iwepo taratibu. Mheshimiwa Mwakilishi hili tutaliweka katika kanuni vizuri ili kusitokee upendeleo wowote.

Kuhusu ngoma yako ya kibuki ambayo inachezwa sana katika Jimbo la Kikwajuni. Ushauri wako tumeuchukua lakini huu kwanza wanapewa leseni chini ya tiba za jadi, inaingia pale kwa hivyo wote wanaofanya mambo ya kibuki wanachukua leseni chini ya tiba za jadi na kuhusu malalamiko ya huyu mama ambaye ana matatizo katika suala hili naomba tushirikiane tumsaidie, tuangalie namna gani mimi, wewe na yeye tutaonana ili tuangalie matatizo yake na tuweze kuyatafutia ufumbuzi.

Suala la wageni na mavazi nimeshalizungumza Mheshimiwa ametoa mchango mwingi kuhusu mkaguzi kuingia kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote katika eneo lote ile ndio kazi yao, na hata hivi sasa wanafanya wanapata vikwazo vingi, lakini wanafanya vizuri na kwa kweli inatusaidia sana angalau kupunguza hali hii.

Kuhusu Sheha awe na uamuzi. Sheha kwa kweli kazi anayoifanya anaifanya kwa niaba yetu na atakapokuwa anafanya kama binadamu, anaweza akafanya matatizo yoyote. Sasa umewekwa utaratibu maalum, kuwe kuna ngazi ambazo zinaweza kufanya *reference* yale ambayo wamefanya na kutoa uamuzi kama ambavyo limezungumzwa.

Kuhusu suala la Nyumba ya Sanaa. Ni kweli nyumba ya sanaa haiko katika hali nzuri lakini tumejitahidi, mimi nilipofika pale inavuja yote lakini *alhamdulillah* tumeshaiezua na kuiezeka upya na taratibu ya kurekebisha zaidi inaendelea kulingana na upatikanaji wa bajeti.

Ushauri wako kuhusu *COSOZA* nimeuchukua tutashirikiana na taasisi inayohusika. Mhe. Bi Panya tunakushukuru sana kwa mchango wako mara zote kwa kweli umekuwa *very active* kuona kwamba mila, silka na utamaduni wa nchi yetu unalindwa si katika michango tu lakini hata katika maeneo mengine. Ushauri wako katika kifungu cha 6 awe, awe, awe ni sahihi tunauchukua, tutafanya marekebisho.

Kuhusu kuwepo kwa viongozi wa dini. Kuwepo kwao ni muhimu sana hasa katika kutoa taaluma, jambo hili linahitaji taaluma kubwa na viongozi wetu wa dini wana nafasi kubwa sana katika kutoa taaluma ya waumini wetu, kwa hivyo serikali imeona sana umuhimu wao na ndio maana wakaitia katika bodi hii.

Uliuliza maana ya ngono. Ngono ni kitendo cha kujamiiana kwa mujibu wa *dictionary* la Kiswahili fasihi. Na kuhusu ushauri wako kwamba tuanze kutoa elimu kwanza tumelichukua na kama nilivyokwambia kwamba tutashirikiana na viongozi wa dini katika kutoa taaluma hii.

Mhe. Mgeni Hassan Juma yeye tunamshukuru sana kwa mchango wake mzuri. Alieleza mambo mengi ya maana sana ametushauri sana yale yote yaliyozungumzwa kuhusu baa, mavazi nimeshayajibu, muundo wa Baraza nafasi ya mwanamke vile vile tumelizingatia na kifungu cha (3) kimetaja hilo.

Kuhusu tafsiri ya neno akili ile iliyomo katika lugha ya Kiingereza ndio sahihi, sifa za mwenyekiti nimeshajibu atakuwa na mamlaka ya kutambua sanaa iliyofanywa sana ni Baraza la Sanaa ni kifungu cha 7(a) na 7(q).

Kuhusu hadithi za kale wazanzibari zipo zimeanza kufanya kazi, juzi nilikuletea gazeti uone juhudi ambazo zimeanza kufanywa.

Mhe. Hija Hassan Hija tunakushukuru sana kwa mchango wako na ushauri uliotupa tusaidiane kuufanyia kazi; sote ni viongozi, sote ni wazazi. Kifungu cha 51(3) kwamba tuongeze neno mwisho wa ukaguzi ushauri wake tumeukubali.

Mhe. Saleh Nassor Juma, muasisi, tunamshukuru sana kwa mchango wake mkubwa hasa msisitizo wa kuwaenzi wasanii wetu wa zamani kawataja wengi sana, hasa keptain Mwadini na wengine, ushauri wake tumeuchukua tunamshukuru sana na yote ambayo mengine ametushauri tutayaingiza katika kanuni.

Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani umetupa mchango mzuri sana, umetushauri kuhusu kuweka *sound proof* hili limo na tumelikusudia kuliingiza katika kanuni. Suala la ufuatiliaji ni kweli palikuwa na watu kidogo sana pale Baraza la Sanaa ndio maana tukaamua sasa shughuli hizi zifanywe pia katika Wilaya zetu tusaidiane katika kudhibiti.

Na kifungu cha 8(1)(c) tafsiri ya neno hadharani tumelikubali kwamba wengine utadhani kwamba labda hadharani ni nje tu lakini waliomo ndani waliojenga jengo kidogo linaweza kuwaletea matatizo katika kulishughulikia, hivyo tunaukubali ushauri wako.

Ninamshukuru pia Naibu Waziri kwa namna ambavyo amenisaidia katika kujibu baadhi ya hoja, lakini zaidi mchango wa Mhe. Asha Abdu Haji ushauri wake namshukuru sana.

Mhe. Salma Bilali na Mhe. Jaku tunawakushukuru sana kwa michango yao.

Mhe. Naibu Spika, jambo kubwa ambalo Waheshimiwa Wajumbe walilisisitiza ni kwamba katika shughuli hii ya usimamizi wa mswada huu Wizara itakuwa na kazi kubwa. Ni kweli kwamba Wizara katika hili ina kazi kubwa lakini tumekusudia kuifanya na tumeianza muda mrefu lakini sheria ambazo tulizokuwa nazo zilikuwa kwa kweli hazitusaidii. Tunamkamata mtu unakwenda naye mahkamani sheria iliyopita ilikuwa alipe shilingi 150 sasa ilikuwa mtihani vijana wananambia Mheshimiwa hizi kazi hazifanyiki. Tunakwenda kule watu wanafanya wanavyotaka lakini ukimpeleka mahkamani sheria inasema analipa shs.150 tukaona aa hakuna tatizo kubwa, kwa hivyo ndio maana tukaja na sheria hii.

Na kumbi ambazo tumekuwa nazo muda wote ni zile ambazo ni *open space,* nazo zimekuwa zikitupa adha kubwa, wananchi wanataka utulivu katika maeneo baada ya mchana kutwa kutafuta maisha lakini jirani zao kuna ngoma na ndirimo kwa kweli tumepata malalamiko mbali mbali.

Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano hapa na Miundombinu jirani yake Raju ilikuwa kila siku napata tabu, lakini nimejaribu kupunguza kidogo nimekwenda mara mbili tatu pale usiku na wasaidizi wangu lakini bado tulikuwa hatujapata hukumu za kutosha. Nimekwenda kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Kiwengwa usiku sana hali mbaya sana maeneo yote ya kijiji yana muziki zinafika kumi, ukiingia ndani wanaocheza ni watu wanne lakini ghasia zake zinakirihisha maili kumi. Na nyengine tumeingia msikitini alfajiri kusali muadhini anaadhini adhana haitoki nje chini yake kuna mapigo ya ajabu sana. Kusema kweli wananchi wamekuwa wakilalamika, masheha wamekuwa wakitulalamikia, Wakuu wa Wilaya wamekuwa wakitulalamikia, serikali imekuwa inatulalamikia na wananchi kwa jumla.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ni kweli kazi tunayo kubwa, nimetiwa moyo sana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu. Naamini kwamba nitapata usaidizi mkubwa katika utekelezaji na usimamizi wa sheria itakayotungwa, mimi bado ninajipa moyo kwamba hatujaharibikiwa sana.

Jana Mhe. Naibu Spika, niliona jambo ambalo lilinifurahisha, lilinipa moyo nilipokuwa katika *cafeteria* hapa baada ya semina. Tulikuwa tunataka Waheshimiwa Wajumbe wanakwenda kunawa pale katika mfereji kasimama Mhe. Jihad na vijana wawili kutoka Ofisi ya Rais Ikulu

Utawala Bora wanakwenda kunawa. Wanakaribia pale Mhe. Mohammed Haji Khalid naye akafika, kama walioamrishwa watu wote watatu walirudi nyuma wakamuacha Mzee Mohammed Haji akanawa, *as if* kama wamepewa amri. Maana yake ni kwamba bado heshima ya uzee katika silka na utamaduni wetu bado zinazingatiwa. Kwa hivyo ikiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lile, Mhe. Jihad Waziri angeweza kusema aa mimi Waziri lakini kuona kwamba Mhe. Mohammed Haji ni mtu mzima, na wale vijana wote wakarudi nyuma wakamuacha yeye kwanza. Sasa nahisi kwamba bado Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaharibikiwa sana, tunahitaji kuwa pamoja kuhakikisha kwamba mswada huu tunaupitisha na tunausimamia.

Serikali Mhe. Naibu Spika, imeleta mswada huu ili kuinusuru jamii ya wazanzibari isipotee zaidi, anasa uasili wake utamaduni wetu, jambo ambalo muhimu sana kwa maendeleo ya jamii ya nchi yote. Nimeridhika sana michango na ushauri kwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na ninaahidi kwamba ushauri ambao umetupa tutauzingatia na mwengine tutauingiza katika kanuni ambazo kimsingi tumeshaanza kuziandaa ili mswada huu ukishapitishwa tuwe na kanuni zitakazotoa nguvu katika utekelezaji wa vifungu husika.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru na ninaomba kutoa hoja.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

Kamati ya Kutunga Sheria

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Sanaa na Muziki Namba 6 ya 1983 na Sheria ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho Namba 1 ya 2009 na Kutunga Sheria mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo

Sehemu ya Kwanza
Masharti ya Awali

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa. Mimi nataka kutoa angalizo tu kwamba katika kifungu hiki cha ufafanuzi neno Mrajis maana yake lina uthibitisho wa kifungu cha 20. Hoja yangu ipo katika kifungu cha 20 hapa natoa angalizo ili mabadiliko yatakapotokezea kufanyika yatagusa na hapa pia. Naomba tuendelee.

Sehemu ya Pili
Uanzishwaji wa Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni

Kifungu 3 Uanzishwaji wa Baraza

Kifungu 4 Muhuri wa Baraza
Kifungu 5 Muundo wa Baraza
Kifungu 6 Sifa za Mwenyekiti

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuja hapa alikuja kuzungumzia juu ya suala zima linalohusiana na sifa hizi za Mwenyekiti, lakini wakati nilipokuwa ninachangia nilisema kwamba hapa sifa ya elimu imekosekana, lakini katika majibu ambayo alikuwa akiyatoa Mhe. Waziri alikuwa anasema kwamba elimu katika eneo hili haina umuhimu sana. Sasa hajui kwamba kwa sasa wale watu ambao wanapewa vyeo vya uenyekiti wana uwezo wa kwenda kuliwakilisha Taifa hata nje ya nchi. Je, itakapokuwa mtu huyu hana elimu kazi hii ataifanya vipi. Naomba majibu ya ziada Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Vijana: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimezungumza kwamba katika suala hili la Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza hili suala la kipaji kwanza muhimu sana. Hili la pili suala la mtu ambaye anaumwa na uchungu wa mila, silka na utamaduni ni jambo la msingi. Nikatoa mfano hapa unaweza ukawa na Mwenyekiti ambaye ana *PHD* ya mambo ya *culture,* lakini ukimuona atavaa suruali chini ya kata "Kei" hapa, ni mtihani ana elimu kubwa huyu lakini ukimtizama anavyovaa, anavyo-*act*, anavyokuwa hafanani hata kidogo kuwa Mwenyekiti wa Baraza hili. Na nikatoa mfano ambao uko wazi sana, nikasema tumkumbukeni Mwenyezi Mungu amrehemu akhera aliko Mzee wetu Bakari Abeid, hakwenda Makerere lakini mtu wa aina ile, na wapo wengi hapa Zanzibar ukimuenzi katika Baraza hili vipaji vyao na uchungu walionao anaweza kulisaidia hili Baraza na ku-*preserve culture* yetu, silka, adabu na heshima ya nchi yetu.

Sasa hili Mwenyekiti anateuliwa na Mhe. Rais, na Rais hatuweki hapa Zanzibar watu ambao hawana mazingatio na vipimo, naamini wakati wa kuweka mtu wa aina hii atayazingatia yote hayo. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika na sisi tulizungumza sana hilo, tulishauriana na wadau wanaohusika mbali mbali tukaona kwamba ni busara kuiweka katika mfumo huu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ambayo Mhe. Waziri amekwishayaongea hapa mimi bado naendelea na msimamo wangu wa kwamba ili tuweze kuitangaza nchi yetu hususan katika masuala haya ya sanaa, kwa sababu muelekeo wetu Mhe. Mwenyekiti sanaa inawezekana ikawa ni ajira katika nchi yetu. Je, inapotokezea mambo kama haya tukamtaka yule Mwenyekiti aende akawakilishe pengine katika mkutano fulani, endapo kama Mwenyekiti yule ana uzoefu tu pengine wa kucheza ngoma au wa kuweza kufanya mambo mengine yoyote atakapokwenda kule ataliwakilisha vipi Taifa? Naomba kupata ufafanuzi zaidi katika hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu hakijakataza, maana ingelikuwa kimetaja humu kama Mwenyekiti anatakiwa asiwe na elimu, hapo kasema ah nyinyi vipi jamani, lakini hajasema hivyo kama Mwenyekiti wa Baraza hili anatakiwa asiwe na elimu. Sisi tumemuachia hiyo mteuzi *appointing authority.*

Sisi tunampa masharti hayo matatu; awe Mzanzibari, awe na uzoefu katika mambo yanayohusiana na sanaa na Mhe. Mwenyekiti hili jambo muhimu sana, ana maadili yanayokubalika katika jamii. Sasa kifungu hiki hakijakataza kuwa na elimu kuteuliwa, sasa

anayeteua atayazingatia hayo, lakini tusimlazimishe kwamba lazima mtu awe na *PhD*, awe na *masters*, awe na *degree* ya kwanza, sisi ndio tumempa sharti hizi na tunaamini kwamba kwa tunakokwenda hakuna Mzanzibari aliye na sifa hizi asiwe na elimu. Kwa hivyo, hapo Mhe. Mwenyekiti ndio mazingatio yetu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti ahsante, na mimi hoja yangu hapa ilikuwa kwa huyu huyu Mwenyekiti ambaye ilikuwa anasema awe na uzoefu katika mambo yanayohusiana na sanaa, lakini haikuainishwa uzoefu huo ni wa muda gani na awe na miaka mingapi katika uzoefu huo?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili uzoefu sisi tuliona kwamba tusiupime kwa mwaka, unaweza kumpata mtu ana uzoefu wa miaka kumi lakini bado akawa hajaiva katika suala hili. Kwa hivyo, sisi tulimuachia mteuzi afanye mazingatio mapana zaidi, lakini kama Mhe. Mwakilishi ana ushauri basi atupe.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, mimi naona tu ule uzoefu ni wa muda mwingi ambapo katika sheria nyingi tunazozipitisha hapa huwa tunasema awe na uzoefu usiopungua muda gani ndio nikawa naona nalo kulizingatia ni vyema, lakini kama anaona hakuna athari yoyote mimi sina tatizo. Lakini mara nyingi tumekuwa tukipitisha sheria hapa tunasema awe na uzoefu usiopungua miaka miwili au mitatu au kama tumeiona mingi tunaipunguza iwe kidogo, tukiona kidogo tunaiongeza iwe mingi kwa sababu ya kuzingatia hivyo, lakini kama linaonekana halina pingamizi yoyote mimi sina matatizo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, katika hili nakubaliana na rai ya Mhe. Mwakilishi kwamba tuweke ana uzoefu katika mambo yanayohusiana na sanaa usiozidi miaka kumi.

Kifungu 6 Sifa za Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa ukweli wake, kauli yake na uungwana wake aliposema mswada huu atauleta haraka iwezekanavyo baada ya kuona maadili na mmong'onyoko unazidi kupotea kwa vijana wetu.

Mhe. Waziri katika mchango wangu wa maandishi nilipendekeza kifungu (h) nilipokuandikia Mheshimiwa utapofanya majumuisho unieleze katika kifungu cha (7) kinachohusu kazi za sanaa naona kifungu hiki kimeonesha sanaa kwa udhibiti wa nyumba ya maonesho na sanaa wakati moja ya madhumuni ya mswada huu ni kudhibiti pia kumbi za starehe kama vile *club*, baa na kumbi za disko. Sasa mbona sehemu hizi hazijazungumzwa katika kifungu hiki tukisema nyumba za maonesho pia zinajumuisha sehemu hizo.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba uongeze kifungu cha (h) kitakachosema kudhibiti kumbi za starehe, *club*, baa, disko kwa upande wa maadili, sauti inayotoka kuelekea

katika jamii na kero kwa wananchi na baa zisiwe ndani ya makaazi ya wananchi. Hilo ndio ombi langu kwako Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba sisi Wizara ya Habari hatuhusiki na masuala ya leseni za baa na uanzishwaji wake na leseni za kulewa na ulewaji wake. Sasa kuingiza katika kifungu hiki cha sheria jambo ambalo halimo katika mamlaka ya wizara yetu itakuwa tunaingilia mamlaka ya taasisi nyengine. Kwa hivyo, naomba anisamehe hilo kwamba hilo hatuwezi kulichanganya litahusika katika taasisi inayohusika ambayo inadhibiti, ina-*regulate*, inakataza mambo hayo lakini humu hayamo.

Mhe. Mwenyekiti, na kuhusu kutaja moja kwa moja ukiangalia hili fungu kutoka 7 mpaka (q) yote hayo Mheshimiwa yamezungumzwa vizuri, sio lazima tutaje kila kitu. Mfano, kuhifadhi, kulinda na kuimarisha mila, silka na maadili ya utamaduni wa Zanzibar. Sasa huwezi kuhifadhi, kulinda na kuimarisha mila kumbe unaachia watu wapige mangoma na kufanya ghasia kwa kweli hili neno ni neno pana linaingiza mambo yote ambayo yamelalamikiwa na ni kero hivi sasa. Kwa hivyo, naomba akubali kwamba tusitaje kifungu kimoja baada ya kimoja, lakini tunapotaja neno kifungu kama hiki (b) huwa kinazingatia mambo yote ya jumla jumla. Na haya baada ya hapo vifungu hivi tumekusudia kuviingiza katika kanuni ambayo kwa kweli ndio ambavyo vitanichambua zaidi yale malengo ambayo Mhe. Mwakilishi tumekuwa tukizungumza sana wakati tofauti katika suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hiki chombo ni mali ya wananchi na kuwepo kwetu dhamana kwenda kuulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu hii dhamana tumeitumia vipi akiwemo Waziri na mimi Mwakilishi wa wananchi. Mimi ningemuomba hili suala akaliweka wazi, hana haja ya kupita na kama nani dhamana anitajie nani dhamana, tupo hapa kwa niaba ya wananchi, anieleze nani dhamana wa suala hili ainuke, sijui umenielewa Mhe. Waziri?

Mhe. Mwenyekiti: Ngoja mimi nisaidie Waziri kasemaje watu wa vileo hawatoi vibali wao, Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ ndio wanaotoa vibali, yeye yuko kwenye sanaa na utamaduni. Sasa kwa kuwa serikali imesikia watafanya utaratibu, kwa sababu siku zote kwenye vileo wanaitwa wananchi wanaambiwa, je, hapa mumekubali pafunguliwe au pasifunguliwe. Wakikataa ikifunguliwa wanakwenda Mahakamani kuweka vizuizi huo ndio utaratibu. Kwa hivyo, yeye hatoi leseni ya mambo ya vileo yaani hizo baa, hatoi yeye iko Tawala za Mikoa. Sasa kama una suala jengine uliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Disko kutoa sauti nje kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri disko kibali unatoa wewe?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, burudani zote zinazopigwa kibali natoa mimi na ndio maana katika mswada huu kuna kifungu sehemu ya sita, kifungu 37, 38,39,40,41,42,43 hivyo vinahusiana mahsusi kwa ajili ya leseni na usalama wa nyumba za maonesho ikiwemo mambo yote hayo.

Kwa hivyo, tumelizingatia kwa upana zaidi na kwa ujumla ndio msingi wa malalamiko mengi ya wananchi. Kwa hivyo, tumelizingatia vizuri sana Mhe. Mwakilishi katika kifungu sehemu ya sita ya mswada huu ambapo kuna vifungu kuanzia 37 mpaka 43.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoteli ziko chini ya dhamana yake, mimi angeweka tu wazi kwamba mziki ule hautoki nje ukaudhi watu kama hii njia ya Kiembesamaki sasa hivi wanafunzi wanapata shida, madaktari shida angeweka tu wazi. Mimi nakushauri Mhe. Waziri ungeliweka wazi kwamba disko litakalopigwa lisiingie katika jamii na hoteli zote ziko chini ya dhamana yako haziko kwa Mhe. Haji Omar Kheri hizi.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio anakwambia hayo yote ukisoma kifungu kuanzia 37 mpaka 43 yamezingatiwa hayo, na fungua mswada uangalie tunakuja huko mbele, sisi tunaendelea wewe angalia huko mbele tunakuja yote yamezingatiwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi katika kifungu hiki Nam. 7 kwenye kazi za Baraza kumeainishwa vifungu vingi hapa na mimi nilijaribu kuchangia vifungu vingi kwamba tuviongeze, lakini vile vyengine naridhika na Mhe. Waziri ambapo anasema si kila kitu lazima tukiweke, lakini kuweka kifungu ambacho kupinga mila zote potofu zenye kuleta madhara kwa jamii hiki ni kifungu muhimu, hapa mimi sijaona katika mswada huu kama kifungu hiki kipo. Kuna mila ambazo hazilingani, hata wakati wa Mtume (S.A.W), Mtume kazikuta mila chungu nzima lakini alipoona mila hii haifai iliachwa na mila inayofaa iliendelezwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hicho nakuomba ukizingatie.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kifungu (b) kuhifadhi, kulinda na kuimarisha mila, silka na maadili ya utamaduni wa Zanzibar. Hicho ndio kifungu chenyewe Mhe. Mwakilishi na sisi hatuna mila potofu, sisi mila yetu ni mila nzuri sana inapendwa na wote wanaotembelea hapa na ndio maana nchi yetu ikawa *cosmopolitan*. Sasa ukinambia kwamba nitie mila potofu sisi hatuna, sisi kazi yetu kubwa ni kuhifadhi, kulinda na kuimarisha mila zetu, hatuna mila potofu sisi na ndio kazi yake.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 7 Kazi za Baraza pamoja na marekebisho yake
Kfiungu 8 Uwezo wa Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9 Mikutano ya Baraza
Kifungu 10 Maamuzi ya Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11 Muda wa Wajumbe wa Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12 Posho kwa Wajumbe
Kifungu 13 Wafanyakazi wa Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14 Sekretarieti ya Baraza
Kifungu 15 Majukumu ya Sekretarieti ya Baraza

Sehemu ya Tatu

Uongozi wa Baraza

Kifungu 16 Katibu Mtendaji wa Baraza
Kifungu 17 Sifa za Katibu Mtendaji
Kifungu 18 Kazi za Katibu Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 19 Katibu wa Baraza
Kifungu 20 Mrajis

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti ahsante, mimi nilikuwa nataka kupata ufafanuzi zaidi kwa sababu Mhe. Waziri alipokuwa akizungumza hapa mimi nilisema kule mwanzo kwamba kutokana na uhalisia ambao umejitokeza katika kifungu cha 24. Uteuzi wa Mrajis mimi sijakubaliana nao kwamba uwe unafanywa na Mhe. Waziri hususan ukiangalia mwisho kabisa katika kile kifungu cha 24, kifungu kidogo cha (3) uamuzi wa waziri utakuwa wa mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, tulivyozoea Mrajis huwa anateuliwa na Mhe. Rais, sasa hapa Mrajis anateuliwa na Waziri. Sasa mimi hapa sijakubaliana napo naomba maelezo ya ziada zaidi katika hili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi niko Barazani miaka mingi karibu mwaka wa ishirini unamaliza na tumekuwa tukitunga sheria nyingi sana. Sikumbuki kuwa na sheria ambazo Mrajis anachaguliwa na Rais, *best practice* ni kwamba Warajis wanachaguliwa na Mawaziri. Sasa labda ikitokea moja, mbili, tatu *exception* itakuwa nimesahau, lakini Warajis wengi ambao wamo katika taasisi zetu huwa tunachagua sisi, hii ndio *best practice.*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mfano mdogo tu Mrajis wa Mambo Msiige ameteuliwa na Rais, sasa anaposema kwamba hakuna Mrajis anayeteuliwa na Rais hapa inakuwa kidogo sijafahamu. Hoja yangu ya msingi hasa Mhe. Mwenyekiti ipo katika kifungu cha 24.

Mhe. Mwenyekiti: Hatujafika huko.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Kwa hiyo, tusubiri ifike 24 halafu tutakuja kuzungumzia hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Ikifika hoja yako utasimama utasema.

Kifungu 20 Mrajis pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21 Sifa za Mrajis pamoja na marekebisho yake
Kifungu 22 Majukumu ya Mrajis pamoja na marekebisho yake
Kifungu 23 Uwezo wa Mrajis
Kifungu 24 Rufaa

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio kwenye hoja yangu hasa, tulikuwa tunataka kufahamu zaidi Mhe. Waziri aliposimama hapa alizungumzia kuhusu utendaji kazi kwa hawa watu watatu ambao niliomba kupata ufafanuzi wake juzi nilipokuwa nachangia.

Mwenyekiti anateuliwa na Rais, Katibu Mtendaji anateuliwa na Rais lakini Mrajis atakuwa anateuliwa na Waziri.

Halafu vile vile maamuzi ambayo huyu atakuwa kama ndio mwenye *power* ya kufuatilia masuala yote na utendaji wake, lakini katika *power* ya maamuzi, maamuzi ambayo yatakuwa yanafikiwa katika Baraza hili la Sanaa Waziri anaweza kukataa maamuzi yote haya, na katika mchango wangu nilisema kwamba hiki kifungu cha 24, kifungu kidogo cha (3) kitakuwa kimevunja Katiba.

Ibara ya 134 kama ambavyo ilikuwa inajionesha kule katika Katiba yetu. Sasa tulimtaka Mhe. Waziri atufahamishe kwa nini huyu Mrajis ana uwezo mkubwa zaidi katika masuala haya kuliko hata Katibu Mtendaji. Naomba ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Mjumbe hajakisoma vizuri hiki kifungu. Mrajis anao uwezo katika kifungu cha 23, kimesema vizuri hapa naomba nikinukuu kwa faida yake na wengine.

Kifungu cha 23(a) kinasema kwamba:

"Kusimamisha au kufuta usajili wa kikundi chochote cha utamaduni kwa makusudi kinachelewesha au kinamzuia mkaguzi au mtu mwengine aliyeidhinishwa kufanya kazi ya ukaguzi kwa shughuli za utamaduni chini ya sheria hii;

(b) Kusimamisha au kufuta kikundi chochote cha utamaduni kufanya maonesho ikiwa kitashindwa au kitakataa kutekeleza amri au maelekezo kilichopewa na Baraza;

(c) Kusimamisha au kufuta usajili au maonesho kwa kikundi chochote cha utamaduni kwa kusubiri maamuzi ya Baraza", naomba nisisitize hiyo, "kwa kusubiri maamuzi ya Baraza ikiwa kutatokezea mambo yafuatayo:

(i) Ikiwa kikundi chochote cha utamaduni kimevunja masharti ya katiba au kanuni zake;

(ii) ikiwa uongozi umepatikana kinyume na katiba au kanuni zao;

(iii) ikiwa kikundi chochote cha utamaduni kimevunja masharti ya sheria yoyote ya nchi inayohusiana na maadili.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mrajis atalazimika kwa kipindi kisichozidi wiki mbili kuliarifu Baraza uamuzi wa kukifungia kikundi hicho na sababu zake".

Maana yake ni kwamba, uamuzi wowote ambao Mrajis ameufanya ndani ya wiki mbili ataupeleka kwa Baraza, ambapo Baraza wanaweza wakakubaliana au wakafuta maamuzi. Kwa hivyo, Mrajis sio kwamba ana uamuzi mkubwa kuliko Katibu au Baraza zima, yeye anafanya yale mambo ya kuhami, hatuwezi kuachia mambo yaharibike kwa kusubiri kikao, anahami pale pale.

Kwa mfano, kuna kikundi hapa kinaonesha mambo yasiyojuzu, yasiyokubalika katika mitaa, sasa tusubiri tu kwamba aa Mrajis anafanya kazi yake halafu analiarifu Baraza, baadae Baraza litafanya uamuzi na kama Baraza limekataa au limekubali, kikundi kinaruhusu kwenda kwa Waziri, waziri amekubaliana au vipi, kwa ushauri wenu nimekubaliana basi uamuzi huo utapelekwa mbele ya Mahakama Kuu. Kwa hiyo, tushakubaliana hiyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mazungumzo mazuri ya Mhe. Waziri bado ni sawa kwamba Mrajis anaweza kufanya kazi zake na baadaye akachukua ile hoja yake akaipeleka katika Baraza, sina tatizo katika hilo, lakini sasa na hilo Baraza lenyewe linaweza likatoa maamuzi ambapo ile bodi nzima inayokaa ikafikia maamuzi yale, maamuzi yakifika kwa Mhe. Waziri akayakataa yote na ikawa yeye maamuzi yake ndio ya mwisho. Sasa hili ndio tatizo lenyewe linalokuja hapa, naomba ufafanuzi zaidi katika hili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, haya ndio mamlaka ya waziri, sasa waziri kawekwa pale vipi.Tumuangalie leo Said lakini muangalie waziri hayo ndio mamlaka yake kusimamia haya mambo ya utamaduni katika nchi. Sasa ikiwa waziri hana mamlaka hata ya Baraza aliloliteua itakuwa Waziri au vipi, haya Mabaraza tumeteuliwa na waziri, Mhe. Rais ameteua Mwenyekiti na Katibu, lililobakia lote ameteua waziri, kama waziri hana mamlaka itakuwa basi waziri ana kazi gani katika wizara.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa umemuelewa Waziri?

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee bwana. *(Kicheko)*

Kifungu 24 Rufaa pamoja na marekebisho yake

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilikuwa nina *concern* yangu katika kifungu hiki cha 24, na wakati Mhe. Waziri anajibu hoja yangu nakumbuka kama alisema anakubaliana na hoja yangu. Sasa wakati unatupitisha katika kifungu hiki ulisema tu kifungu cha 24 bila ya kusema na marekebisho yake. Swali langu ni kwamba, tunapitisha kifungu cha 24 kama kilivyo au na yale mapendekezo ambayo Mhe. Waziri amenikubalia.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu yaseme mapendekezo, huna?

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Waziri mwenyewe anayajua ndio maana kakubaliana na mimi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Wanu Hafidh juzi alitoa mchango mzuri sana na akatushauri kwamba kifungu hiki cha kwamba uamuzi wa Waziri utakuwa ni wa mwisho, basi tusiitie kama ilivyo isipokuwa katika sheria itamke kwamba, kama mwananchi hatoridhika na maamuzi ya waziri basi awe na uwezo wa kupeleka shauri lake Mahakama Kuu, jambo ambalo baada ya mashauriano na Mheshimiwa *AG* tumekubaliana hatulipingi, kwamba tuweke hivyo na tumekubali. Kwa hivyo, anachozungumza ni hakika kwamba tuseme pamoja na marekebisho yake tumekubaliana naye.

Mhe. Mwenyekiti: Waziri amekubali tuendelee Katibu.

Kifungu 24 Rufaa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 25 Maombi ya usajili pamoja na marekebisho yake
Kifungu 26 Ada na malipo
Kifungu 27 Kuanzishwa kwa Kamati za Wilaya za Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni
Kifungu 28 Muundo wa Kamati ya Wilaya ya Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni
Kifungu 29 Kazi za Kamati za Wilaya za Sanaa na Sensa ya Filanu na Utamaduni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 30 Mkaguzi wa utamaduni wa wilaya

(Hapa Wajumbe walipiga makofi kwa kuingia Mhe. Asha Bakari Makame ukumbini)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa imetosha, keshakaribishwa Mhe. Asha Bakari Makame, tunakukaribisha sana, tuendelee Katibu.

Kifungu 31 Sifa za mkaguzi wa utamaduni wa wilaya
Kifungu 32 Kazi za mkaguzi wa utamaduni wa wilaya pamoja na marekebisho yake
Kifungu 33 Uwezo wa mkaguzi wa utamaduni wa wilaya

Sehemu ya Nne
Maombi ya Kibali

Kifungu 34 Utoaji wa kibali

Sehemu ya Tano
Maonesho ya Machapisho au Usambazaji wa
Mabango ya Matangazo

Kifungu 35 Maonesho ya machapisho au usambazaji wa mabango ya utangazaji
Kifungu 36 Ukatazaji wa maonesho ya machapisho na usambazaji wa mabango ya matangazo

Sehemu ya Sita
Leseni na Usalama wa Nyumba ya Maonesho

Kifungu 37 Leseni ya vikundi vya utamaduni
Kifungu 38 Kwenda kinyume na...

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia nilizungumzia kuhusu kifungu ambacho kikundi cha sanaa kinapokwenda kinyume na yale ambayo wanatakiwa kufanya, kifungo hiki kikundi kitahukumiwa. Sasa sheria inasema kwamba kitalazimika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni tatu za Tanzania au kufungwa. *Concern* yangu nilimuuliza Mhe. Waziri kikundi kitafungwa au kitafungiwa? Wakati ananijibu alinielekeza kwenye tafsiri ya neno kikundi huko ndio kanichanganya zaidi, naomba anipe maelezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kikundi kitafungwa. Kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe walisema juzi kwamba wimbi hili limekuwa kubwa sana, watu wanajifanyia wanavyotaka, wanapiga muziki maeneo wanayotaka,

wakati wanaotaka bila ya kufuata taratibu zozote. Sasa hili limekuwa likituathiri sana na tumeamua kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe hapa tuwe na adhabu kali ya kudhibiti hili.

Sasa katika hilo kwanza ni faini ambayo wajumbe wamenishauri isiyozidi badala yake iwe isiyopungua. Tumekubaliana nayo na ya pili ni kifungo, kikundi kifungwe. Kikundi kimekuja hapa kina-*perform* hakina leseni yoyote kimekuja tu hapa kinafanya minenguo yake kinavyotaka, wanavyofaa basi tudhibiti, na ili kudhibiti lazima watu wawe na woga. Kwa hiyo, maamuzi ya serikali kupitia mswada huu ni kwamba kikundi kifungwe, tukishapata kikundi kimoja, viwili ambavyo vimefungwa basi nidhamu itarudi, na utaratibu utakubalika; lakini tukienda hivi hivi ambavyo tunakwenda tutapiga makelele hakuna ambacho kitafanyika.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi hatalala, wengine wataokuweko chini ya baa nyengine hawalali, lakini tukitoa adhabu kali hili litaondoka. Kwa hivyo, sisi tunafunga ndio mapendekezo yetu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nimefahamu *concern* ya Mhe. Waziri lakini hoja yangu ni kwamba, kwenye baadhi ya vikundi kunakuwa na watu wameajiriwa tu na wewe kama muajiriwa inabidi wakati mwengine ufuate *order* ya muajiri.

Sasa kwa mfano wale wapiga bendi kuna wale *dancers* wanakuwa wanakwenda kucheza tu lakini sio *part* ya ile bendi yenyewe kama bendi. Sasa ukisema kwamba kikundi kitafungwa ina maana kwamba wale wote watachukuliwa watapelekwa jela. Hii haoni kwamba wale wengine ambao ni waajiriwa tu itakuwa kama wanaonewa na wao sio wenye kikundi chenyewe.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, yeye juzi Mhe. Mwakilishi alitwambia kwa kweli lazima tuwe makini katika mambo haya, tushachukuliana muda mrefu watu wanafanya wanavyotaka. Kwa hivyo, kila mtu ambaye ana-*perform* anacheza lazima ajiridhishe kwamba katika mchezo wake anaoufanya basi taratibu na sheria zimefuatwa, sio aje tu katika *stage* aanze kunenguanengua na kuchezacheza anavyotaka tu kwa sababu ameajiriwa, hapana. Lazima yeye mwenyewe ajiridhishe katika uongozi wao kuhakikisha kwamba mambo hayo yamekaa vizuri, tukiachia hivi waziwazi kwa sababu mimi nimeajiriwa tu hii sheria itapata matatizo kutoka mwanzo.

Kwa hivyo, lazima tukubaliane kwamba mtu yeyote ambaye anakwenda ku-*perform* yeye mwenyewe ajiridhishe kuwa sheria za ku-*perform* zimekamilika. Hii ndio sababu ambayo tumechukua kuhakikisha kwamba mambo haya hayaendi kiholela holela kama ambavyo tumeachia siku nyingi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mheshimiwa tuendelee.

Kifungu 38 Kwenda kinyume na masharti ya leseni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 39 Usalama wa majengo ya maonesho
Kifungu 40 Leseni na majengo ya maonesho na usalama wa watu waliohudhuria
Kifungu 41 Uwezo wa Mkaguzi kuingia katika nyumba ya filamu
Kifungu 42 Maelezo ya picha za filamu

Kifungu 43 Uwezo wa kukagua

Sehemu ya Saba
Wajibu wa Watoaji Huduma za Mitandao ya Intaneti

Kifungu 44 Utaratibu
Kifungu 45 Watoaji wa huduma ya mtandao wa Intaneti

Sehemu ya Nane
Katazo la Picha za Ngono

Kifungu 46 Katazo la picha

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia katika kifungu hiki nilisema kama adhabu iliyotolewa katika makosa haya inaonekana ni ndogo, nikapendekeza palipotolewa adhabu ya shilingi milioni mbili iwe shilingi milioni tatu, na palipotolewa adhabu ya shilingi milioni moja iwe shilingi milioni mbili. Sijui Mhe. Waziri anasemaje juu ya hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani mimi wakati nafanya majumuisho hapa nimesema kwamba hiki kifungu kimesema atakuwa ametenda kosa atakapopatikana na hatia na kulipa faini ya shilingi milioni mbili au kifungo cha miaka miwili. Baada ya kufikia ushauri wake sisi tumeweka kwamba kisichopungua, faini isiyopungua shilingi milioni mbili na kifungo kisichopungua miaka miwili.

Sasa hayo itakuwa ni ya Jaji au Hakimu, tumetoa kisichopungua kwa hiyo akiona mitatu, minne, mitano, kumi, ishirini sisi tuko juu, lakini sisi tumeweka hapa *bar* kwamba kisichopungua miaka miwili na faini isiyopungua shilingi milioni mbili. Kwa hivyo, yeye ameweka shilingi milioni tatu tumempa Hakimu au Jaji tumempuruzia kamba zaidi anaweza kuzidi juu lakini asipungue chini.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante tuendelee.

Kifungu 46 Katazo la picha za ngono pamoja na marekebisho yake
Kifungu 47 Picha za ngono za watoto
Kifungu 48 Kutaifisha na kuharibu picha za ngono

Sehemu ya Tisa
Masharti ya Fedha

Kifungu 49 Fedha za Baraza
Kifungu 50 Bajeti
Kifungu 51 Ukaguzi wa hesabu

Sehemu ya Kumi
Makosa na Adhabu

Kifungu 52 Makosa na adhabu
Kifungu 53 Ukatazaji wa umiliki wa filamu na machapisho

Sehemu ya Kumi na Moja
Masharti Mengineyo

Kifungu 54 Kanuni
Kifungu 55 Kufuta na kubakiza

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Baraza la Sanaa na Sensa
ya Filamu na Utamaduni ya 2015

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni ya mwaka 2015 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe: Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunawashukuru kwa kazi nzuri tuliyofanya ya kupitisha mswada. Katibu tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Miradi na Maridhiano namba 1 ya 1999

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwasilisha Mswada wa Mapendekezo ya kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano namba 1 ya mwaka 1999 na Kutunga Sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kwanza awali ya yote nitoe shukurani maalum kwa Kamati inayosimamia Afisi ya Viongozi wakuu kwa kweli kwa mashirikiano makubwa waliyotupa katika kuupitia mswada huu na wameupitia zaidi ya siku tatu mswada, ni mkubwa na tunashukuru tumeafikiana kwa mengi sana takribani yote na hatimae kukubali kuyaacha mawili matatu kwamba uletwe Barazani.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, naomba kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kukubali jana kuwa pamoja katika semina maalum ambayo imetayarishwa na wizara yetu pamoja na Wataalamu wale wa Benki ya Dunia. Ni imani yangu kwamba ile darasa maalum walilotupatia limetusaidia sana katika kuufahamu sera yenyewe na pamoja na sheria hii kama ilivyowasilishwa.

Sasa baada ya utangulizi huo Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako mapendekezo ya mswada wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaadhimia kuimairisha huduma na ujenzi wa miundo mbinu ili kuweza kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wa Zanzibar, katika kufikia adhama hiyo serikali kwa msaada wa Benki ya Dunia imekamilisha mchakato wa sera kuhusu utoaji wa huduma, ujenzi wa Miundo mbinu kwa mashirikiano baina Sekta ya Umma na Sekta binafsi yaani *PPP* na kuidhinisha pamoja na kuandaa muongozo wa utekelezaji.

Kupitia Sera hiyo Sekta ya Umma na Sekta binafsi zitaweza kutambua miradi yenye tija kwa taifa ili iweze kutekelezwa kwa njia ya mashirikiano, katika kufanikisha suala hilo kunahitajika kuweko mfumo madhubuti wa kisheria na kitaasisi katika kusimamia utekelezaji wa Sera ya *PPP*.

Mhe. Naibu Spika, Kutokana na haja ya kuwa na sheria itakayoweza kutumika kwa miradi iliyo na mfumo wa *PPP* wataalamu kwa vipindi tofauti walikusanya taarifa na kuzipitia kumbukumbu za mipango ya maendeleo ya Zanzibar na pia wamepata fursa ya kukutana na wadau katika Sekta za Umma, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo na michango yao yote imeingizwa katika sheria inayopendekezwa.

Aidha, Mhe. Naibu Spika, maoni na mapendezo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa yalikuwa na umuhimu wa kipekee yamezingatiwa na kuwekwa katika sheria iliyoko mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kufuta sheria ya maridhiano ya mwaka 1999 na kuweka sheria mpya ya kanzisha na kusimamia miradi ya *PPP* kutapelekea kuanza kusajiliwa kwa miradi ya *PPP* hapa Zanzibar. Miradi ambayo inategemewa kwa kiasi kikubwa kukuza sekta mbali mbali za Maendeleo na hatimae kukuza na kuimarisha uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nadharia na wazo la *PPP* inahusisha Mipango ya Maendeleo ikiwemo Dira ya Maendeleo 2020 ya Zanzibar MKUZA II na Sekta nyengine katika utekelezaji wake. Hivyo kutakuwa na uhusiano wa karibu baina ya mapendekezo ya mswada huu na utekelezaji wa sera na sheria nyengine hapa nchini. Miongoni mwa sera na sheria hizo ni kama zifuatazo:-

- Sheria ya Manunuzi ya Umma namba 9 ya mwaka 2005 na muungozo wake;
- Sheria ya Uendelezaji na Udhibiti wa Vitega Uchumi namba 11 ya mwaka 2004;
- Sheria ya Tume ya Mipango ya Zanzibar namba 3 ya mwaka 2012;
- Sheria mbali mbali za Kodi;
- Sheria ya Ardhi ya mwaka 1992 na;
- Sera ya Vitega Uchumi ya mwaka 2005 na Mpango Mkuu wa Usafiri wa mwaka 2007.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya mswada huu ni kupendekeza sheria mpya itakayosimamia vyema utekekelezaji wa miradi itakayoshirikisha Sekta ya Umma na Sekta binafsi na kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano namba 1 ya mwaka 1999.

Mhe. Naibu Spika, sheria iliyopo hivi sasa haikueleza wazi wazi utaratibu wa mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi katika uendeshaji wa miradi kwa pamoja na badala yake inaelezea kuhusu miradi ya maridhiano pekee. Vile vile imeonekana ina mapungufu ambayo yanakwamisha utekelezaji.

Miongoni mwa mapungufu kwa sheria hiyo ni hayo yafuatayo:-

(a) Sheria imetungwa bila ya kuwepo Sera ya *PPP;*
(b) Haikuweka utaratibu wa Uhakika na Uwazi katika Uzabuni na Ufatiliaji wa utekelezaji wa Miradi;
(c) Haikueleza kwa uwazi majukumu ya kitaasisi na dhama zao
(d) Haikuweka utaratibu unaoeleweka katika kusuluhisha migogoro baina ya washiriki na;
(e) Haikuzingatiwa kuanzishwa kwa mfuko wa kuendeleza miradi ya *PPP*.

Mhe. Naibu Spika, aidha sheria iko kimnya katika maeneo muhimu yafuatayo:-

(1) Miradi inayoasisiwa na muwekezaji kama ilivyo katika Rasimu ya Sera.
(2) Ushiriki wa Serikali za Mitaa ambao ni muhimu katika utekelezaji wa Mifumo ya *PPP*
(3) Ugharamiaji wa Matayarisho ya Miradi ikiwemo utafiti wa awali na tafiti nyengine pamoja na kuajiri watalamu washauri na waendelezaji miradi.

Mhe. Naibu Spika, Mswada unaopendekezwa una sehemu kuu 10 vifungu 72 na jaduweli moja.

Sehemu ya kwanza ina vifungu viwili vinayoelezea masharti ya awali ya jina fupi, kuanza kutumika kwa sheria na Ufafanuzi.

Sehemu ya Pili Mhe. Naibu Spika, ina vifungu 6 vinavyoweka masharti ya mashiarikiano baina ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi yakijumuisha upeo na aina ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Mkataba wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Muda wa mashirikiano, Umiliki wa mali na haki ya kifedha.

Sehemu ya tatu Mhe. Naibu Spika, ina vifungu 10 vinavyowekwa masharti ya Mfumo wa Kitaasisi na Majukumu ya kila taasisi yakijumuisha kuanzishwa kwa Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Majukumu ya Idara upatikanaji wa nakala za Sheria au Kanuni uanzishwaji wa Kamati ya Wataalamu, Kazi za Kamati ya Wataalamu, Wajibu na Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Utekelezaji.

Mhe. Naibau Spika, sehemu ya 4 ina vifungu vinavyoweka masharti ya Utambuzi wa Miradi yenye Tija, Mfumo wa Maendeleo ya Mradi na Madhumuni yake, kugharamia upembuzi wa awali na upembuzi yakinifu na uanzilishi wa Sekta Binafsi.

Sehemu ya 5 Mhe. Naibu Spika, ina vifungu 18 vikiweka utaratibu wa Zabuni za miradi na uteuzi wa Muwekezaji Rasmi ukijumuisha hatua za uteuzi wa Muwekezaji Binafsi, Madhumuni Taratibu za Vigezo vya Uteuzi wa Awali. Pia mgongano wa Maslahi, maamuzi ya Uteuzi wa awali, dhamana za Zabuni na Vigezo vya Tathmini.

Sehemu ya 6 Mhe. Naibu Spika, ina vifungu 3 vinavyoelezea maombi yatokanayo na miradi iliyoasisiwa na muwekezaji binafsi.

Sehemu ya saba ina vifungu 15 vinavyoelezea nakubaliano ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ikijumuisha sheria zinazotumika Zanzibar, Umuliki wa Mali, Haki za Matumizi, Masharti ya Fedha, Dhamana za Mali na Mapitio ya Makubaliano.
Sehemu ya 8 Mhe. Naibu Spika, ina vifungu 7 vinavyoweka masharti ya muda kuongeza muda, na kusitisha makubaliano.

Sehemu ya 9 ina vifungu 3 vinavyoweka masharti ya usuluhishi wa migogoro ikijumuisha migogoro baina ya Serikali na Muekezaji binafsi, usuluhishi wa Kimataifa na Migogoro inayohusisha wateja au watumiaji wa huduma wa miundo mbinu.

Sehemu ya 10 Mhe. Naibu Spika, ina vifungu vitatu vinavyoelezea masharti mengineyo yakijumuisha Haki za Wazabuni, Kanuni kufuta na Kubakiza baadhi ya utekelezaji wa vifungu vya sheria inayopendekezwa kufutwa.

Aidha, jaduweli la mswada linaelezea kuhusu miradi ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.
Kwa kuhitimisha Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya. Naomba sasa kuwasilisha mswada huu mbele ya mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kujadiliwa

kuzingatiwa na kupata maoni ya Waheshimiwa Wajumbe, ili hatimae uweze kupitisha na Baraza lako tukufu kwa dhamira ya kuanza kuipokea na kuitekeleza miradi ya mashirikiano yaani *PPP,* kwa lengo la kuleta mabadiliko ya kiuchumi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Shadya Mohammed Suleimna (kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kufika na kuweza kukutana mbele ya Baraza lako Tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo na ustawi wa nchi yetu na watu wake, ikiwemo kupitisha miswada mbali mbali.

Mswada huu ulio mbele yetu, Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya miradi ya maridhiano Namba 1 ya mwaka 1999 na Kutunga Sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi maoni kuhusu Mswada niliokwishauainisha hapo juu.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Kamati, kuishukuru kwa dhati serikali kupitia Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, kwa kuweza kuona umuhimu wa kuleta mswada mbele ya Baraza ili uweze kujadiliwa na kupitishwa na kuweza kufikiwa lengo lililokusudiwa la kuwa na sheria madhubuti itakayoweza kutimiza ndoto za wananchi wa nchi katika kufikia maendeleo ya kiuchumi na Ustawi wa jamii kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo Kamati yangu inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kwa kuwasilisha mswada huu muhimu ambao utasaidia katika kuivusha nchi yetu kutoka kwenye uchumi unaotegemea Serikali pekee katika kuleta Maendeleo na kwa sasa kufungua ukurasa mpya wa mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, dhana na maudhui ya Mswada huu wa mashirikiano baina ya sekta ya Umma na sekta binafsi ni kukusanya nguvu za pamoja katika kuleta maendeleo katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati tulipokuwa tukiujadili na kuupitia mswada huu ambapo waliujadili bila kuchoka, ili kuhakikisha kwamba lengo la mswada huu linafikiwa na hatimaye nchi yetu inakuwa na sheria nzuri itakayoivusha nchi yetu kuelekea kwenye neema.

Mawazo na mapendekezo yao yamewezesha leo hii kufika hapa na kuweza kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu na hatimaye kupitishwa kwa ajili ya kufikiwa lengo lililokusudiwa na serikali kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mjumbe
5. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
6. Mhe. Ashura Sharif Ali - Mjumbe
7. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu, na
9. Ndg. Makame Salim Ali - Katibu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwatanabahisha Wajumbe kwamba marekebisho makubwa yamefanywa na Kamati yangu yamo kwenye orodha ya marekebisho ya Kamati waliyopatiwa, hii ni sehemu ndogo tu ya marekebisho hayo. Hivyo, orodha ya marekebisho hayo pia ni sehemu ya hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, licha ya baadhi ya mambo muhimu ya mswada huu yaliyopendekezwa na Kamati kwa wizara kushindwa kuingizwa kama yalivyopendekezwa, bado kamati yangu imeona umuhimu wa mawazo ya kamati kwa vifungu husika kutobadilika na bado inasisitiza kwamba yazingatiwe ili dhana ya ushirikishwaji baina ya sekta ya umma na binafsi iwe na uhalisia na ionekane wazi wazi.

Mhe.Naibu Spika, baada ya dibaji na tanbihi hiyo fupi naomba sasa nijilekeze kwenye marekebisho ya msingi yaliyofanywa na Kamati yangu kama hivi ifuatavyo:

Kifungu cha 9(3) (c) kinachohusu "Kuanzishwa kwa Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi" kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza maneno na kitasomeka " “awe afisa mwandamizi wa umma au mtu yeyote mwenye uzoefu usiopungua miaka 15 katika masuala ya uongozi" na yaongezwe maneno "kwa mkataba".

Sababu ya marekekebisho haya ni kuifanya Sheria iruhusu kwa mtu yeyote yule mwenye sifa zilizotajwa kwenye kifungu cha 9 (3) (a) na (b) ambaye hayupo kwenye Utumishi wa Umma kuweza kuteuliwa kushika wadhifa huo wa kuiongoza Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa mkataba.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyoelewa sote kwamba nchi yetu ya Zanzibar imejaaliwa kuwa na wasomi wengi sana japo kwa bahati mbaya kwa sababu tofauti wengi wao hawapo Zanzibar kwa sasa, hivyo kuwepo kwa kifungu hicho angalau kitaweza kuipa nafasi mamlaka ya uteuzi kuwa ni wigo mpana katika kufanya uteuzi wa nafasi husika.

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba suala la usimamizi wa miradi mikubwa kwa Watumishi wetu wa serikali kiuhalisia uzoefu wao bado ni mdogo au haupo kabisa kwani kwenye utekelezaji wa miradi hakuna miradi mikubwa iliyosimamiwa na taasisi zetu wenyewe.

Kwa upande wa sekta binafsi kipindi cha miaka mitano tu hasa kwa makampuni yaliyopo nje unaweza kukuta mtu ameshasimamia miradi mikubwa si chini ya mitano kwa wastani wa mradi mmoja kwa kila mwaka. Kutokana na ukweli huo ndio maana Kamati inaona uzoefu kwenye eneo hili bila ya shaka yoyote kwenye sekta binafsi utakuwa upo mkubwa zaidi kuliko kwenye eneo la utumishi wa Serikalini.

Mhe. Spika, Kifungu cha 14 kinachohusu "Muundo wa Kamati ya Wataalamu ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

Katika kifungu hicho Kamati inapendekeza na inashauri kwa msisitizo zaidi kuwepo na angalau nafasi zisizopungua mbili za wajumbe wa kudumu kuingia kwenye Kamati ya Wataalamu ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi. Hivyo Kamati inaongeza kifungu kidogo cha (h) ambacho kitasomeka kama ifuatavyo:

> (h) “Wajumbe wawili kutoka nje ya Utumishi wa Umma”.

Sababu za kuongezwa kifungu hicho ni kwamba Kamati hii ya Wataalamu kwanza si ya kusimamia miradi ya Serikali bali kazi zake ni kwenye miradi ya Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, hivyo kama ni mashirikiano baina ya sekta mbili (umma na binafsi ni busara na ni vizuri kama mashirikiano hayo yakaonekana mpaka kwenye muundo wa Kamati yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kuifanya kamati kuwa na muundo wa upande wa umma pekee itapoteza jina na kuitwa kamati ya serikali na siyo kamati ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, mifano ya muundo unaopendekezwa na kamati yangu ni kwa mfano wenzetu nchi jirani ya Kenya ambao ndio wanaoongoza kwa kufanya miradi mingi na mikubwa ya *PPP* basi wao kamati yao kwanza upande wa serikali ina wajumbe sita na wajumbe wanne kutoka nje ya utumishi wa umma na kuifanya kuwa kuwa na jumla ya idadi ya wajumbe kumi tu wa kamati hiyo. Hivyo bado Kamati inaona hakuna sababu ya msingi ya kukataliwa kwa pendekezo hili la kuingizwa kwa angalau wajumbe wawili kutoka nje ya utumishi wa umma.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 38 (5) kinafutwa na kuandikwa.

> 38 (5) “Kila makubaliano yaliyokusudiwa kukubaliwa kwa mujibu wa Sheria hii, kabla ya kuidhinishwa na Waziri mwenye dhamana na miradi ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi itawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata Ushauri wa kisheria ambao utatolewa kwa kipindi kisichozidi miezi miwili”.

Sababu ya marekebisho haya ni kumpa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nafasi yake ya kuishauri tu Serikali na siyo kutoa maamuzi ama kukubaliwa au kukataliwa kwa mradi wowote ule.

Aidha, Kamati imeongeza kifungu kipya cha 38 (6) ambacho kitasomeka kama ifuatavyo:

Kifungu cha 38 (6)

"Endapo Ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali haujatolewa ndani ya kipindi cha miezi miwili na hakujatolewa sababu yoyote ya kuchelewa huko, itatambulika kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameyakubali makubaliano hayo yaliyowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki.

Sababu ya kuongezwa kwa kifungu hiki ni kuipa muda maalum Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kuifanya kazi iliyopendekezwa kwa muda maalum ili miradi iweze kwenda mbele na bila kutokea kwa ucheleweshaji wowote ule.

Mhe. Naibu Spika, kufanikiwa kwa sheria hii na ili malengo yaweze kufikiwa ni lazima utaratibu wa sasa wa asilimia kumi (10%) uweze kuondoka. Bila kuondoka kwa tabia ya kudai *10%* basi hakuna mwekezaji atakayekuja kuwekeza nchini kwetu na wawekezaji hao hao watakimbilia sehemu nyengine kama Kenya na nchi nyengine zinazotoa vipaumbele na mazingira mazuri zaidi kuliko yetu sisi.

Aidha, Kamati inashauri kupitia sheria hii kuwekwa vivutio maalum (*incentives)* vya kuweza kuwavutia wawekezaji kuwekeza kwenye miradi ya mashirikiano kwa njia tofauti kama ambavyo wenzetu wanafanya.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine kuhusiana na uvumbuzi wa miradi kamati inashauri kwamba lazima ilindwe ili kushajihisha watu na sekta binafsi kubuni na kutekeleza miradi kwa ufanisi zaidi na pia kulinda haki zao za ugunduzi.

Mhe. Naibu Spika, kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na jinsi mswada ulivyo ila bado kuna haja ya kujifunza zaidi kwa nchi za wenzetu ambao wameanza zamani kwenye miradi hii ya *PPP* ikiwemo nchi ya Nigeria, Ghana, South Africa, Mozambique na Kenya kwa upande wa Afrika ya Mashariki.

Mhe. Naibu Spika, ni matumaini ya Kamati yangu kwamba kuwepo kwa Sheria hii ni hatua nzuri na ya kihistoria kwa nchi kuelekea safari ya kuleta maendeleo endelevu na ya haraka kwa wananchi na nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumalizia hotuba yangu naomba kwa mara nyengine tena kuikumbusha Wizara pamoja na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu juu ya vifungu vya 9 (3) (c),

14, na 38 (5) na 38 (6) kuungana na Kamati ili dhana nzima ya mashirikiano baina ya sekta ya Umma na binafsi iweze kufikiwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wangu wa Kamati kwa kuweza kunipa mashirikiano muda wote hadi kuweza kukamilisha ripoti hii ya Kamati yako.

Mhe. Naibu Spika, aidha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa na wa hali ya juu, kwa niaba ya Kamati na baada ya kuingizwa kwa marekebisho hayo naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Kaimu Mwenyekiti kwa niaba ya kamati yako. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wangu doctor na Katibu wake kwa kutuletea Mswada huu wenye mantiki kubwa hasa lengo la kuwapa fursa nzuri hawa wawekezaji wetu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu umekuja kwa wakati mzuri. Kwa kuwa wananchi na hasa na wazalendo wana lengo kubwa la kutaka kuwekeza. Sasa hii *PPP* ndiyo ambayo itawapa fursa nzuri ya kuweza kuwekeza kwa mujibu wa sheria hizi ambazo tulizoleta za marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, wawekezaji wetu, na tukija na wawekezaji wa nje ambao nao ni *target* kubwa kwa Serikali, kwa sababu ni sehemu ambayo moja kubwa sana na ambayo tunategemea kupata hasa yale mambo tunaita kodi; kodi zinazofanya nchi ikawa nzuri na hasa katika masuala yale ya mambo ya wananchi kama njia, afya, mshahara na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, lakini unajua sasa hivi nchi za wenzetu wanakuwa wamo katika ushindani wa mambo ya uwekezaji. Ni vizuri sana kwa kuwa sasa hivi tumefungua milango ya uwekezaji katika hii Zanzibar, kuna wengine huwa wanajiuliza sheria zikoje zitamlinda vipi, haki gani ambayo itakayompa yule mwekezaji inapokuwa kuna tatizo limemtokezea katika uwekezaji. Tulijaribu kuweka vifungu vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, sasa sisi tatizo letu moja zuri, katika Kamati yetu ina mtaalamu ana sifa zote na kumbukumbu zote. Hilo kwanza tumpongeze sana Mhe. Ali, hilo siyo siri na hata mwenyewe Katibu wangu wa Wizara hii na doctor mwenyewe walikiri. Kwa sababu unapotunga sheria lazima zile sheria ziowane na nchi jirani; nchi za Jumuiya ya Madola na nchi ambazo zilizokuwa tuna udugu nao wa karibu, zinazoendana vizuri na hili suala la *PPP*.

Mhe. Naibu Spika, nimsifu sana mzee wangu alikuja na sheria zote za Kenya, Tanzania Bara, hata Commoro nazo ndiyo huko huko nyumbani haiwezi kuwa kote Mzee Ali kuwa nazo. Mhe. Naibu Spika, alijaribu sana mheshimiwa wangu Mzee Ali kutaka kutusomesha hali halisi ya kuona jinsi gani tunaweza tukalingana na zile nchi na tukatoa sheria ikaweza ikasaidia, kwa sababu hivi Kenya wanatushinda sana katika uwekezaji kwa sababu zao zipo wazi kabisa,

zimetoa fursa, zimewatia kwenye Bodi ya kuwekeza kupata ushauri na wao na hili Serikali wameliona, na wamelikubali. Wenzetu wana wanne, sisi tuna watu angalau wawili, wasikivu sana na hasa Katibu wao.

Mhe. Naibu Spika, maana yake unajua ofisi au wizara inaongozwa na *doctor*, basi ujue hakuna kitu ambacho kitakuwa kinafeli. Halafu chini yake akiwa kama na *master* na ana digrii. Kwa kweli tulikwenda nao vizuri sana ilichukua siku nne Mswada huu, kwa sababu ni Mswada ambao ni mzito ambao unaotaka kuleta sura mpya katika nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kuna vifungu tulivikubali kuwa mtu atakuwa na uwezo wa kukata rufaa ili aweze kufanikiwa katika lengo lililokuwa zuri kabisa. Juzi nilipokuwa nikilalamika, nilimpinga bure tu Mheshimiwa wangu *doctor*, kumwambia kuna kampuni ambayo tayari hapa Zanzibar ilikuja na *idea* yake nzuri ambayo inaitwa *SACRONA*, suala ya kuwekeza umeme wa taka taka na mambo mengine.

Aliniambia mheshimiwa mambo mazuri, mimi nilimkatalia nikawa mkali sana na yeye anajua mimi sifanyi kitu cha mchezo, kwa sababu vitu ambavyo vinavyotia tija katika nchi hii sivikubalii kiovyo ovyo tu. Lakini nimshukuru sana Mheshimiwa na ninafuta ukali wangu. Ile kampuni hivi sasa tayari, Bodi ya *ZECO* imeshapitisha tunangonjea Waziri asaini.

Sasa imekwenda *within time* na sheria hii ya mkataba, ni sheria hii ambayo iliyoletwa na *PPP*. Kwa sababu tulikuwa tunaambiwa kuwa katika sheria hii inaeleza mtu ambayo anaweza kuwa *idea* yake, halafu akiipeleka kule na hiyo imepewa sheria tumekubaliana. Waziri kakubali suala hilo, amesema *okay* mtu yule ambaye atapewa nafasi ya peke yake na yale mengine yatatiwa kwenye *tender board* ambayo Serikali ambayo kama Serikali itakavyoona.

Hilo mimi ninakubaliana Mhe. Naibu Spika, ninamuunga mkono kwa asilimia mia kwa mia Mhe. Waziri kutokana na hali ilivyo. Kwa sababu wawekezaji wengine wanakuja na *idea*. Kama sasa hivi, kuna kampuni nyengine ninaileta sasa na ninaanza kuipigia debe ili Serikali iweze kuipokea kampuni hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kampuni hiyo inaleta umeme wa jua. Wenzetu kule Marekani sasa hivi wana mradi wa ondoa giza Afrika. Na mimi ninatamka kuwa ondoa giza Zanzibar. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Naibu Spika, tuvikubalie hivi vitu kwa sababu unajua kila kiongozi anatakiwa awe mbunifu. Tumepitisha sheria hivi sasa hapa ya ubunifu, ubunifu wenyewe unatakiwa utumie akili. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunapokaa, maana yake sisi wengine tupo kwenye *politics* na tupo kwenye *business*. Huu ukweli lazima tuuseme kwa sababu business ambayo inaisaidia ile Serikali yako, siyo *business* inayokusaidia wewe, haiwezekani kwa sababu tunaingia kwenye *internet*. Kwenye *internet* unakuwa unaangalia jinsi gani kampuni inataka kuwekeza pahali,

lakini haijapata pahali. Sasa wewe una *lobby* nao, unaandika nao mpaka munafika pahali wanakubali.

Kwa hivyo Marekani wamekuja tena kutaka kuwekeza suala la *solar*. Mhe. Naibu Spika, ni mradi mzuri, tena *very cheap* huo, hawataki *single cent* ya *government*, wala hawataki kile kitu wanakiita *guarantee*. Wanakuja na zana zao, wapewe eneo lililokuwa zuri. Wenzetu kule Tanzania Bara tayari wameshawapokea kwa mikono miwili kabisa, tena nilishangaa sana.

Mhe. Naibu Spika, *wallahi* mimi ninaamini ingekuwa *approve* anapewa Mheshimiwa wangu *doctor* Mwinyingi, basi na *wallahi* na yeye angewapokea *immediately*. Kwa sababu *doctor* ametembea nchi nyingi sana huyu, aliona hiki cha kuona alete vitu hivi, anakutana na watu wa *DIASPORA* mara kwa mara. Ningependa sana na ndiyo nimevutiwa na sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, tungeomba sana apewe *main power* ya *immediately* kabisa, anaona wakati mradi huu unafaa basi aweze kuwapokea kwa kuwasaidia Wazanzibari. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kwa kweli masuala ya umeme nchi yetu bado ipo giza kabisa Zanzibar. Umeme wenyewe unakuwa *power* zake ni ndogo sana, *over load* imekuwa kubwa, watumiaji wamekuwa wengi, halafu hata bei bado haijawa ya kuridhisha ni bei ambayo wanyonge hawana uwezo wa kuweza kumiliki ule umeme.

Mhe. Naibu Spika, sasa makampuni yakiwa kama matatu tu yasije mengine baada ya hayo, itakuwa tayari umeme umeshapunguka bei. Sasa sheria hii imetoa upana huo, makampuni yaje. Serikali mambo mengine itashindwa kuyatekeleza wataitisha Bodi. Serikali lazima siku hizi isiwe choyo, maana yake niseme Mhe. Naibu Spika, haiwezekani kuwa na uchoyo. Serikali haina uchoyo kwa sababu ndiyo madhumuni ya Mswada huu kuwa pale tulipokosea au tulipobana, sasa madhumuni yake makubwa ni kuachia milango wazi na hii ndiyo shughuli yetu nzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningeomba kuuliza suala moja. Mhe. Naibu Spika, kuna makampuni mengine hapa hayakukubalika. Je, Mhe. Naibu Spika, katika sheria hii wanaweza wakakata rufaa, tena wakaleta mambo yao ili wakaweza Serikali kuangalia vizuri kabla hatujaweza kuwalisha hasara.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tukenda katika mambo ya utalii kuna miradi mingi sana watu wengine wamekuja hapa wamefutiwa ardhi zao kinyume na utaratibu na watu wanataka kuweka miradi mikubwa ya *five star*. Sasa watu kama wale ambao tayari wanatafuta ufumbuzi wa kuweza kufuata sheria, hajaanza kushitaki kwenda katika vyombo vya sheria, hawajaanza ku-*provoke* katika nchi zao kama Zanzibar ina hivi na hivi, isipokuwa tu wanatafuta ufumbuzi wa *silence* kabisa. Je, Mhe. Naibu Spika, katika sheria hii unawapa *power* ya kuweza ku-*return back* tena kuja ku-*apply* tena na vyombo ambavyo vinavyohusika vikaweza kusaidia. Sasa moja agizo langu naomba hilo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini la pili niombe sana ushauri ninaanza kutoa. Mhe. Naibu Spika, tunaunga sasa hiyo tayari na ofisi hii tuna tatizo sana na hili tukitaka tusitake tulikubali. Mara nyingi sana tukiunda ofisi tunapenda kuzikandamiza katika sehemu ambazo ni finyu.

Mhe. Naibu Spika, hii ofisi siyo ya mchezo. Kwanza ningeomba tuwe na *standard office* ambayo itaweza kuonesha na hii dhana yenyewe ambayo kwa sababu dhana hii *total* kabisa inathibitisha kwenye madola. Maana yake tuseme watu ambao ma-*foreigners*, watu wa *citizens* wenyewe lakini iendane. *For example* kama *ZIPA*, jengo lile la *ZIPA* kidogo utaona utasema *yes* hapa *ZIPA* wamejiweka vizuri. Sasa mimi Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana wakati tunaunda sheria hii ofisi yao iwe nje na jengo la aina yoyote ambayo nimekusudia wasiwekwe ndani ya Ikulu, wasiwekwe katika *another office*, maana yake ndani na ofisi nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningeomba tujaribu kuwaweka *independant* kabisa, tuwatafutie eneo lao zuri au tutafute jengo ambalo kwa ovyo ovyo tuliondoe tulifanyie ukarabati mzuri, mule unatakiwa ziwemo *sytem* mule, kompyuta za kileo, vitu ambavyo vinavyokwenda na wakati, *internet full time*. Kwa sababu pale nyinyi kazi yenu kuangalia tu duniani kuna nini na wakati wowote munakuwa tayari munapokea na kutoa. Sasa mimi ningeomba sana kuwa hilo nilikuwa naona nilisemee ili tuna tabia moja ya kuwa tunaunda hii sheria, halafu baadae tunakuwa tunaitupa.

Mhe. Naibu Spika, lakini pili niombe sana katika sheria hii kabla ya Mhe. Rais mara nyingi sana anakuwa anakawia kutia saini kwa *experience* yangu. Lakini niombe kitu ambacho ni cha msingi na cha muhimu, kabla ya hapo basi ningeomba sana maafisa wetu wakapewa *training* au wakapewa mafunzo wakatolewa nje ya nchi kwenda kuangalia *example* ya wenzetu ambao wanaokuwa wana vitengo kama hivi. Ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, tuji-*prepare* katika hatua hizo ili watu watakapokuja hata ofisi itakapokamilika, kwa sababu kwa kukamilika kwa ofisi hii siyo jambo ambalo la jana na leo.

Mhe. Naibu Spika, ninaomba sana Mhe. Waziri ni msikivu sana. Kwa hivyo naomba sana hili suala ni lazima tulitilie maanani kuwa hawa watu wetu maafisa, unajua mara nyengine hupendelea maafisa wa aina gani. Hebu sasa hivi Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri onesha *example*. Mara nyingi sana Mhe. Naibu Spika, tunapenda kuwachukua watu kutoka *department* hii tukatoa *department* hii, tukawekeza pale. Mhe. Naibu Spika, ile kwa kweli mimi sifurahiki nayo. Kwa nini nikasema sifurahiki nayo na kwa nini tuna vijana wetu wapo nje *form six*, wana madiploma yao, wana madigrii wapo nje, kwa nini tusiwachukue wale.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini tusiwachukue tusianzie na wale kwa sababu wale unapowachukua, ukiwapika vizuri hawajaanza hata na *single cent*, wanaonja na ukali wa maisha tu huku nje, wanang'ang'ana tu huko.

Kwa hivyo, mimi ningeomba sana mheshimiwa hebu tuanzishe *new*, onesha mfano mheshimiwa *doctor*. Ndio maana ukaitwa *doctor* kwa sababu tayari ni mvumbuzi wa jambo, *PhD* sio mchezo, huipati ovyo ovyo. Sasa na wewe onesha mfano wa hii *department* yako kwa sababu ni kubwa sana. Kwa hivyo wachukuwe wale vijana waliokuwa kwenye maabara waliofika viwango

hivyo. Kwa kweli mheshimiwa utakapochukua watu wengine wataku- *corrupt, I am sure* kabisa nakuambia, hamtokwenda vizuri, kwa sababu wanajua kwa sababu sasa hivi ofisi hii tayari anaweka matumaini kila mtu anaomba dua, wengine wanaanza kwenda kwa waganga ili kuomba mimi kwa hiki kitengo nilichokua nacho kwa vyovyote nita- *shift* kwenda kule.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba wachukuwe ndugu zetu, watoto wetu wako wengi sana nje wanatembea tu na *PhD* zao, wanatembea na *degree* zao, wanatembea na *master* zao hawana pa kuzipeleka mheshimiwa. Sasa tunapoamua kuviweka vitengo kama hivi basi lazima kawachukuwe wale, ninaku- *guarantee one year* utaona ni jinsi gani, kwa sababu kwanza watakuwa na hamu ya kufanya kazi vizuri, halafu utakuwa umewaivisha vizuri kimaadili ya kikazi. Kwa hivyo, mheshimiwa hilo nimeona niweze kupata wazo moja hilo.

La pili, niende katika hawa wazalendo wenyewe wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, ok semina umewapa viongozi hakuna tatizo kwa sababu hawa ndio wapiga debe wa wananchi huko kwenye jimbo. Lakini ningeomba sana kwa makusudi, kwa sababu mara nyingi sana tunapitisha sheria wananchi hawajui ile mantiki.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikuambie kitu kimoja, siwezi mimi nikamsifu mtu pumba tu. Namsifu mtu kutokana na ule uwezo wake. Kuna wawekezaji hapa ambao ni wa mwanzo niliyemuona sasa hivi anataka kuing'arisha Zanzibar hapa ni huyu kijana anayeitwa Tawfiq, ana miradi mingi sana. Sasa hivi anataka kutuletea tule mchele wa Zanzibar, tayari ameshaanza kuingia mwekezaji huyo.

Kwa kweli Mhe. Waziri watu kama hawa ni wa kuwakumbatia na kuwaweka karibu. Anataka kuigeuza Zanzibar iwe katika mazingira ya kuelekea katika *system* za London. Kwa hivyo, Mhe. Waziri watu kama hao lazima tuwape kipaumbele cha mwanzo, sio kitu cha mchezo.

Leo Zanzibar muulize mtu tunalima mchele, watu wanashindwa kusema, hakuna historia, labda historia nitamuuliza Mzee Ali kama Zanzibar ni lini tumelima mchele wa kujitosheleza, labda karne Mhe. Mzee Ali nafikiri atakuwa anajua hii pengine. Lakini yeye anasema Zanzibar lazima tule mchele, tuwe na mchele wetu. Sasa wawekezaji kama hao ndio katika nafasi hizi ni lazima tuwape kipaumbele cha mwanzo. Ikitolewa *order* basi lazima tuwape *priority* wao ya mwanzo, kwa sababu tayari wameonesha hamu ya kuigeuza Zanzibar, kila pembe utaona sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, leo tuna hospitali ile pale ya kimataifa iko Mnazi Mmoja pale, hatwendi tena India. Tulikuwa tunakwenda India mtu anaumwa na udole tu, yeye hapa hapa anakuonesha jinsi gani udole ule utaweza kutibiwa. Kuna zana za kisasa *modern,* hebu waone watu kama hao unawafikiria vipi mheshimiwa. Ni lazima watu kama hao tuwa- *engage*.

Mhe. Naibu Spika, unajua wenzetu kule Ulaya wanaweka nyumba moja kubwa sana, hata Tanzania Bara sasa hivi wana *system* hiyo. Miradi yote wanaiweka katika *Housing* moja, NBC wanawaweka ni rahisi tu. Sisi bado hatujafikia *standard* hiyo, lakini ndio kwanza tunaanza na PPP, sasa hiyo PPP ndio tutakuwa kama wenzetu *housing* moja ambao wenye miradi mikubwa itakuwemo mule ndani.

Sasa hilo ni suala ambalo niombe Mhe. Waziri alikubali, kwa sababu tusingojee aje mshauri kutoka nje. Washauri Mhe. Naibu Spika, tuko wenyewe humu ndani. Hii *system* niliyokuambia hivi sasa Mhe. Waziri kufanya nyumba moja miradi yote ndio hii sasa inakuja PPP, tukawa na jumba moja lenye hadhi miradi yote ya kitaifa itatambulikana pale, ndio wenzetu Bara walivyopiga hatua kwa kufanya hivyo. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana Mhe. Waziri hilo tulifikirie sana.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie sasa nimshukuru sana Mhe. Waziri Dk. Mwinyihaji. Lakini vile vile niende kwa Mwanasheria, nimshukuru na yeye, wanasheria wake tulikuwa nao muda mrefu na tulikubaliana kutoa *challenge*, lakini kulikuja *challenge* moja wanasheria sikupata jibu, naomba leo nipate jibu.

Niliuliza sisi Zanzibar mara nyingi sana tunatumia sheria za nchi gani, lakini bahati nzuri mwanasheria yule simtaji kama mama au baba, alisema kuwa tunatumia sheria za Jumuiya za Madola, nikamwambia kama tunatumia sheria za Jumuiya za Madola, je, sheria hizi za wizara wao wakituletea sheria wanatumia wapi. Akasema sijui, akababaisha.

Sasa Mhe. Naibu Spika, sheria lazima ziendane na mfumo wa kisasa, wizara inapoleta sheria nawaomba sana wawe waangalifu, waangalie sheria hizi zitalingana na nchi gani kama kumbukumbu alizozitoa Mhe. Mzee Ali, halafu watuletee kwenye meza.

Unajua sheria nyingi sana nimejaribu kuzipitia hapa, *Wallahi* basi tu nimesema ndio lakini baadaye nakuja kujuta, kwa sababu najua nimepitisha sheria, nimeangalia kwenye *dictionary*, nimekwenda kwenye *archive* ya Mhe. Mzee Ali hakuna kitu, hakuna iliyolingana na sheria ya nchi nyengine yoyote. Lakini mfumo huu kwa kuwa tulikuwanaye mtu ambaye *standard* kabisa na anakumbukumbu za nchi. Tazama sasa hivi sheria hii ilivyosimama vizuri, sheria hii imesimama vizuri na wajumbe wote naamini hakuna atakaye *challenge*, kutokana na hii sheria imejiandaa vizuri.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, niunge mkono kwa asilimia mia moja pamoja na watu wa Jimbo la Kitope, hii yote ni elimu kutoka Jimbo la Kitope, hakuna mtu mwengine anaweza kunipa elimu nyengine, ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naunga mkono.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa fursa ya kuzungumza machache katika sheria hii inayokuja mbele yatu. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba keshaisifia sana na ametuomba na sisi tuisifie, isipokuwa kidogo tutataka maelezo.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii imekuja wakati mzuri kidogo kwa kuona kwamba ipo haja sasa ya serikali kuongezewa nguvu na watu wengine, kwa sababu yeye mwenyewe kiujumla imeshindwa. Sasa kama watatokea wengine wakaona ipo haja ya kufanya hivyo, sasa watakuwa na uhuru wa kufanya hivyo wa kushirikiana na serikali.

Mhe. Naibu Spika, tulipokuwa tunawezeshwa juzi, Mwezeshaji wetu alikuwa anatokea Marekani na yeye anasema anafanyakazi *World Bank* na twabaan Marekani ni nchi moja ambayo kwa ujumla tunaielewa kiuchumi na kisiasa ilivyo. Alijaribu kutushawishi sana kwamba sheria hii ikipita labda nchi yetu nayo itanufaika kwa maendeleo ya kiuchumi.

Pia katika maelezo yake alitumia neno moja mara nyingi alikuwa analikariri kariri, neno ambalo kwa Kiingereza ni *myth.* Sasa *myth* kwa Kiswahili ni imani ambayo unaijenga lakini ukweli wa imani ile haipo. Labda nitowe mfano kwa imani waliyokuwa nayo wenzetu wa Kinjeketile wakati wa vita vya maji maji, wao waliaminia kwamba ukinywa maji yale basi risasi za Mjerumani hazitokupata au zitapita tu hutokufa. Matokeo yake sio kweli, waliokuwa na imani ile au hiyo *myth*, walipokwenda kwenye mapambano risasi zikawaingia mwilini na wakafariki.

Sasa hii *myth,* labda na mimi nione tu kwamba kwa vile walituletea neno hili alikuwa na maana yake kwa sisi tuliopo Zanzibar kwamba huwenda na sisi ikawa tunajenga hiyo *myth*, kwa sababu Marekani kama ni mfano waliotupa ni nchi moja ambayo kuna *good governance* na kuna uwazi.

Sasa sisi nina imani kwamba hatujawa na hiyo *good governance* na huo uwazi wenyewe. Sasa ikiwa ndio hivyo basi hiyo sheria inaweza ikabakia kuwa ni *myth*, ni imani lakini ukweli wenyewe haupo. Kwa hivyo, nina wasi wasi kwamba tunapitisha sheria lakini bado hatujajiandaa kuwepo na huo utawala bora na uwazi katika utendaji wetu.

Mhe. Naibu Spika, labda mimi kwanza kidogo nianze huku kwenye jadweli na ndio ninakopata wasi wasi kwamba labda sasa tunaingia katika hiyo *myth* wenyewe. Katika jadweli tumeorodhesha baadhi ya mambo ambayo yatakubalika katika kuingia miradi ya mashirikiano, na yo ni usafiri wa reli na mfumo mwengine wa usafiri usiokuwa wa reli na huduma. Hapa Mhe. Naibu Spika, tumeshajenga wazo kwa imani yangu kwamba hivi Zanzibar kweli tunaweka la mwanzo iwe ni reli na sio usafiri mwengine. Mhe. Mwanasheria hebu nisaidie kwa nini imefanyika hivi, kwamba reli tuna wazo la kwamba tuwe na reli kabla ya kushughulikia usafiri wa aina nyengine.

Kwa hivyo, ningemuomba waziri akaiunda vingine hii, akaitafutia lugha nyengine, lakini hii lugha ya kwamba tuanze na reli, mimi nahisi kwamba tutakuwa tunajenga hicho kitu kinachoitwa *myth,* yaani ni imani ambayo haipo. Hebu ondosha hili neno usafiri wa reli, ungesema usafiri wa nchi kavu, angani na baharini, lakini ukisema kwamba usafiri wa reli, siju kama umeshafika wakati wa kuwa na sisi tuwe na reli iwe ni kipaumbele cha mwanzo kulikoni huo usafiri wa hiki chengine.

Mimi nafikiri Mhe. Waziri hii sentensi ungeiweka vizuri ikawa ni usafiri wa nchi kavu, baharini na angali, lakini ukiweka neno reli inajenga imani nyengine ya mwanzo na hapo mimi ndio naanza kusema kwamba hapa sasa tunaingia katika hiyo *mirth* ambayo haitawezekana.

Mhe. Naibu Spika, niende tena kidogo niangalie kifungu cha 45. Kifungu hiki kiko chini ya makubaliano ya ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi, na kifungu hiki kinasema makubaliano yataongozwa na sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, isipokuwa kama makubaliano yataelezwa vyenginevyo. Sasa mimi napata wasi wasi hii vyenginevyo inakusudia nini, kama sheria ilikuwa inasema kwamba itaongozwa na sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, basi kwa nini tusi- *stick* hapo tu, hizo sheria nyengine zinatoka wapi au ni sheria zipi hizo nyengine ambazo zitakuja kinyume na hii sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Pia kifungu cha 2 kinasema, mwekezaji binafsi, wanahisa wake na wafanyabiashara wengine watakuwa huru kuchagua sheria zitakazoongoza. Sasa sheria gani zitakazoongoza zaidi ya sheria hizi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, namuomba waziri hebu kidogo anipe uelewa hapa kakusudia nini anaposema kwamba sheria hizi watakuwa na uhuru wa kuchagua sheria zao wao wenyewe wanahisa na sio sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sasa hapa ndio najenga hoja kwamba hapana ujanja ujanja katika sheria hii, kwa nini tusi- *stick* moja kwa moja tukasema sheria zitakazoongoza mambo haya ni sheria ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zije sheria nyengine ambazo zitakazokubalika na wanahisa wa mambo hayo.

Mhe. Naibu Spika, nije kidogo katika kifungu cha 10 ambacho nacho kinafuatiwa katika mfumo wa kitaasisi na majukumu. Kifungu hiki cha 10 kinasema,

Kifungu cha 10

"Idara kimsingi inahusiana na kusimamia dhima za kifedha na makubaliano"

Sasa mimi imani yangu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba katika makubaliano yetu inawezekana kwamba sekta binafsi ikachangia pakubwa zaidi katika utoaji wa hiyo huduma na serikali pengine ikawa yeye ina *portion* ndogo tu katika uchangiaji wake. Sasa ukiweka *control* kwamba iwekwe kwa serikali ya kifedha, idara isimamie mambo hayo, yule ambaye atakuwa ame-*contribute* au amechangia pakubwa. Yeye atakuwa na imani gani kwako wewe kwamba um-*control* kiasi hicho. Nafikiri kipengele hiki labda kinaweza kikaweka kizingiti kwa hawa ambao wanataka kuja kuingiza pesa zao kuchangia na serikali ili kuanzisha huduma yoyote ile, wakaleta wasi wasi kwamba kwa nini sisi fedha sisi ndio tulio- *contribute* kiwango kikubwa. Lakini sasa iwe idara itakuwa na mamlaka sisi ya kutuchunguza tutafanya nini, baada ya wao labda katika makubaliano yetu, kungojea sisi nini makubaliano yetu tumeambiana kwamba sisi kwa wewe unatakiwa mwaka gawiwo lako litakuwa kiasi fulani, lakini waingilie mambo ya ndani ya kifedha ambayo wao watakuwa na mchango mdogo tu.

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi ndipo ninapopata wasi wasi sasa kwamba sasa je, labda pengine hizi fedha wao wamechangia fedha ya serikali inatakiwa sawa iidhinishwe na itakuwa na wajibu wa kuangaliwa, lakini fedha ya binafsi je, itakwenda katika sheria gani hata hawa na wao wawajibike kwamba pesa zao zichunguzwe aina kama hiyo. Kwa hivyo, nina wasi wasi kwamba tutakuwa tunaelekea huko huko kwenye *myth*, hao ambao tunawaweka kwamba kuja wao kutusaidia katika sekta hizi wakaleta wasi wasi wa kutokukubaliana na sisi katika utaratibu wetu ambao tumeuweka. Haya inawezekana pengine yakawa ni vikwazo au *stabling block* kwa hayo makubaliano ambayo tunakubaliana.

Mhe. Naibu Spika, mimi sikuwa na mengi sana, labda ningesubiri majibu baadaye nikasema kwamba naunga mkono au nakataa hoja hii.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo sana katika mswada huu wa sheria ya kufuta sheria ya miradi ya maridhiano ya mwaka 1999 na kutunga sheria mpya kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu baada ya kuona kuwa kumejitokeza changamoto nyingi katika sheria hii au imefutwa kabisa sheria hii kuonekana kuwa haina maslahi na nchi yetu kwa ujumla. Kwa hivyo, nichukuwe nafasi hii kumpongeza, pamoja na wenziwe wote waliokaa wakaweza kufikiria jambo hili kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu na kwa wananchi wake kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuingia kwenye madhumuni na sababu za kuletwa au kuanzishwa kwa mswada huu. Katika madhumuni Mhe. Waziri ametuambia kwamba kwa kuhakikisha taratibu za mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kuwa na uwazi kiushindani na zisizofungamana na mgongano wa kimaslahi, sheria hii itaongeza idadi kubwa ya miradi ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa kupelekea kukua kwa uchumi na maendeleo, Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni haya ni madhumuni mazuri na mimi nayaunga mkono kwamba ni dhahiri kuletwa sheria kuwa nchi yetu itaondokana na uchumi ulio duni, na kuelekea kwenye uchumi ulio na maslahi ya nchi yetu lakini pia na maslahi ya wananchi wetu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, lakini pia ushirikiano wa baina ya wananchi na katika miradi hii mbali mbali ambayo kuwa italeta uwazi na matumizi bora ya fedha za umma.

Jengine Mhe. Naibu Spika, pindipo mswada huu Mhe. Rais atauridhia na kukuli na kuusaini basi itawezesha makampuni makubwa makubwa ya nje, lakini pia na ya ndani ambayo kuwa italeta ile miradi ya mikubwa na hatimae baada ya kufanyiwa uchambuzi wa kina na upembuzi yakinifu kuonekana kuwa miradi hiyo ina maslahi ya nchi yetu, basi tutapata faraja kubwa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuona madhumuni hayo niaze katika huu mswada katika kifungu hiki cha sita ambacho kuwa kinazungumzia muda wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, kutaelezwa katika makubaliano husika muda wa mashirikiano baia ya sekta ya umma na sekta binafsi utalazimika kuonesha yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi naungana na kifungu hiki cha sita kwa sababu miongoni mwa moja ya changamoto ambayo kuwa hayo yaliyokuwemo katika hiyo sheria ya mwanzo, na kukosekana kwa ufanisi wa miradi mbali mbali katika nchi yetu ni kukosa ule muda au mikataba ambayo kuwa ilimuwezesha yule muwezeshaji mikataba ambayo kuwa ataweza kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi. Kwa hivyo nipongeze sana kuweza kuweka kifungu hiki, hili litatuondoshea matatizo mengi kabisa kuja kwa miradi ambayokuwa haina mikataba maalum, halafu pengine kupelekea serikali kupata hasara kubwa, na iliyokuwa haina tija.

Suala jengine kuna kifungu hiki cha tisa kuanzishwa kwa Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi, kuanzishwa Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya umma na sekta binafsi ndani ya Tume ya Mipango ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba hii tume ni kubwa na ni tume ambayokuwa tutegemee mafanikio kuliko kutofanikiwa, kwa sababu ukisema kuwa hii tume ni ndani ya Tume ya Mipango ya Zanzibar, ina maana sio tume ya mchezo mchezo, na tuwaombe basi tume hii ituletee mafanikio makubwa na ituondolee zile kasoro ndogo ndogo zilizokuwepo katika sheria za nyuma zilizopita.

Kwa hivyo Mheshimiwa baada ya hiyo kuna kifungu kingine cha 10(g) ambacho kuwa kinazungumzia kutoa taaluma kwa umma na kuwajengea uwezo na ufanisi juu ya miradi ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, itajumuisha malengo na utaratibu wake kwa wadau hawa wafuatao.

Mhe. Naibu Spika, wametajwa huku chini lakini pia nipongeze na hili kwa kuanzishwa au kwa kutoa hii taaluma kwa umma ni jambo la faraja, na hili ni miongoni mwa changamoto iliyokuwa ilirudisha nyuma kufeli kwa hiyo sheria iliyokuwepo, kwa sababu wananchi ilikuwa kwa kiasi fulani wanadharauliwa katika shughuli zao za nchi yao. Kwa hivyo hili pia lilipelekea kufelisha kwa vijana kujaribu kuvamia miradi mingi ambayo kuwa ikija hapa lakini pia kwa sababu walikuwa hawana mikataba maalum kupelekea kukosa hata haki zao za kimsingi au jasho lao walilokuwa wakifanya kazi kwenye zile kampuni.

Kwa hivyo kutoa taaluma kwa umma ni jambo muhimu sana kwa hivyo mimi ningemshauri Mhe. Waziri, katika kutoa taaluma hizi kwa sababu tumezoea tunapotaka kuelimisha jamii au kutoa taaluma kwa jamii basi ni kupitia katika ofisi hizi za Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa au kuchukua Masheha kwenda kuwapa taaluma. Lakini taaluma zile hatimae hazifiki kwa wale walengwa, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri Mwenyezi Mungu atakapojaalia haya mambo yakafanikiwa basi taaluma hizi tunaziomba zianze kwenye shehiya na sio kwa Wakuu wa Mikoa wala wa Wilaya, zianze kwenye shehiya ili wale wadau na wao basi waweze kujua nini kinachoendelea katika Serikali yao.

Suala jengine katika kifungu hiki hiki cha 10(g) kuna vifungu vidogo hapa karibuni sita; kuna hiki kifungu ambacho kinaeleza kutatua migogoro. Mhe. Waziri katika hiki kifungu cha tisa kutatua migogoro kwa sababu hapa kuna hii uanzishwaji wa Idara, lakini pia kutakuwa na hii Kamati ya Wataalam sasa hawa watakaotatua migogoro ni hii idara peke yake itakayoanzishwa au itakuwemo na hii kamati ya wataalam. Kwa sababu kama ni Idara peke yake tu basi lazima apatikane mtu maalum aliye na uwezo wa fani hasa ya kutatua hii migogoro, na kama ni hii kamati ya wataalam bado mimi katika hawa wanaoelezwa hapa sijaona kuwa wana utaalam wa kuweza kutatua migogoro.

Vijifungu mbali mbali hapa ni kifungu cha 14 ambacho kuwa kinaeleza kamati ya wataalam, wametajwa lakini pia naona na hawa hawa ni fani ya utatuzi wa migogoro, bali ni watu watendaji wa shughuli zao nyengine muhimu lakini kwa ufanisi wa utatuzi wa migogoro bado.

Hapa Mheshimiwa Waziri uje kunipa ufafanuzi wa hii idara na hii Kamati ya wataalam ambayo kuwa itakuwa na uwezo wa kutatua hii migogoro ni wapi. Kwa sababu ukizungumzia suala la migogoro Mhe. Waziri ni suala ambalokuwa litakuwa ni suala la kutafuta mtu aliyekuwa na ile fani ya kutatua ile migogoro.

Mhe. Naibu Spika, nishukuru tena kwa kunipa nafasi hii lakini pia tena nimpongeze Mhe. Waziri, lakini nimuombe Sheria itakaposainiwa basi jambo kubwa ni usimamizi, hiyo kamati ya utaalam yote inayotajwa ya Makatibu Wakuu bila ya kuwa na ufanisi katika shughuli zetu basi hatwendi mbele na tutabakia pale pale na tutaendelea kutafuta sheria za watu ambazo kuwa hawaoneleani muhali wala hawaoneleani kwamba huyu ni wangu au huyu ni hivi basi

tutaendelea kutafuta sheria hizo na sisi tukisema tuzilete Zanzibar lakini hatimae tutakuwa hatufanikiwi.

Mhe. Naibu Spika, kinachokosekana katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kukosa usimamizi, usimamizi haupo makampuni yakishafika akishapewa onyesho na yale maelekezo, basi watu warudi maofisini mwao hakuna linalofuatiliwa hatimae kinachofanywa watu wanakuja kujuta jambo limeshafanyika, kwa hivyo naomba Mhe. Waziri tujifunze katika makosa ambayo kuwa yametutokea katika Sheria iliyopita.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na mimi sina sababu ya kutoiunga mkono Sheria hii kwa sababu ni mmoja wa kutaka hayo maendeleo na huo umasikini kuondoka katika hiki kisiwa cha Zanzibar. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia Mswada huu, Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Maridhiano, napenda kuipongeza Wizara ya Nchi (AR) Ikulu na Utawala bora kwa kuwasilisha Mswada huu, Mswada ambao unaweza kuleta mabadiliko katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya mradi yameelezwa kwenye mswada huu ni mazuri tu na moja ya madhumuni ya mradi ni kuendeleza miundombinu ya kitaifa kwa mashirikiano baina ya Sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, kuiga mazuri sio dhambi, nchi za wenzetu mbali mbali wamefanya mfumo huu wa PPP ukiangalia wenzetu wa Kenya wanao mfumo huu wanatumia, wamejenga bandari karibu 381 na mafanikio mazuri tu. Ukiangalia Afrika ya Kusini nao wanatumia mfumo huu na duniani kiujumla wengi wanatumia mfumo huu wa PPP, mfumo ambao ushirikishwaji wa sekta za umma na sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na michango miwili tu kutokana na michango mingi kwa sababu tumepewa semina jana tumeelewa vya kutosha, na hata ukiona unauliza majadiliano ndio maana watu wengi wameelewa hata kuchangia wengine wanakuwa hawana, kwa kweli tumeelewa vya kutosha. Mimi nitakwenda katika michango yangu miwili tu nitakwenda katika kifungu cha 14(I) ambacho kinaeleza Muundo wa Kamati ya Wataalam Mashirikiano baina ya Sekta ya na Sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi kinaeleza kamati ya wataalam wa Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi itaundwa na wajumbe wafuatao, wametajwa hapa wajumbe wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Zanzibar ambae atakuwa Mwenyekiti, Muwakilishi atakayeteuliwa kutoka Wizara ya Fedha, Naibu Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu anayehusika na Ardhi wote ni wajumbe hao, Katibu Mkuu anayehusika na Miundombinu, Katibu Mkuu anayehusika na Mazingira pamoja na Mkurugenzi mtendaji wa Mamlaka ya Vitega Uchumi.

Kifungu 14(2), Mhe. Naibu Spika, kinasema Kamati ya Wataalam inaweza kumualika mwakilishi wa sekta ya umma ambaye ni mwenye mamlaka ya utekelezaji wa miradi

iliyobuniwa kwa mfumo wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, manunuzi au makubaliano ili wawe wajumbe wa kamati ya wataalam.

Mhe. Naibu Spika, mimi kifungu hiki nakiunga mkono kwa sababu Kamati hii ni kamati ukiangalia kamati takribani ni ya Makatibu Wakuu na watendaji wao wakuu wa Serikali, kwa hivyo kumleta mtu wa sekta binafsi kuingia katika sekta hii kwanza wewe utakuwa sio muajiri wa Serikali, isitoshe ukiangalia katika majukumu ya Kamati. Mhe. Naibu Spika, naomba niseme majukumu mawili tu ya kamati katika kifungu cha (e) na (f). Jukumu la kamati Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Kamati hiyo ya wataalam inasema kutunza siri zinazohusiana na taarifa muhimu za kibiashara zinazopatikana chini ya sheria hii hadi muda ambao taarifa hizo zitakapotolewa kwa umma.

Nyengine kutunza siri zinazohusiana na mjadala ndani ya Kamati ya wataalam zitakazotokana na utekelezaji wa majukumu chini ya aya (a) hadi (d) na kifungu cha 13 cha Sheria hii. Kwa hivyo hapa nashauri Mhe. Naibu Spika, hiki kifungu kinajitosheleza kama atahitajika mtu kutoka nje kama kwenye sekta binafsi ambaye anatakiwa utaalam wake, huyu mtu anaweza kualikwa tu akaja akatoa ushauri wake, akatoa utaalam wake na yakachukuliwa maoni yake lakini sio kutoka mjumbe nje ya Serikali akaingia katika kamati hii. Hii ni kamati ya watendaji, ni kamati ya wataalam, kwa hivyo mtu wa nje ataitwa kama mshauri tu wa kutoa ushauri wake na utaalam wake.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika kifungu cha suala zima la elimu; unajua kuna miradi mingi inakosekana ufanisi kutokana na kutopewa elimu mwanzo watu kabla ule mradi haujaanza. Nasema hivyo kwa sababu katika mafunzo tuliyopata jana alitoa mfano hapa Afrika ya Kusini kulijengwa barabara nyingi kupitia mfumo huu wa PPP, lakini walianza mradi bila ya kuwaelimisha wale wananchi katika maeneo husika, matokeo yake hata ule upokeaji wa watu kupokea ule mradi umekuwa ni mbaya. Wakiambiwa kuchangia wanakuwa wanakataa kutokana na kutokuelewa madhumuni mazima ya mradi ule, lakini nilikuwa naomba kipengele hiki kimo katika sera, kimo katika kipengele cha *capacity building,* ni vizuri na naki-*support* kwa kuwa kimo lakini ni vizuri elimu ikatolewa kabla ya huo mradi kuanza.

Kwa sababu mradi ukianza wakipata elimu hao wananchi katika maeneo husika, kwanza wataona huu mradi ni wao hata ukitokea uharibufu wowote wananchi wanaweza wakatoa taarifa katika taasisi husika na wao watakuwa walinzi wa ule mradi katika maeneo yao. Kwa hivyo suala la elimu ni muhimu. Ni muhimu katika mradi na suala hili lianze kabla hata ule mradi haujaanza kutekelezwa elimu itolewe.

Mhe. Naibu Spika, mimi kama nilivyosema vipengele vyangu viwili tu, nakubaliana na mswada huu, vipengele vyote vilivyokuwemo humu na naunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutupa uhai na uwezo wa kuondoka katika maeneo yetu hadi hapa.

Pili nadhani mimi mwenyewe nitakuwa mchache wa shukurani kama vile vile sikutumia fursa hii kukushukuru wewe kwa kuweza kunipatia na mimi dakika chache sana za kuweza kutoa mawazo yangu kwenye hii hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, uliopo mbele yetu ni Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano Nam. 1 mwaka 1999 na Kutunga Sheria Mpaya kwa Ajili ya Kuanzishwa na Kuendesha Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Naibu Spika, kama kuna jambo moja kubwa sana na muhimu na zuri ambalo serikali imefanya ni kufuta hizi sheria na kufuta hizi mpya. Kwa mnasaba huo napenda nichukue fursa hii, kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuweza kutuletea Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, nimelazimika kutoa pongezi hizo, kwanza na-*declare interest* kwamba mimi ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati iliyojadili Mswada huu, kwa hivyo nimetumia muda mwingi sana katika Kamati. Hapa kitakachobakia ni kutia tia nyalio tu, mchango sana nimeutoa kwenye Kamati yangu,.

Waheshimiwa kwa kweli Mswada huu ni mzuri na kwa vyovyote vile kama kuna baadhi ya mambo humu, kama ambavyo kamati yangu ilieleza serikali kama itafanyiwa marekebisho basi mimi naamini Wazanzibari watapata kile wanachokihitaji.

Mhe. Naibu Spika, sheria hizi zilizopita ambazo tunazifuta, zimeshindwa kabisa kabisa kusimamia miundombinu. Kama ilivyoeleza madhumuni ya mswada huu katika ukurasa wa 380. Madhumuni ya kuletwa huu Mswada ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya nchi, kwa mashirikiano ya serikali na sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, kama kuna kitu muhimu ambacho kinaweza kuinua uchumi wa nchi ni *infrastructure,* hiki ni kitu muhimu sana katika maendeleo ya nchi. Serikali yetu kwa kipindi kirefu ilikuwa ikijipiga kifua peke yake, jambo ambalo kwa kweli katika mambo mengi walikuwa wanashindwa kukamilisha. Kwa mfano katika kipindi kirefu hapa tulikuwa na matatizo ya miundombinu ya viwanja vya ndege hasa pale Pemba, ilikuwa ni tatizo na mpaka sasa bado ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kiwanja kile serikali iliahidi kutia mishumaa, maana haina taa lakini tukaambiwa itaingizwa mishumaa. Lakini kiwanja kile mpaka sasa hivi taa hamna na hata hiyo michumaa imeshindwa kuingizwa. Hii ni kwa sababu serikali peke yake yaiwezi kufanya jambo. Mimi naamini hapa kuna watu ingelikuwa sheria hiyo imeshapita, basi naamini kuna watu ndani na nje ya nchi tayari uwanja wa ndege wa Pemba achilia mbali kutia mishumaa kama ambavyo imedaiwa siku za nyuma, wao wangetia taa na kuufanyia ukarabati wa hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nawanasihi sana kwamba sheria hii tuipitishe kusudi tuweze kuendeleza ile miundombinu kama dhamini ya Mswada huu ulivyo. Kwa mfano uwanja wa ndege wa Pemba, siku zote tulikuwa tukipigwa maneno hapa na Waziri wa Fedha, uwanja wa ndege sijui umeshakuwa tayari, sijui mkandarasi keshakuwa hivi, sijui keshafanya hivi, hakuna lolote lililotokea. Ni kwa sababu serikali peke yake haiwezi kufanya jambo, tukiongeza na hawa basi

naamini mambo yatakuwa mazuri, kwa hivyo tuupitisheni huu Mswada kusudi na sisi tuweze kunufaika pale.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa hivi tuseme Mhe. Waziri, laiti ingelikuwa yeye mwenyewe ana wake wawili na mmoja yupo kisiwa cha Pemba na ikafika saa moja ya usiku hajasafiri, basi ingekuwa haipo tena zamu yake kwa siku ile kule Pemba kwa sababu ya miundombinu ya nchi tumeshindwa kuifanyia marekebisho. Sasa naamini serikali ikishirikiana na sekta binafsi, Rais akisaini Mswada huu watajitokeza wengi na hapo ndipo itakapowapatia wananchi kile wanachokihitaji.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi kabla ya Mswada huu kuletwa nilikuwa nina mradi mkubwa na nimeanza kuutia huku chini watu wanaupiga piga mateke huku. Nilikuwa nina mradi mkubwa sana ambao naamini sheria hii ikishaanzishwa, nitaupeleka serikalini ili tuweze kushirikiana na serikali katika kuwapatia wananchi unafuu katika mambo kadhaa. Mimi nina mradi wa *Schistosomiasis Biological Centrol* ni mradi huu hautumii mahela mengi kama serikali wanatumia *thermotherapy* kuweza kutibu mambo ya kuifanya Zanzibar iwe *free millennium zone* wametumia pesa nyingi. Mimi ninahakikisha mradi wangu nikiupeleka serikalini tukishakupitisha sheria hii kwa kushirikiana na serikali tunaweza kuifanya Zanzibar *free from Schistosomiasis*. Huu ni mradi ambao baadae nitauelezea sana kama Mhe. Makame Mshimba mradi ule wa umeme, mimi naamini wangu utakwamuka. Ni mradi unaotumia Biologia tu wala hutumii Kemikali, unachukua chonjwe unawaweka katika maziwa wale wanakula kowa, baada ya muda kowa hakuna na kichocho hakuna kabisa kabisa, *without snails no schistosomiasis* nimeshafanya sana *feasibility study* lakini peke yangu nilikwama na serikali ilikuwa haina sheria ya kusimamia hili. Naamini itakapopitishwa sheria hii mradi huu wa *Schistosomiasis Biological Control* utafanikiwa sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani msije ukagati gati kuipitisha hii sheria. Hapa ingelikuwa sheria hii ipo zamani inafanya kazi, basi Mradi wa Mhe. Makame Mshimba wa kutumia zile taka taka kupata umeme, tungekuwa mbali sasa hivi. Mbali na ule kutoka Tanga basi ungechanganyika umeme wa Tanga na wa Mhe. Makame Mshimba pale, naamini tusingeshindwa hata siku moja ukumbe wetu umeme. Sasa hii sheria tujitahidi kuipitisha kusudi tuwe na muangaza wa kutosha hapa.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika hiki kifungu Nam. 14, kinachohusu muundo wa Kamati ya Wataalamu ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi. Hapa nikiwa kama Makamu Mwenyekiti wa hii Kamati, lazima tukubali tulivyokubaliana. Tumekubali kutokukubaliana katika Kamati, tumekubali kutokukubaliana na serikali pale ambapo tuliwataka waingize watu wawili nje ya sekta ya umma wao wamekuwa *very rigid*.

Mimi naomba serikali isibabaike katika hili. Huu ni utaratibu wa kawaida, wa kuingiza watu katika *decision making* na hii ndio demokrasia na *transparency* pamoja na Utawala Bora. Mnapowaingiza watu wa sekta binafsi katika *technically committee* mtakuwa mmetekeleza kwa vitendo, ile dhana ya utawala bora. Msihofu na kama wanatujibu eti kwamba kutakuwa na zile *personal interest*, msijali tutawalisha viapo hawa, ukishakuwalisha viapo hawa hawatoi siri, hawa kutoka sekta binafsi, hata siku moja hawatatoa siri.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo serikali nawaombeni sana katika hili, yaani sisi hii sheria tunaihitaji sana, lakini jitahidini na nyinyi msiwe wakaidi, hichi kifungu Nam. 14 muingize watu wawili, tena mtaweza kuvuna sana. Wenzetu Kenya wamefanya hivyo katika sheria yao, sisi tunaogopa nini. Mnaweza mka-*import* watu wakaja wakawa *technically idea*, wakiwa *permanent member* katika hii Kamatim kuna wataalamu wengi *DIASPORAS* mnaweza mkawa-*invite* hapa wala sio dhambi. Sio kuwa- *invite* tu kuwaingiza katika Kamati hizi, hata wale *DIASPORA*.

Kuna jamaa mmoja yeye ni *Interpol* lakini anafanya kazi yake vizuri sana, basi Rais Kikwete akaamua japo hayupo nchini hiyu nimchukue awe IGP, akaondoshwa huko alipokuwa akaja akapewa u- IGP Bw. Said Mwema na akafanya kazi kwa umakini wa hali ya juu sana. Sasa kwa mfano una jambo la kompyuta hapo una mradi mkubwa wa mkongo wa mawasiliano ukasema unakwenda kumchukua Hassan Omar Ali, *specialist* kule Americ umlete hapa itakuwa umefanya kosa! sio kosa Mzee Said Mwema kaletwa hapa Mzee Kikwete kutoka kwenye *Interpol* akaja akawa IGP. Je, kuleta mtu ukaja ukamuingiza hapa.

Mimi nadhani katika hili msiwe na shaka, tuwaingizeni hawa ili watu wawili, serikali msiwe wakaidi. Mtu ni yule asemwae akasemezeka kabisa. Tunawanasihi sana, sisi hii sheria tunaihitaji mno. Miradi yetu mengine tunayomfukoni hivi sasa. Mkitia *sign* tu hapa sisi tunaleta miradi yetu tunashirikiana hapa. Sasa tujitahidini sana Waheshimiwa na mimi kwa sababu ni Kamati yangu na tumeshajidili na tumekorofishana kidogo tu katika kipengele hichi. Naomba sana serikali mkubali kufanya hilo na muone kama hilo ni muhimu sana kuwapata watu nje. Kwa sababu ukiangalia hii kamati wote hii ni wa serikali watupu, msiyaogope haya mawazo ya nje. Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa Wajumbe naamini na nadhani mmenifahamu sana maelekezo yangu kuhusu kipengele hiki.

Nawaombeni sana serikali tuzidi kuisindikiza hapa, iweze kuingiza watu wawili nje ya sekta ya serikali na hatimaye tuupitishe huu Mswada mia kwa mia. Baada ya maelezo hayo na baada ya marekebisho ya Kifungu Nam. 14 basi mimi nitaunga mkono hoja mia kwa mia, asante.

Mhe. Naibu Spika: Asante Mheshimiwa tunamalizia na mchangiaji Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, asante na mimi kwa kunipa fursa hii kwa kuchangia Mswada huu lakini ningeomba nichangie jioni kwa sababu muda haunitoshi na mimi nina mengi ya kuyazungumza. Kwa hivyo naomba nije nichangie jioni.

Mhe. Naibu Spika: Sasa hakuna mchangiaji, anza utamalizia jioni. Anza dakika 10 utamaliza halafu utakuja kumalizia jioni. Si ndio utaratibu bwana1

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Muda hakuna Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Hizo tano naanze atakuja kumalizia jioni.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia machache katika Mswada huu. Kwa kweli Mswada huu kama walivyokwisha kuchangia wenzangu kwamba ni Mswada mzuri, ambao sasa unataka kutukwamua sisi wananchi wa Zanzibar pamoja na kufanikisha mambo mengi katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya

Zanzibar. Mbali na maoni ya Kamati ambayo wametoa maoni yao na hiyo ni moja ya juukumu la kamati hizi, kufanya kazi zao kwa ufanisi, kwa mujibu wa kazi zetu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii ni nzuri na madhumuni yake tumeyaona kwamba ni kufuta sheria ile iliyopita ambayo na sasa hivi tuna sheria ambayo inasema kwamba Kufutwa kwa Sheria ya Mradi wa Maridhiano ya Mwaka 1999 na Kutunga Sheria Mpya kwa Ajili ya Kuanzisha na Kuendesha Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi na Mambo Mengine.

Kama ulivyoonyesha Mswada huu kwamba unavifungu vingi tu na una Sehemu Kumi. Vifungu ni vizuri na vina ufafanuzi. Kwa sababu tunataka mafanikio ya ushirikiano huu baina ya serikali pamoja na sekta za umma, kwa kweli niiyombe serikali kama serikali ni jukumu lake la kuleta maendeleo katika nchi hii na sasa hivi inataka kwenda kuendesha kwenye ushirikiano na sekta za umma. Jukumu hili lilikuwa ni la serikali na tunaona kwamba sasa hivi tunataka kubadilika kama wenzetu wa nchi mbali mbali, wameanzisha ushirikiano huu wa serikali pamoja na sekta za umma. Mbali ya kwamba nchi yetu hii ni historia tunaiyona kwamba ni nchi ambayo inafuata maridhiyano ya kimataifa. Kwa hivyo ni lazima na sisi kama sehemu ya ulimwengu ni lazima tuyafuate haya.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza naunga mkono Mswada huu, hatuna sababu ya kwamba tusiupitishe, una mambo mengi sana, hasa pale niliposoma kwamba serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imesheweka kipaumbele katika kuendeleza miundo mbinu ya kitaifa kwa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kukuza uchumi endelevu na maendeleo.

Kwa kweli jambo lolote likiwa sio endelevu basi linakuwa halina faida na ni lazima tupate jambo ambalo litakuwa endelevu. Maendeleo ni lazima yawepo, maendeleo ya sekta mbali mbali na mambo mbali mbali. Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, sheria hii.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa utamalizia jioni. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha kuna tangazo hapa limeletwa na Katibu wa Wanawake wa CCM, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, anasema kwamba Waheshimiwa wote wa CCM wanawake tukiahirisha kikao mbakie kwa muda kuna mambo muhimu mnataka kuarifiwa. Baada ya tangazo hilo naahirisha kikao chetu hadi saa 11:00 za jioni.

(Saa 7:00 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano bado yanaendelea, nina wachangiaji wawili wa mwisho ambao kwa bahati mbaya sana siwaoni hapa ambao ni Mhe. Fatma Mbarouk Said na Mhe. Mohammed Haji Khalid. Waheshimiwa kwa hivyo kwa maana hiyo kama kuna mtu yeyote ambaye anataka kuanza kuchangia achangie hadi hapo waliojiandikisha wakija wataendelea.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kupata fursa ya kuweza kuuchangia mswada huu kama ambavyo wenzangu walitangulia wakati wa asubuhi na kuweza kuchangia mawili matatu katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli mswada huu jana tulifaidika tukaweza kupata semina yake na kwa namna fulani wajumbe wameuelewa vizuri sana mswada na ndio maana hata siku ya leo ukaona kwamba wajumbe wamekuwa wazito kidogo katika kuchangia mswada huu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ni fursa nzuri sana kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza letu hili Tukufu la Wawakilishi la Zanzibar lakini pia kwa ndugu zangu ambao wanakwenda sambamba na kushughulika na sekta binafsi juu ya masuala yao ya kujiendeleza katika kutafuta mustakbali mzuri wa kujiendesha kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina *argument* ya aina yoyote katika mswada huu kama ambavyo katika Semina jana tulivyokuwa tumechangia pale sisi tunasema kwamba mswada huu ni mzuri na tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kukaa na mwisho kabisa wakaamua kutuletea mswada huu kwa lengo la kuweza kuoanisha sasa, baina ya watu ambao wanashughulika na sekta binafsi vile vile na Serikali kuweza kufanya kazi kwa pamoja kwa malengo ya kuweza kuisaidia zaidi na kuinyanyua sekta hii binafsi ili iweze kwenda vizuri kama ambavyo nchi za wenzetu wanakwenda na sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi tatizo langu ni moja tu, katika kile kifungu cha 14 pale, kile kifungu cha 14 Mhe. Mwenyekiti, bado mimi naendelea kusisitiza Mhe. Waziri atakapokuja hapa aangalie uwezekano wa kuweza kufikiria zaidi ni namna gani ya kuweza kuihusisha sekta binafsi katika kutengeneza ule uwiano na ukaribu zaidi wa kufanya shughuli zetu zile kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali tunayokwenda nayo kwa sasa tunayo mifano hai mifano ambayo inawapa fursa watu binafsi kuweza kuchukua madaraka makubwa na kuweza kuchangia maendeleo ya nchi yao pasina kutokezea matatizo ya namna yoyote.

Sasa na mimi kwa vile nimetokea katika sekta binafsi naona itakuwa ni jambo la fahari sana kwamba hapa leo nasimama na kuweza kutetea kwamba wale wajumbe ambao watakuwa wanatoka katika sekta binafsi waweze kuwa wajumbe katika kamati zote ambazo zitakuwa zinaundwa ili kuweza kuleta ufanisi zaidi. Kwa yale ambayo yatakuwa yana matatizo na kiserikali yale aa sitaki kuyaingilia, ninaheshimu sana taratibu hizo na naomba ziendelee. Lakini kila ambapo panahisika wanaweza watu wa sekta binafsi wakashiriki na wao ni kuwa ni miongoni mwa wajumbe basi ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie na atuonelee huruma na atusaidie, ili tuweze kuona kwamba sekta binafsi zinashiriki katika kamati zote ambazo zitakazokuwa zinaundwa kwa lengo la kufikia yale malengo ambayo yalikuwa yamewekwa juu ya kuziimarisha na kuzinyanyua sekta binafsi ili ziweze kuendelea vizuri na nchi ziweze kuwa na uchumi ambao utakuwa wa kuendelea zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, si siri kwamba sekta binafsi ndipo hasa kwenye uwezo mzuri wa kifedha, tutakapoweza kuja kuwashirikisha katika mambo ya msingi kama haya sekta binafsi inaweza kuchukua nafasi yake na uchumi wa nchi ukaweza kugeuka ghafla moja na kuweza kupata maendeleo makubwa zaidi, lakini katika misingi ya kuzingatia taratibu, sheria na kanuni tunazojiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelekezo haya sasa kwa sababu nimesema mswada huu mimi sina mengi sana ya kuweza kuchangia lakini ninachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na kamati yake na makatibu wake na watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na hatimaye sasa baada ya kazi kubwa iliyofanywa katika kamati inayosimamia viongozi wakuu wa Serikali, kamati ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wa Wenyeviti, Mhe. Hamza Hassan Juma kwisha kufanya marekebisho makubwa kwenye mswada huu. Nasema mswada huu kwa sasa uko safi na kwa niaba yangu na wajumbe wenzangu waliokuwemo humu nawaomba tuukubali mswada huu na tuupigie kura za ndio kwa asilimia mia kwa mia.

Baada ya maelekezo hayo nasema ahsanteni sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa jioni hii na mimi kupata fursa ya kusema maneno mawili matatu katika mswada huu ulioko mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa jioni hii kuendeleza shughuli zetu za kazi zetu za kazi zetu za kawaida.

Aidha, nitoe pongezi maalum kwa Mhe. Waziri na uongozi wake wote kwa kutayarisha mswada huu na leo hii ukawepo penye meza. Mhe. Mwenyekiti, katika uzoefu wangu kwa muda mchache Barazani miswada ya Mhe. Mwinyihaji Makame mara nyingi huwa inakwenda na kurudi.

Kipindi cha miaka 2 na nusu ya mwanzo iliyopita uliletwa mswada mimi nikiwa ni mjumbe wa Kamati ya Viongozi wa Kitaifa na mswada huu tuliujadili katika kamati tukausimamisha, ukaja tena ukasimamishwa. Kwa kweli miswada yake mara nyingi huwa inakwenda aina hiyo. Sina hakika inapotayarishwa huwa kuna kitu gani ambacho kinafanya mishwada yake iwe inakwenda na kurudi, kwenda na kurudi kama mwendo wa *amoeba*.

Mhe. Mwenyekiti, na huu vile vile umekwenda na kurudi mpaka umefika pahala baadhi ya vifungu wamefika pahala kukubaliana kutokubaliana na kamati yake. Hiki ni kiswahili cha kisasa kukubaliana kutokubaliana lakini kwa ufupi ni kuwa watu walivyosema hivyo kulikuwa hakukubaliana ni maneno tu ya kujizungusha kwa sababu tumekubaliana kutokubaliana *that means* watu hao wawili walipokuwa wakijadili itakuwa hawakukubaliana hiyo ni lugha ya kwenda hapa na pale.

Kwa kweli wamefika pahala niseme kuwa kuna baadhi ya vifungu kamati na serikali wamefika hivyo wanavyotaka wao kukubaliana kutokubaliana lakini niseme wamefika pahala ambapo hawakukubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na hili jaduweli la miradi ya mashirikiano baina ya sekta za umma na sekta binafsi. Hapa ipo miradi kadhaa karibu 20 iliyowekwa hapa kama pengine ni mfano wa miradi ambayo inaweza ikatekelezwa kwa ushirikiano baina ya sekta za umma na sekta binafsi. Mhe. Mwenyekiti, nianze baadhi yao kujaribu kutoa maelezo yangu kulingana na vile ninavyohisi mimi. Tujalie huu wa tatu uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa aina zote za nishati.

Mhe. Mwenyekiti, umeme ni moja katika sehemu ya nishati, nchi yetu pamoja na yote lakini bado tunalo tatizo kubwa la umeme. Umeme tulionao wa ZECO kulingana na maisha ya watu wetu bei yake ni kubwa kidogo kwa hivyo kama itatokea Kampuni au muekezaji anayeweza kuwekeza katika suala la umeme kwa gharama nafuu kuliko hii iliyoko basi ni vyema akawa-*invited* akapewa masharti ya Zanzibar na akawekeza. Lakini kama muekezaji yoyote kwa suala la nishati ya umeme ikawa umeme atakaozalisha hatimaye utakuwa na bei zaidi wa ule wa ZECO huyo itakuwa hatufai. Kwa sababu lengo ni kupunguza gharama za mtumiaji yaani mlipa kodi ikiwa hii ya ZECO anahisi kuwa ni kubwa halafu tukamleta muekezaji ambaye atazalisha umeme lakini kwa gharama kubwa zaidi umeme huu utakuwa bado hauna manufaa kwa Wazanzibari.

Kwa hivyo ni vyema wakati ambapo wahusika watakaposajili wafanye mahojiano ya kutosha na muekezaji ili tuone gharama za uendeshaji wa mradi wake utakavyoweza kuisaidia Zanzibar na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, jengine miradi ya ujenzi wa nyumba makaazi ya umma na makaazi ya kijamii, kadhalika kama kutakuwa na muekezaji ambaye ataingia Zanzibar anataka kujenga nyumba za kuishi watu wizara husika ikampatia ardhi na nyumba atakazojenga zikawa zina kodi nafuu au akaziuza kwa bei nafuu muekezaji huyo tumkaribisheni. Kwa sababu Zanzibar tuna tatizo kubwa la makaazi watu tumeongezeka kwa kima kikubwa sana, uzazi umekuwa mwingi mno kwa hivyo watu tunaongezeka kwa kasi na kila anayezaliwa hatimaye iko siku atahitaji makaazi. Mimi Mhe. Mwenyekiti, tulizaliwa watano katika ukoo wangu lakini mimi binafsi peke yangu tayari nimezaa kumi na mbili mke mmoja tu.

Sasa sisi tulikuwa watano, mimi peke yangu ninao 12, kuna dada yangu anao zaidi ya hao, kuna na mwengine anao zaidi ya hao. Katika sisi watano kama tungelikuwa tumekaa pamoja tunatosha kufanya kijiji kikubwa sana pamoja na watoto wetu, hii inaonesha namna ambavyo tunaongezeka na kila mmoja anahitaji makaazi, maji safi, nyumba bora na kadhalika.

Kwa hivyo kama kutakuwa na Kampuni yoyote au muekezaji yoyote anayetaka kuekeza katika suala hili la ujenzi tumpokee alimradi tu nyumba zake atakazojenga ama kwa kuuza au kwa kupangisha bei yake iwe ni nafuu ili Wazanzibari waweze kumudu hizo gharama.

Mhe. Mwenyekiti, nyengine imo inayohusu masuala ya maji, Zanzibar pamoja na kuwa tunavichimba visima vingi kwa ajili ya kupata maji safi na salama bado tatizo la maji ni kubwa tena kubwa mno, kubwa tena kubwa sana, kubwa tena kubwa kabisa. Sasa kama atatokea muekezaji ambaye anataka kuwekeza katika shughuli za maji huyu naye kadhalika ni vyema akapokelewa akaelekezwa na akatusaidia katika kuweka miundombinu bora ya maji ili matatizo yaliyokuwa hivi sasa yapungue kwa kiasi kikubwa. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi zote ambazo Serikali inachukua kuhusu maji bado maji ni tatizo sugu mno.

Kuna vijiji au mitaa wanapata maji wiki mara moja, wengine kila baada ya siku kumi, wengine kila baada ya mwezi, wengine kina mimi hata hatujui maji yatatufika lini pamoja na kuwa tuna bomba za maji ndani. Kama ingelikuwa kama watu wengine wenye hasira pengine hata ile bomba yangu nyumbani mwangu ningeliing'oa, kwa sababu imekaa tu. Hii ina maana kuwa

tatizo la maji bado lipo katika sehemu yangu na sehemu za watu wengine nadhani liko hivyo hivyo.

Sasa kama tutakuwa na muekezaji Mhe. Mwenyekiti, ambaye atawezakusaidia upunguzaji wa matatizo haya katika miradi hii iliyotajwa hapa ni vyema huyo akapokelewa, akaelimishwa ili tuweze kwenda naye sambamba katika hii miradi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme jambo moja wawekezaji hawa binafsi wanapokuja lazima wanakabiliwa na chombo ambacho kimewekwa kuwasajili.

Hivi karibuni sisi hapa tulipitisha sheria ya rushwa, tulipitisha sheria ile Mhe. Mwenyekiti kwa sababu tumetunga sheria pengine ama ipo au harufu ya rushwa ipo katika taasisi zetu. Sasa tuna-*invite* wawekezaji tusije tukamsajili mtu kutoa huduma kwa kutegemea kupata rushwa ili aweze kusajiliwa. Sisemi kuwa watu wanafanya hivyo lakini kwa sababu sheria ipo na sheria imewekwa kwa sababu haya masuala yapo baadhi ya wakati wananchi wananunua haki zao, kununua haki ni kwa jambo ambalo ni wajibu upate lakini kama hukukunjua mkono haki hiyo huipati. Mhe. Mwenyekiti, Kiswahili kuna misemo ya aina mbili, "ukitaka cha mvunguni sharti uiname" lakini mivungu ya sasa ukiinama utakwama.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuwa "mkono mtupu haurambwa" mambo yote haya, misemo yote hii ni misemo inayoashiria utoaji wa kitu ili upate haki yako. Kutoa chochote kwa mkono mtupu haurambwa ni kwamba mtu umpe chochote ili akupe hiyo haki yako. Si msaada ni haki yako sharti unataka la mvunguni lazima uiname ni kwamba utoe chochote upate hicho unachotaka.

Mhe. Mwenyekiti, misemo hii yote ni misemo ya Kiswahili kwa wakati wake inayoashiria kuwa lazima kama unataka kitu kwa mtu na wewe utoe kitu. Kutoa kitu kwa sababu unataka kitu, hii ni aina ya rushwa kama kitu kile ni haki yako kupata bila ya kulipia chochote.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hii ni miradi ambayo wawekezaji wanakuja kama tutakuwa na masharti yetu mbali ya yale masharti ya kawaida ikawa lazima wainame, lazima mkono mtupu haurambwa hawa wawekezaji watatutoroka na hatimae tutabakia kama tulivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kulingana na hali yetu ilivyo wenzetu mawaziri, nafikiri wengi mmeshakwenda nchi nyingi mbali mbali na nyengine ambazo sisi tumepata uhuru mwanzo, lakini wao wameendelea zaidi kuliko sisi kwa nini waendelee zaidi? Pengine mipango yao waliojipangia katika kutekeleza maendeleo ya nchi zao ni mizuri zaidi kuliko ya kwetu. Hapa mwalimu alikuwa ni Mwenyekiti wa nchi tano za ukombozi; zile nchi ambazo mwalimu kazisimamia kwamba zijikombowe nyengine zimetupita sisi Zanzibar kwa maendeleo, kwa nini? Kulingana na mipango yetu isiyokuwa mizuri katika kuwahudumia watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa leo tumefika pahala kuona kwamba serikali inahitaji kushirikiana na wengine kuleta miradi ambayo itasaidia serikali kutoa huduma bora kwa wananchi wake, ni vyema tukaondoa dosari, kasoro na tofauti tukawa wakweli katika masuala haya. Vyenginevyo tutakuwa tunapepea mwiku (uporo), kukila kitu ambacho kimeshapoa unakifanya kwamba kioze. Kwa hivyo, ili wawekezaji wetu au wawekezaji ambao wana nia ya kuja kuwekeza Zanzibar, tuondoe kasoro zetu ili wavutike, wahamasike, washawishike na wakubaliane na sera zetu za nchini katika kuekeza shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, nigusie kidogo katika kifungu cha 46 ambacho katika ukurasa wa 371, samahani Mhe. Mwenyekiti. Kifungu hiki cha 46 kinasema hivi: “Makubaliano yatakayofikiwa baina ya Wizara ya Fedha kwa niaba ya serikali na mwekezaji binafsi kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 17 cha sheria hii”. Sasa hicho kifungu cha 17 mheshimiwa ndio ambacho kiko katika ukurasa wa 362, kifungu cha 3 ambacho kinasema hivi:

“Kwa madhumuni ya makubaliano na utekelezaji wa miradi, mzabuni atakayeteuliwa kwa mujibu wa sheria hii, ataanzisha taasisi ya biashara katika mfumo wa ubia au kampuni yenye mtaji wa ukomo utakaosajiliwa kwa sheria za Zanzibar kabla ya kurasimisha makubaliano hayo”.

Mhe. Mwenyekiti, hii naikubali kwamba lazima mwekezaji yeyote asajiliwe kulingana na sheria za Zanzibar. Tusimsajili au asije na usajili wake ikawa kasajiliwa nje ya nchi nyengine akaja kufanya kazi Zanzibar ikawa sisi hatuna pakumkamata.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata akasajiliwa Zanzibar tujaalie mwekezaji huyo kenda kinyume na taratibu za usajili wake. Je, kuna adhabu yoyote ambayo ipo ya kisheria tunaweza kumchukulia pale ambapo tumemsajili kwa masharti tuliyokubaliana na hatimae akavunja hayo masharti au hayo makubaliano wenyewe. Je, tunayo adhabu yoyote dhidi ya mwekezaji wa aina hiyo?

Mhe. Mwenyekiti, nirudi nyuma katika kifungu cha 9 ambacho kiko ukurasa wa 359.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki cha 9 kinazungumzia maneno yake ya pembeni kinazungumzia kuanzisha kwa Idara ya Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, niliposoma kifungu hiki nimeona kuwa hii idara imemtaja mmoja tu, yaani ni Mwenyekiti ambaye ndiye atateuliwa na Rais kwa sifa ambazo zimetajwa. Lakini sikuona kuwa idara hii ina wajumbe, wajumbe wake wameonekana kuwa wamo ndani ya Tume ya Mipango, lakini hawakuteuliwa kuonekana kwamba hawa ndio wajumbe wa idara hii. Kwa hivyo, idara hii kimsingi ina mwenyekiti tu, kama si hivyo ningependa nipate maelekezo ili nifahamu na mimi hawa wajumbe wa hii idara watatokea wapi. Ingawaje nilijua kuwa wamo ndani ya Tume ya Mipango, lakini kwa kuwa ni idara ingeainishwa kuwa wajumbe wake ni hawa na wenye sifa hizi kama ilivyowekwa sifa za mwenyekiti wa hii Tume.

Mhe. Mwenyekiti, nisogee mbele kidogo ukurasa wa mbele wa 360, kifungu cha 13 kazi za kamati ya wataalamu. Hapa zimetajwa nyingi na takriban zote nazikubali na nazipongeza. Lakini kifungu cha 14 ambacho kipo ukurasa huo huo kimezungumzia muundo wa Kamati ya Wataalamu. Kamati ya Wataalamu ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi itaundwa na wajumbe wafuatao:

(i) Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Zanzibar ambaye atakuwa Mwenyekiti, twende kwa mtiririko mpaka wa mwisho kwenye (g) katajwa Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wote hawa waliotajwa wanatoka katika taasisi zetu za serikali, sheria hii au mswada huu tunaoujadili ni wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Sasa mtu ambaye tunataka tushirikiane nae, tunaunda Kamati ya Wataalamu yeye tunamtoa nje hayo mashirikiano yako wapi? Hapa bado serikali haijakuwa tayari kufanya mashirikiano na hizi taasisi za watu binafsi kwa sababu tunaunda kamati ambayo ndio kubwa katika mambo yote, lakini mwenzetu ambaye tunashirikiana nae tunamuweka pembeni.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba serikali isiwe kachu, sijui kama hilo neno mnalijua maana yake ni baadhi ya mwahala ikubaliane na maoni ya kamati inayohusika, ikubali na mawazo ya Waheshimiwa Wawakilishi wanaochangia kwa sababu kama wao wakishikilia vile vile ilivyokuja tu itakuwa chombo hiki kinakuja kupitisha vile serikali ilivyoona iwe tu.

Serikali inaleta, inafanya marekebisho, kuna mambo wao hawayataki lakini baada ya michangio tunaelekezana wanaridhia, lakini kama kila kitu wanashikilia vile ambavyo wao wameona, hapa itakuwa kwa kima fulani, serikali haitaki kupinga katika vile ilivyoona na itakuwa hawataki mawazo ya ziada kutoka kwa Waheshimiwa Wawakilishi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti ningeomba mimi kwa kuwa ni suala linalohusu sekta za umma na zile binafsi, na hawa binafsi na wao katika kamati hii waingizwe, kwa sababu mswada wote unajadili masuala hayo hapa hakuna kwamba kuna siri ya serikali au siri gani, mswada huu unahusu mashirikiano baina ya sekta za umma na zile za binafsi. Kwa hivyo, kwa nini wao wasiwemo?

Mhe. Mwenyekiti, tujaalie kuna mtoto wa kike au wa kiume zimekuja posa, mtoto ana pande mbili kwa baba na mama, lakini tunapokaa kumjadili mume tujaalie mtoto wa kike kaja kutakiwa na mtu tutakapokaa kumjadili mume yukoje upande mmoja wananiambia ah! nyinyi mama kumjadili huyu mume kwanza tokeni. Lakini mtoto ni wa pamoja lakini kwenye kujadili tabia za mume upande mmoja tunautoa nje, sijui huyu anayetolewa atajihisi vipi akijihisi na yeye ana haki sawa na wewe katika suala lile, na kinyume chake.

Pengine mtoto wetu wa kiume anataka kuoa tunataka kuchunguza tabia za msichana anayemtaka lakini upande mmoja aah, hizi habari za kumchunguza mtoto wa kike tuacheni sisi tu, nyinyi kaeni nje. Kwa hiyo, upande ambao unaambiwa ukae nje utajihisi vipi katika suala la pamoja *similarly* na mswada huu au na sheria hii na kamati hii kwamba wale ambao tunataka tushirikiane nao kuna kamati kubwa ambayo ya kitaalamu lakini wao tunawataka wasiwe wajumbe. Maana yake nini? Je, ni kweli tuko tayari kushirikiana na sekta binafsi au tunaileta tu kwa kuwa duniani ipo na sisi tuwe nayo, kwa kuwa watu wanafanya na sisi tufanye, kwa kuwa wenzetu wamefanya na sisi ndio hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, ili sheria hii nzuri na iwavutie hao tunaotaka kuwa wawekeze ndani ya nchi yetu, tusijaribu kwa njia yoyote ile kuwafanya kuwa wao yako masuala kwa sheria hii masuala hayo iwe wao hayawahusu, kwa nini yasiwahusu na ndio tumefanya tuwe na mashirikiano nao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi huu mswada kwangu ni mgumu sana sikuupitia na kwa kweli kwa kuwa sijaupitia vyema kuna jambo jengine dogo tu nimalizie.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kule mwanzo kuwa nchi yetu inahitaji tufanye juhudi zozote zile za kukwamuka hapa tulipokwama. Kuna nchi ambazo sisi tulizisaidia zikomboke leo wao wako mbele katika maendeleo kuliko sisi tuliowasaidia. Kama ingelikuwa ni mtoto kusomeshwa na mzee wake mtoto akawa bora ni *well-done* lakini nchi kusema nchi nyengine imo katika ukoloni tukasaidia ikafanikiwa na hatimae sisi tuliosaidia ikawa tuko mkiani, tujione kwa nini tuwe nyuma na hawa wote tumewasaidia na sisi nguvu zetu mpaka wakafika hapo.

Mhe. Mwenyekiti, nyinyi mnaotembea mara nyingi mnatusifia Rwanda na Burundi jinsi walivyofanikiwa katika mambo mbali mbali; nchi ambazo zimepata uhuru karibuni kuliko sisi. Lakini sisi tunasimama hapa kuwasifu kwa jinsi walivyoendelea, hatujitazami kwa nini wakatupita. Wao wana nini na sisi tuna nini, wao wanafanya vipi na sisi tunafanya nini, tusisifu tu. Tutazameni kwa nini watu tuliowasaidia wakawa ni *far better* (wako mbele sana) hata kama wata-*mark time* moja mbili hapo hapo bila ya kwenda sisi hatuwafiki, kwa nini na sisi hatujaapizwa.

Ni kwamba bado yale mambo manne aliyoyasema mwalimu katika Azimio la Arusha bado hatunayo. Mwalimu alisema ili tuendelee tunahitaji mambo manne watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Watu tunao, ardhi ndogo tukitenda vizuri tunayo, tumekosa mambo mawili ya mwisho siasa safi na uongozi bora. Tukitengeza katika siasa safi na uongozi Mhe. Mwenyekiti, tutakwamuka hapa tulipokwama. Inawezekana tutimize wajibu wetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohammed Haji Khalid, uwanja ulikuwa wako leo, nakushukuru kwa mchango wako.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kufuatia neema zake hizi za uhai na uzima ili tuweze kujadili mambo yanayotuhusu katika maisha haya ya dunia. Pia, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutia baraka zangu katika Mswada huu ambao ni muhimu na wenye maslahi kwa wananchi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ni masikini na tunakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo hii miundombinu ambayo huwa tunaihitajia sana kwa ajili ya wananchi wetu. Sasa hatuwezi kuepuka hata siku moja kuwa na ushirikiano na makubaliano na sekta binafsi, ili angalau waweze kuzibaziba mule ambamo Serikali inaendelea kushindwa kumuhudumia. Lakini pia, niipongeze Serikali kwa kuona kwamba sheria ile ambayo ilikuwa inatuongoza katika mambo haya ya ushirikiano ilikuwa ina mapungufu mengi.

Kwa sababu ya mapungufu hayo kulikuwa kunatokezea matatizo ya hapa na pale ambayo mara nyengine yanapelekea Serikali kupata hasara kubwa. Ukisoma madhumuni na sababu ya Mswada huu utaona kuna mambo mengi ambayo Serikali wameyazingatia yakiwemo Kamati ya wataalamu ambayo ni Kamati muhimu sana katika kutathmini miradi. Pia, kuna utaratibu bora wa uidhinishaji wa miradi na uimarishaji wa uwezo wa Serikali kwa kutathmini miradi ndiyo Kamati ya kitaalamu hiyo.

Vile vile, Mswada huu unakusudia kuweka mazingira bora ya kisheria kwa wawekezaji binafsi, ikiwemo kuwadhibiti, lakini pia na kulinda haki zao. Kwa sababu ukifanya jambo kwa mujibu

wa sheria kuna haki na wajibu inaweza kupatikana katika sheria. Lakini pia, Mswada huu umezingatia kuwepo na uwazi zaidi katika kuingia mikataba hii, maana yake kabla tulikuwa tunatumia sheria ambayo mambo haya hayakuwa wazi sana, ukija unasikia tu kwamba hapo bwana kapewa fulani, lakini utaratibu uliotumika kumbe haukuwa rasmi, matokeo yake tunaambukia kwenye hasara.

Kwa hiyo, nasema Serikali imefanya jambo zuri sana kuleta huu Mswada ili masuala haya kuyapatia ufumbuzi mapema zaidi.Nataka nitoe angalizo tu kwamba, katika kuingia mikataba ikiwa hatukuwa makini sana, basi pamoja na kutengeneza sheria nzuri, lakini siku moja tunaweza tukaja tukaambukia tunaendelea kuitia nchi hii hasara. Kwa sababu kuna wawekezaji wengine wanakuwa wajanja na hawana nia njema.

Kwa hivyo, Kamati ile ya wataalamu hadi iweko makini sana wakati wa kufanya mikataba na wawekezaji binafsi ili ukiandaliwa mkataba basi uwe unajumuisha mambo yote ambayo hayawezi kutoa mwanya kwa mwekezaji kuweza kufanya ujanja na kuweza kujipatia manufaa mengi zaidi kuliko wananchi wanaokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo fupi, naomba sasa nianze kwenye vifungu, nataka nianze kwa kifungu cha 12 ambacho kiko kwenye ukurasa wa 360. Kifungu hiki kinaanzisha Kamati ya wataalamu na kifungu cha 13 kinaeleza kazi za wataalamu. Sasa tatizo nililoliona hapa kuna *duplication* ya maelezo, maana nilitarajia kifungu cha 12 kwa sababu kinaanzisha Kamati ya wataalamu, kifungu kiseme tu, tutakuwa na Kamati ya wataalamu, tumalizie hapo.

Sasa tukija kwenye kazi yale majukumu ya Kamati ya wataalamu yaelezwe pale kwenye kifungu cha 13 ambacho ndicho kinachoeleza kazi za wataalamu. Lakini sasa hiki kifungu cha 12 kimechanganya mambo yote, kinaanzisha Kamati ya wataalamu, lakini wakati huo huo kinaeleza na kazi za Kamati ya wataalamu. Ukija kifungu cha 13 kinaeleza tena kazi za Kamati ya wataalamu, sasa naona kama kuna *duplication* fulani.

Mimi nilikuwa napendekeza kifungu cha 12 kisomeke hivi; "Kunaanzishwa Kamati ya wataalamu ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi", basi. Yale maneno ambayo itakuwa na jukumu la kupitia upembuzi yakinifu wa miradi na mambo mengine, kwa sababu yamo katika kifungu cha 13 hapa yafutwe. Nafikiri Mhe. Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu watakuwa wame-*note* hilo jambo.

Halafu kifungu cha 14 pale kunakuwa na Muundo wa Kamati ya wataalamu na muundo wenyewe kunakuwa na katibu mtendaji, tume ya mipango Zanzibar ambaye atakuwa mwenyekiti. Lakini kuna mwakilishi atakaeteuliwa kutoka Wizara ya Fedha, huyu naye sina mjadala naye, kwa sababu bila shaka Wizara ya Fedha itatafuta mtaalamu kama ambavyo hiki kifungu kinadai wataalamu kimpeleke hapa. Pia, kunakuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu nae ni mtaalamu kwa mambo ya sheria lazima awepo, lakini sasa kuna kifungu (d), (e), (f) na (g), hawa mimi nina wasiwasi nao kidogo na mmoja ni (d) "Katibu mkuu anayehusika na ardhi".

(e) "Katibu Mkuu anayehusika na miundombinu", (f) "Katibu mkuu anayehusika na mazingira" na (g) "Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, hawa si wataalamu ila hawa ni watendaji katika taasisi zao. Sasa kwa sababu hii Kamati hii ni ya wataalamu, mimi nilizania wangekuwepo wataalamu ambao ni *professional* katika masuala haya, lakini hawa ni watendaji zaidi kuliko utaalamu na ndio maana katibu mkuu wa wizara fulani anaweza kubadilishwa akapelekwa wizara nyengine bila ya kuangalia ana *profession* gani.

Sasa Kamati hii itakuwa ina mapungufu ya wataalamu hasa waliokusudiwa, ila itakuwa na watendaji wengi, ingawa huko mbele kuna kifungu kinaruhusu kuwaalika au kuwaajiri kwa muda wataalamu kutoka nje ya hii Kamati, lakini sasa hii Kamati inaitwa ya wataalamu. Sasa mimi najenga wasiwasi kwamba hii ni Kamati labda tuseme ni *executive,* lakini haitakuwa Kamati ya wataalamu hasa.

Kwa hivyo, kuna haja ya kufanya marekebisho ili tuone wanaingia wataalamu ambao ni *professional* kwa ule utaalamu uliokusudiwa, kama ni *contractors*, masuala ya majenzi na mengineyo wawemo mle, lakini katibu mkuu ni mtendaji bwana.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye kifungu cha 17 kinasema; "Wajibu na Majukumu ya Mwekezaji Binafsi". Hapa kuna neno sitaki nilione humu kwa sababu halileti sura nzuri. Hiki kifungu kinasema; "Kuna mwekezaji binafsi ana haki zote kama zilivyoainishwa kwenye mkataba, ikijumuisha bila ya mipaka haki pekee ya kutumia huduma za umma". Sasa tatizo langu mimi ni hii "bila ya mipaka".

Nadhani haileti sura nzuri, kwa sababu hakuna utendaji usiokuwa na mipaka wala hakuna uhuru usiokuwa na mipaka, hili neno pia limetumika katika kifungu cha 16, lakini huku ni tofauti kidogo kwa sababu huku angalau hii taasisi ya mamlaka ya umma ndio ambayo inapewa bila ya mipaka. Pia, nayo ukiangalia si lugha nzuri sana, lakini kwa sababu taasisi ya umma unaweza kusema bila ya mipaka, lakini mwekezaji binafsi ukisema bila ya mipaka. Nafikiri unakuwa unampa uhuru mkubwa zaidi ambapo mara nyengine anaweza akautumia vibaya kwa maslahi yake binafsi.

Sasa pendekezo langu hili neno "bila ya mipaka" litolewe na ibakie sentensi itakayobakia hii "ikijumuisha haki ya kipekee ya kutumia huduma za umma", lakini lazima kuwe na mipaka na ukomo katika kutumia huduma za umma. Nafikiri Mhe. Waziri atakuwa amenifahamu hapo.

Kifungu cha 18 hii *marginal note* ina tatizo kidogo, kwa sababu inasema "Wajibu na Majukumu ya Watumiaji wa Huduma au Miundombinu ya Umma". Lakini ukisoma humu ndani kuna mambo mawili; mna wajibu na haki au haki na wajibu. Sasa nilikuwa napendekeza hii *marginal note* iainishe basi, yaani haki na wajibu badala ya kuwa wajibu na majukumu, nafikiri akiangalia vizuri Mhe. Waziri anaweza akakubaliana na mimi.

Nikiondoka hapo niende kifungu cha 21, lakini nianze kifungu cha 20 ambacho kinaanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Mradi. Kifungu cha 21 ni madhumuni ya huo Mfuko wenyewe sasa ulioanzishwa na kifungu cha 20. Sasa ukisoma ile *article (a)* inasema madhumuni ya Mfuko huo; (a) "Kugharimia gharama za kuendeleza mradi ikijumuisha upembuzi yakinifu wa awali na upembuzi yakinifu halisi wa mradi", halafu kuna (b), (c) na (d). Lakini ukisoma kifungu cha 22,

sasa majukumu ya kugharamia yanahama kule kwenye huo Mfuko anapewa Wizara ya Fedha, nilikuwa najiuliza, je, ni Mfuko au Wizara ya Fedha watakaohudumia.

Kwa sababu kifungu cha 22 kinasema; "Wizara ya Fedha itagharamia gharama zote za upembuzi wa awali na upembuzi yakinifu wa miradi kupitia vifungu vya bajeti vya mamlaka husika...".Lakini Mfuko kule ushabeba hiyo gharama na majukumu mengine, sasa tuwaachie nani, tuwaachie Wizara ya Fedha au tuuachie Mfuko? Nafikiri hapa Mhe. Waziri akija aje anipe ufafanuzi kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho si kubwa sana ni kwamba ndani ya kifungu cha 25 ukisoma kifungu kidogo cha (6) kinasema hivi; "Majibu yanayotolewa na Mamlaka ya Umma kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, yatatolewa kwa maandishi kwa Wazabuni wote waliopo". Sasa nakitafuta kifungu kidogo cha (4) sijakiona hakimo katika huu Mswada. Nafikiri kuna haja tufanye marekebisho na hicho kifungu cha (4) ambacho ni muhimu sana kwa kweli, basi kiainishwe hapa maana ukitoka cha (3) kuna cha (5) cha (4) hakipo, sasa kiwekwe ili kionekane na hiyo kazi ambayo imepewa kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chonga naomba nikubaliane na Mswada huu, hasa kwa umuhimu wake wa kuziba mianya ambayo mara nyengine Serikali inakuwa na ugumu kidogo wa kutekeleza na ni mambo ambayo yana maslahi kwa wananchi. Kwa hiyo, nakubaliana nao. Ahsante sana.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu kuhusu masuala ya uwekezaji. Kwa kweli mimi mchango wangu nachangia ukurasa wa 359, kifungu cha 9, kuhusu mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Huu ni ukombozi wa nchi yetu. Kwanza kuhusu afisa mwandamizi wa umma ni mtu yeyote mwenye uzoefu usiopungua miaka 15.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala haya mimi nachangia kwamba mtu huyo ambaye ana uzoefu zaidi ya miaka 15, muda huu kwanza upunguzwe ili kuhakikisha kwamba mtu ambaye anaweza kuendeleza suala hili, basi ni mtu ambaye anakwenda na wakati na umri wake unaofanana. Kwa hivyo, ni bora mtu mwenyewe nafasi hii aweze kuwa na uzoefu si zaidi ya miaka saba. Hii itasaidia kwamba mtu ambaye anahusika na suala hili ana umri wa kiasi na sio umri mkubwa kiasi ambacho miaka 15 ambapo ni umri mkubwa sana wa kuweza kukaa mtu nafasi hii ya kuweza kuendeleza suala hili.

Uhusiano wa sekta ya umma na sekta binafsi afisa mwandamizi ama mtu yeyote ambaye anahusika na kuendeleza suala hili ni yule ambaye anatoa mashirikiano makubwa sana na Serikali pamoja na sekta ya umma na sekta binafsi ndani ya Tume ya Mipango ya Zanzibar.

Kwanza itasaidia kiafya maendeleo ya uwekezaji kwa muda mrefu kuhakikisha mwekezaji ambaye amechukua nafasi hii anashirikiana vizuri na sekta binafsi ili kuhakikisha maendeleo ya nchi yetu yanakuwa kama yalivyopangwa. Kwa sababu mtu mwenye uzoefu anatakiwa awe mwanamke ama mwanamme, lakini tuhakikishe kwamba sekta hii inaongozwa na mtu mwenye uzoefu na uwezo wa kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika kifungu cha 10 kupitia mradi wa kushauri au kusimamia dhamana za kifedha zilizowekwa, hii ni kama ilivyopendekezwa kwa sababu watu waliopendekezwa ndio hao wanaofaa kuweza kuendeleza suala hili. Katibu Mkuu Mtendaji wa Tume ya Mipango Zanzibar ambaye atakuwa Mwenyekiti. Hii nafikiri mimi haina tatizo ni suala ambalo limekubalika na limekaa katika sehemu katika dhamana yake ambayo umepangwa.

Nikienda (b) "Mwakilishi atakaeteuliwa katika Wizara ya Fedha, Naibu Mwanasheria Mkuu". Kwa kweli kuhusu suala hili ni huyu ambaye anaefaa katika sehemu hii na ndiye anae uwezo wa kukaa na kuhakikisha kwamba suala hili linaweza kutekelezwa kutokana na dhama zake pamoja na kuhakikisha kwamba sekta zote mbili anaziunganisha; Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambazo zitakuwa na mashirikiano ya pamoja ili kuhakikisha maendeleo ya uwekezaji yanaendelea kwa haraka na kwa kasi kama yalivyopendekezwa.

Kipengele cha (c) "Naibu Mwanasheria Mkuu ndiye anayehusika" Na nikienda (d) "Katibu Mkuu anayehusika na ardhi" kwa sababu ardhi ndiyo inayotoa madini mengi ya kuweza kuhakikisha kwamba mikataba yote ambayo imekubaliwa ndiko inakotoka kuhakikisha kwamba ardhi ndiyo inayotoa madini ya kufanyia shughuli zao.

Kipengele cha (f) "Katibu Mkuu anayehusika na mazingira" Kwa kweli tuhakikishe kwamba mazingira yote yako salama kwa sababu mara nyingi sekta ambazo zinaweka au zinachukuwa dhamana ya kuhakikisha kutengeneza, lakini mwisho zinaharibu mazingira. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo kwa hakika watu hawa wote waliopangwa hapa ndio watu wanaohusika na ndio wenye dhamana ya uwekezaji katika nchi yetu na ndio watakaoleta maendeleo ya kasi kuhakikisha nchi yetu inapata maendeleo ya uwekezaji kama yalivyokubalika au kama yalivyopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa 360, kifungu namba 14 kinasema;

"Kamati ya Wataalam ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi itaundwa na wajumbe kama hawa waliopendekezwa pamoja na mashirikiano yao ili kuhakikisha kwamba sekta hii ina nguvu na inatoa maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar pamoja na kuhakikisha vijana wake wanapata maendeleo pamoja na ajira kama zilivyokubalika katika Sekta hii ya Umma na Sekta Binafsi ambayo itashirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba kupanga maendeleo yao ili kuhakikisha uchumi pamoja na maendeleo yanakwenda kwa kasi kama yalivyopangwa na sekta hizi mbili kwa mashirikiano ya pamoja".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu namba 16 kinasema; "Mamlaka ya Utekelezaji kwa niaba ya Serikali itakuwa na haki zote zilizoainishwa katika mkataba, ikiwemo mipaka ya usimamizi pamoja na mipaka ya utendaji". Sekta hizi zitakuwa chini ya Serikali na zitakuwa na uangalizi pale zinapokwenda kinyume na sheria ambazo zilizoomba, Serikali itabidi kuingilia kati kuhakikisha kwamba wanafatilia masuala yote ambayo waliyokubaliana katika mkataba kabla ya kuanza shughuli zenyewe za utendaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika kifungu cha 18 kinasema;

"Umma una haki ya kutumia miundombinu na huduma za Umma zinazotolewa na muwekezaji binafsi chini ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi katika misingi ya kutobagua kuwa na haki ya kupata huduma ambazo zilikubaliana na Serikali".

Mhe. Mwenyekiti, pande zote mbili zina haki sawa; haki hizi isiwe kwamba Sekta ya Umma ndiyo unayopewa nguvu zaidi kwamba Sekta ya Watu Binafsi imezoroteshwa kwamba haitopewa madaraka ya kuweza kama imeomba sehemu ya kuchimba dongo ama kuvuruga miti, hii haki itoke sawa sawa ili kuhakikisha kwamba watu wote hawa wanaleta maendeleo ya pamoja ili kuhakikisha nchi yetu ina haki ya kuweza kuhakikisha maendeleo mazuri yanapatikana, hasa katika maendeleo ya umeme ambayo hivi sasa ni lazima kwamba ikiwa sehemu itapata haki kama ni kukata miti, ni lazima sekta hii ipate nafasi ama ni kuchimba sekta hii ipate nafasi ili kuhakikisha inakuzisha maendeleo ya haraka katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, huo ni mchango wangu mdogo tu ambao nilioupanga kuhakikisha kwamba kutoa dhamana kwa sekta mbili hizi; Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ziende sambamba ili kuhakikisha maendeleo ya haraka yanapatikana kwa nchi yetu ili kuhakikisha awamu zinazofuata ni awamu zinazoleta maendeleo kwa nchi yetu.

Ahsante sana kwa mchango wangu. (*Makofi*)

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii jioni hii ikiwa ni mara ya pili, asubuhi nilichangia kidogo tu kutokana na hali ya kwamba nilikuwa sikujitayarisha na hata hivi sasa kidogo nina ghofu hata kuuchangia huu Mswada kwa sababu huu Mswada naona kidogo una ugumu wake na ni wa kitaalamu zaidi.

Lakini kwa ujumla kwamba huu Mswada na madhumuni yake ni mazuri kabisa kwa Serikali kuazisha sheria hii, kwa kweli kama walivyosema baadhi ya wenzangu kuwa ni mkombozi na ni jambo zuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia Mswada huu na ingawaje jana tulipata semina, lakini kwa kweli mimi nimekwazika kwa sababu jana katika mafunzo yale nilikuwa mguu ndani mguu nje sikukaa nikasikiliza kwa undani zaidi kwa sababu nilikuwa na majukumu mengine. Kwa hivyo, sikuendelea na semina ile.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa sababu ni jukumu langu kwa kupitisha sheria hizi na kufuta sheria zilizokuwa zimepitwa na muda. Kwa hivyo, na mimi nichukuwe fursa hii ili kuchangia machache.

Kwa kweli kama ilivyokuwa jana tulipokuwa tukiwasilishiwa na mtu wa Benki ya Dunia ambaye jana alituwasilishia ni kwamba kila mara alikuwa akizungumza kwamba akimithilisha kwamba ni sawa sawa na ndoa, kwa hivyo, na ndoa mnatakiwa muwe na ukweli na mapenzi ya ukweli na ya udhati na mnapokuwa mmefunga ndoa, basi mnakuwa kwa kweli hakuna siri ndani

yenu na mara nyingi watu wanaambiwa kwamba kuna msemo moja kwamba "Ukimuonea haya mke ndugu basi unakuwa huzai nae".

Kwa hivyo, nafikiria kwa Mswada huu ulikuwa hauna siri kwa sababu kuna kipengele ambacho wenzangu wameshakisema kuhusu kuanzishwa kwa Kamati ya Wataalamu.Hii wenzangu wengi waliochangia hapa walisema kwamba kuwachukuwa watu wa nje nao mkawatia kwenye Kamati hii kwa kweli kutatokea ule utokaji wa siri, yaani kutakuwa hakuna siri.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, yote mawili kwa sababu hakuna jambo lililokuwa lina faida likawa halina hasara. Lakini vile vile, mnapokuwa kwenye ndoa kwa kweli mnakula kiapo, anaemuendea mwenziwe kinyume anakuwa yeye na Mungu wake. Lakini kwa kweli sheria hii ni nzuri na ni katika kupunguza umasikini kama kweli tutaifatilia hasa na tutaitekeleza ipsavyo sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengi ambayo Serikali kwa upande wake inaona kwamba nitasema ni mzigo kwa mambo mengine kufanywa na Serikali na inarahisisha sana kutekeleza sheria hii ikawa kuna mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi. Lakini kama vile vile nilivyoona kwenye Mswada huu kwamba kuna sehemu inasema kwamba; "Kutakuwa na Mfuko wa Fedha ambao utakuwa umo katika sheria hii".

Lakini vile vile mfuko huu ambao ni wa maendeleo ya miradi ningeomba sana mfuko huu basi uwe unafanyiwa *Auditing* na vile vile kwa sababu ni fedha ambazo ni ruzuku kutoka Serikali na ambazo fedha ambazo tunaidhinisha sisi kama Wawakilishi wa wananchi. Kwa hivyo, ningependa sana kwamba fedha basi ziwe zinakaguliwa kwa sababu bila ya kuzikagua fedha hizi zinaweza zikatumia ndivyo sivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli niseme kwamba sheria hii iko kitaalamu na hasa pale tulipoona kwamba kuna *draft* hii inasema kwamba *Zanzibar Public Partnership Policy* ambacho ni kitabu kikubwa na kina lugha kidogo ya kigeni, lakini unapopitia pitia tu huku unakuta kuna mambo mengi ambayo yamo humu ikiwa ni moja ya ku-*introduce* hii *PPP,* mna *key element* ya *policy* hiyo na moja inasema "*Establishment of Institutional Framework of PPP Agender with the PPP Technical Committee consists of Seiner 0fficial to guide policy".*

Halafu vile vile, kuna *The PPP to Barclays within the Zanzibar Planning Commission Resource Centre of Expertise Invest Practical.* Kwa hivyo, haya yote ni mambo ya msingi ambayo wanasema ni kama ufunguo au ni kitu ambacho kina umuhimu. Lakini vile vile, kama nilivyosema kwamba hizi *documents* zote zimo katika lugha ambayo haieleweki.

Kwa hivyo, wengi wetu tunaaweza tukatafsiri neno moja moja lakini mengine yakatushinda na hasa hapa katika hiyo "*Key element of the policy"* ambayo imejumuisha kuna vifungu mbali mbali ameviainisha hapa lakini sasa kuna mambo yameandikwa kwa ufupi vile vile inakuwa ni tatizo kwetu sisi kujua maana yake.

Lakini nashukuru kwamba wataalamu wenyewe wako juu na nimepata kufahamu, kwa mfano kuna *MDA,* wakituandikia kwa ufupi kwamba *MBA* kama mtu ambaye si mtaalam inakushinda kuifafanua kwamba imekusudia nini na wengi niliwauliza humu ndani kwamba *MDA* maana yake ni nini, tulitafutana kwanza wengine.

Kwa hivyo, mambo kama haya hizi *introduction* na mambo mengine basi lazima na sisi angalau kuwe na ufupisho wa yale maneno yakawa wametafsiriwa. Kwa hivyo, imeipata kwamba ni *Ministry Department and Agency* ambayo ni mawizara maidara na taasisi.

Kwa hivyo, hapa nimeona namna ya hii *document* ambayo ukiisoma kwa undani zaidi, unapata moja moja na unaona kwamba ina mafanikio gani ambayo yamo humu na kwenye mafanikio lazima matatizo yanakuwepo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba sheria hii ina mambo mengi na mambo mengi ya kitaalamu. Lakini vile vile, kuna kifungu namba 50 nikienda kwenye hii sheria inasema;

> "Uendeshaji wa Miundombinu".

Kifungu (d) ambacho kina kifungu kidogo (a),(b), (c) na (d), kinasema;

> "Upatikanaji wa huduma bila ya ubaguzi wa miundombinu ya Umma inayoendeshwa na muwekezaji binafsi".

Hiki kitu ubaguzi kwa sababu tukianzisha taasisi hizi na kama tulivyozowea kwamba taasisi hizi wakati mwengine inakuja kitu kama ubaguzi labda wa mtu katoka wapi au katoka kwenye chama gani au katokea vipi. Hii madhali tumeamua kwamba tunakwenda na kitu hiki, basi kama tunapopiga vita rushwa basi na huu ubaguzi pia tuone kwamba si mzuri.

Lakini vile vile, kifungu namba 54 kinasema kuhusu dhamana.

> "Kwa mujibu ya masharti yaliomo katika makubaliano, Muwekezaji Binafsi ana haki ya kuweka dhamana mali yake yote inayohusiana na mradi kama inahitajika katika upatikanaji wa fedha inakavyohitajika kuendesha mradi".

Mhe. Mwenyekiti, dhamana ni jambo zuri na kwa sababu tunataka tufanikiwe na kwa sababu unapotaka kufanya biashara huwezi kufanya biashara ukawa huna kitu chochote cha dhamana. Kwa hivyo, hili ni jambo muhimu, lakini kuna jambo jengine. Kifungu cha 54(2), kinasema;

> "Wanahisa na muwekezaji binafsi wana haki ya kuweka dhamana hisa zao kwa muwekezaji binafsi".

Kwanza hii wana hisa wengi wetu tutakuwa hatutumii, tunataka Mhe. Waziri akija atufafanuliwe na hasa mimi mwenyewe ninayesema hivi pengine wenzangu watakuwa wanajua, lakini ndio hii wanahisa inakuwaje kuwaje hii hisa ya mtu, kwa sababu tunasikia tu kuna hisa hisa zinakuwa unajiunga kwenye kampuni, sijui unakuwa na hisa. Nilikuwa naomba kwamba hii Mhe.Waziri

akija kidogo anifahamishe kidogo kwamba ni nini hisa na natakiwa nifanye nini ili niwe mwana hisa wa kampuni.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu namba 55, kinahusu kubadilika kwa sheria, kinasema;

"Makubaliano wataweka utaratibu kwa muwekezaji binafsi kulipwa fidia kutokana na gharama za utekelezaji wa majukumu yake yanayotokana na makubaliano yaliyozidi kuongezeka au kushuka thamani wakati wa utekelezaji au kushuka kwa sababu ya mabadiliko ya sheria au Kanuni zinazohusu nyenzo za miundombinu au huduma zitakazo..."

(*Hapa kipaza sauti hakikusikika*)

Sasa hapa pia sijafahamu itakapobadilika sheria, kwa hivyo, utalipwa fidia na kama mulikuwa na ubia au mulikuwa pamoja, kwa nini sheria hiyo itakuwa inamlipa hiyo kulipa fidia kwa muekezaji binafsi. Hapa sielewi naomba vile vile Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anifahamishe zaidi ili nifahamu.

Vile vile, kifungu cha 57, kinahusu kwamba; "Uingiliaji kati ya Mamlaka ya utekelezaji". Kifungu hicho kinasema kwamba;

"Kwa mujibu wa mazingira yaliyowekwa katika makubaliano mamlaka ya utekelezaji ina haki kwa muda kuingilia kati uendeshaji wa huduma kwa madhumuni ya kuhakikisha ufanisi na uendeshwaji wa huduma wakati uvunjifu wa makubaliano kwa muekezaji binafsi kwa kutekeleza majukumu yake na kurekebisha uvunjifu uliotokea ndani ya kipindi muafaka baada ya kutoa taarifa ya kufanya hivyo na mamlaka ya utekelezaji".

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hii sheria ni nzuri na ina mambo mengi na muhimu kwetu sisi kama wananchi na Wawakilishi wa wananchi. Kwa hivyo, sitokuwa na mengi kwa sababu kama nilivyosema kwamba huu Mswada kwa kweli ni wa kitaalamu zaidi na unahitaji tuupitishe kwa nguvu zote, kwani mbali ya maoni ya ile Kamati na naomba kwamba tuupitishe.

Lakini yale machache ambayo nimeyasema kwa Mhe. Waziri, basi aniongoze ili niweze kufahamu zaidi atakapokuja hapa nitakuwa pamoja na yeye na naunga mkono hoja hii asilimia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Fatma Mbarouk Said, anayefuata ni Mhe. Panya Ali Abdalla, baadae atakuja Mhe. Subeit Khamis Faki na kwa bahati nimepata na wachangiaji wengine wawili ambaye atafuata Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na mchangiaji wa mwisho ni Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali.

Mhe. Panya Ali Panya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na ninashukuru na mimi kwa kunipatia fursa hii.

Kwanza kabisa na mimi nianze mchango wangu. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea Mswada huu ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano ya Nam. 1 ya 1999 na kutungwa sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha maridhiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji kwa kuleta suala hili kwa wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza nianze kwenye madhumuni na sababu ya kuletwa Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu madhmuni na sababu;

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeviweka vipa umbele katika kuendeleza miundombinu ya kitaifa kwa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kukuza uchumi endelevu na maendeleo". Kipa umbele hiki kitafikiwa kwa kuendeleza Sera ya Taifa, mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi na miongozo, kufutwa kwa sheria ya mradi ya maridhiano ya Nam.1 ya 1999, kutambua miradi yenye tija ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi na utoaji wa mafunzo kwa Idara ya Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi".

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye Mswada huu katika kifungu cha 9(3). Kwanza hapa kifungu kinaeleza "Mtu ili awe kateuliwa kuwa kamishna chini ya kifungu cha (2), kifungu hichi ni lazima awe na sifa zifuatazo.

Mhe. Mwenyekiti, imeandikwa Mzanzibari.Ninashauri ili "awe" iwepo "awe Mzanzibari". Halafu kwenye kifungu cha (c) pia "Awe Afisa Muandamizi wa umma au mtu yeyote mwenye angalau uzoefu wa miaka 15 ya uongozi wa sekta binafsi".

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nilikuwa na namshauri Mhe. Waziri, 15 ni muda mrefu kidogo. Nilikuwa naomba kama apunguze angalau iwe kama 10. Kwa sababu 10 nadhani kwa uzoefu mtu anaweza kuwa tayari ameshakuwa nao wa kutosha. Kwa hivyo, ushauri wangu hapa nilikuwa naomba apunguze kidogo angalau iwe ni 10.

Mhe. Mwenyekiti, nikija tena kwenye kifungu cha 14(1) ambacho kifungu hichi kinasema;

"Kamati ya Wataalamu ya Mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi itaundwa na wajumbe wafuatao".

Mhe. Mwenyekiti, wakaanza kutajwa wajumbe hawa kifungu cha (a) mpaka kifungu cha (g). Kwa hivyo, mimi kifungu hiki sina matatizo nacho kwa wajumbe hawa ambao wametajwa hapa na kwa sababu gani sina matatizo nacho, kwa sababu kuna kifungu cha (2) ambacho kinasema;

"Kamati ya Wataalamu inaweza kumualika muakilishi wa sekta ya umma ambaye ni mwenye mamlaka ya utekelezaji wa miradi iliyobuniwa kwa mfumo wa mashirikiano

baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, manunuzi au makubaliano ili wawe wajumbe wa muda wa kamati ya wataalamu".

Mhe. Mwenyekiti, ingelikuwa kifungu hiki hakipo, basi mimi ningeweza kukipinga hiki kifungu cha hawa wajumbe, lakini kwa kuwa kinatoa fursa ya wajumbe hawa una uwezo wa kuwaalika wataalamu wengine ambao ukaja ukakaa nao, basi ina maana hiki kifungu kinajitosheleza kwa sasa, hakina tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, na kama ilivyoelezwa katika kifungu hichi cha (e) na (f), kwa sababu kuna utunzaji hapa wa siri. Ni kweli hakuna hata mtu mmoja ambaye anafanya biashara akakubali siri ikatoka nje. Hata sisi wenyewe tu wafanyabiashara mtu mmoja mmoja huwezi ukaweza ukatoa siri ya biashara yako vipi unaifanya, lazima tuitunza siri hiyo, hata kama unapata faida vipi, pengine unaweza kusema mimi aah! sina hata faida yoyote ninayopata kwa sababu inakuwa ni siri yako wewe mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nikija kwenye kifungu cha 15(a) kinachoeleza;

"Uidhinishaji wa mikataba yote mikubwa inayohusu mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuwekwa saini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Wizara ikijumuisha uwidhinishaji wa upembuzi yakinifu kwa miradi mikubwa, nyaraka za zabuni, mikataba, mashirikiano ya kimkataba kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati ya Wataalamu".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki sina tatizo nacho lakini naweka angalizo kwa sababu mara nyingi matatizo yanajitokeza katika kufunga mikataba ikiwa feki au ikiwa haipo katika umadhubuti na hili jambo la hapa ni zito. Kwa hivyo, inahitaji tuwe makini katika ufungaji huu wa mikataba ili kuepusha migogoro ya baadae itakuja kujitokeza katika ufungaji huu wa mkataba ambao utakuwa haupo katika umadhubuti. Na utakua kuondoa dhana nzima iliyokusudiwa katika uanzishwaji wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, tunapofunga mikataba naomba hapo tuwe makini ili tuweze kuwa mikataba mizuri ambayo itaweza kulipeleka mbele jambo letu hili tunalokusudia kulifanya.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, ushauri wangu katika makampuni ambayo yatakuja kufanya ubia haya na Serikali, basi yawe ni makampuni yenye uwezo mkubwa na pia Serikali iwe imeyafanyia utafiti mzuri makampuni haya ili ijiridhishe, isije ikafunga mkataba na makampuni ambayo labda hayakutimiza zile sifa au viwango vizuri baadae yakaja yakaipa hasara Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pia, niseme mfumo huu kwetu ni mgeni, ndiyo mwanzo tunauleta. Tumeelezwa hapa kama mfumo huu wenzetu wameutumia kama nchi ya Kenya na Afrika Kusini na wameweza kupata mafanikio makubwa. Sasa kwa kuwa tayari sisi kwetu mfumo huu ni mgeni, basi mimi nilikuwa naishauri Serikali tuweke *pilot area* kwa Wizara kwa sababu tusije tukenda tu moja kwa moja, ili tuone utekelezaji wake utakuwaje na changamoto zake zitakuwaje.

Kwa sababu mwanzo unakuwa ni mgumu. Tukiweza kufanya hivyo basi tunaweza tukaziona zile changamoto zitakapojitokeza na sisi zikaja zikaturahisishia tukaweza kujipanga vyema katika mipango yetu mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa jambo hili litakuwa ni geni kwetu, nilikuwa nasisitiza upatikanaji wa elimu. Elimu kwa wananchi juu ya dhana nzima ya *PPP* kabla ya kuanza miradi ni muhimu sana kupatiwa wananchi wetu, ili miradi itakayoanzishwa katika maeneo husika ili na wananchi na wao waweze kutoa mashirikiano kwa kuona kwamba mradi huo kumbe ni wa kwao.

Mhe. Mwenyekiti, tutakapowashirikisha wananchi wakaweza kujuam hivyo tutakwenda nao sambamba na wataweza kuona kumbe kama mradi huu ni wa kwetu watauthamini na wataujali, hatimaye hayatojitokeza matatizo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka nichangie Mswada huu kwa kuona ubora wake, lakini sikuwa na mambo mengi. Kwa hivyo, nilikuwa tu ninataka niseme hayo machache, lakini nikubali kwamba naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana*. (Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla. Sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Subeit Khamis Faki baadae ni Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na mchangiaji wa mwisho ni Mhe. Mohamedraza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana jioni hii ya leo kunipa fursa na mimi kuchangia mawili matatu katika Mswada huu muhimu uliopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kwa maana hiyo Mswada huu tumeupitia sana kwenye Kamati, tumeeleza pa kueleza. Kwa hivyo, kiufupi mimi ni mjumbe wa hii Kamati na mengi maoni yetu yamesemwa katika ripoti yetu ya Kamati asubuhi wakati Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, alipowasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

Lakini hata hivyo itakuwa sikuutendea haki huu Mswada kama na mimi sitachangia maneno mawili matatu.

Mhe. Mwenyekiti, huu Mswada ni muhimu kweli kwetu sisi, ni muhimu kwa sababu umekuja wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ikiwa utatekelezwa vilivyo kama nchi za wenzetu wanavyoutekeleza, basi ni Mswada ambao unaweza ukatusaidia katika nchi yetu kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi yetu na pia kutoa ajira kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu wa mashirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi ni muhimu sana. Lakini mimi kidogo siku zote huwa na wasi wasi na wasi wasi wangu ni kwa ajili sisi tunakuwa tunatunga sheria nzuri, lakini utekelezaji wake unakuwa ukisuasua.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu suala hili la Mswada huu unaotuletea na nawaomba Wajumbe tuupitishe kwa nguvu zote, ili uweze kutusaidia. Lakini naiomba Serikali sana iwe makini na Mswada huu na iweze kutekeleza yale yaliomo kwenye sheria hii ili tuweze kupata mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Serikali naiomba kwanza hawa wawekezaji ambao ni watu wa *PPP* ambao kuwa tunategemea kuwa na mashirikiano na Serikali, basi kwanza Serikali ikubali kuwafungulia milango na iwafungulie milango kwa uhakika, iwape nafasi wawekezaji kwa kushirikiana na Serikali, lakini iwafungulie milango ya kuwapa nafasi kufanya kazi zao na Serikali iwe muadilifu kwa kufuatilia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kama kweli Serikali itawafungulia milango wawekezaji. Mimi naamini kama watakuja watu na watashirikiana na Serikali na tuna nafasi kubwa ya kufaidika katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu watu wanakuwa wanasuasua wawekezaji, kwa sababu wanaona kama labda Serikali inajaribu jaribu na ndiyo maana moja tulipotangaza maeneo huru, hadi leo hakuna muekezaji hata mmoja anayekuja kuwekeza katika maeneo huru, labda tajiri wetu huyu aliyekuepo hapa Said Bakheressa ameweka kule Fumba Kiwanda kile cha maziwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Serikali kwa sababu ikifungua milango, kuna watu kwa wenzetu wanawekeza kwenye viwanja vya ndege, Serikali inashirikiana na watu binafsi, sehemu za bandari. Kwa hivyo, naomba Serikali hata kwenye bahari ifungue milango kwa hawa wawekezaji washirikiane na Serikali na naamini kama ikiwa Serikali itawapa nafasi watu kweli, basi bahari inaweza ikatoa ajira kwa wananchi wetu kwa sehemu kubwa sana. Kwa hivyo, naomba sana Serikali iwawekee wazi wawekezaji washirikiane na Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia, naomba mwenzangu alisema kama kwenye mikataba yetu, lazima mikataba iangaliwe vizuri. Hao wawekezaji watakapokuja basi hiyo mikataba iwekwe mikataba vizuri, kwa sababu wananchi wetu wataingia kwenye ajira na wakiingia kwenye ajira lazima isimamie, ione kama mikataba ya wananchi inawekwa vilivyo, ili tuweze kupata faida na tuweze kupata manufaa.

Mhe. Mwenyekiti, huu Mswada ni mzuri kama nilivyozungumza. Huu Mswada unatupa moyo wa kuwa tunaweza hapa tulipo tukasogea mbele zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana na naiomba sana Serikali. Kwanza urasimu upungue, kusiwe na urasimu mwingi kwenye sheria hii. Wakati wanapokuja wawekezaji pasiwe na urasimu na tukiweka urasimu mkubwa watakimbia. Kwa sababu moja ya matatizo yetu ni urasimu, anapita mtu huku anakwenda huku na kule, urasimu usiwe mkubwa sana lakini kuwe na vitu ambavyo ni madhubuti vinavyoweza kulinda zile mali za Zanzibar ziweze kufaidisha Zanzibar pamoja na wageni wanaokuja wafaidike lakini na Zanzibar iweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nitakalozungumza kwenye kifungu kidogo hiki cha 14. Kifungu cha 14 katika Mswada huu kinazungumzia Kamati ya Wataalamu.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Makamu Mwenyekiti alipozungumza wa Kamati yetu, kama hiki kifungu tulikubaliana kutokubaliana, lakini naomba Serikali ikubali yale maombi yetu ya Kamati ikubali, kwa sababu kifungu hiki cha 14, kuhusu Kamati hii ya wataalamu, Mheshimiwa kwa ruhusa yako naomba nisome kifungu cha 14;

"Kamati ya wataalamu ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi itaundwa na wajumbe wafuatao".

Naomba niwasome hawa wajumbe muangalie;

(a) Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Zanzibar ambaye atakuwa ndiye Mwenyekiti;
(b) Mwakilishi atakayeteuliwa kutoka Wizara ya Fedha;
(c) Naibu Mwanasheria Mkuu;
(d) Katibu Mkuu anayehusika na ardhi;
(e) Katibu Mkuu anayehusika na Miundombinu;
(f) Katibu Mkuu anayehusika na Mazingira; na
(g) Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Kitega Uchumi Zanzibar;

Mhe. Mwenyekiti, haya ni mashirikiano baina ya taasisi za watu binafsi na Serikali yenyewe. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama ni mashirikiano kwa nini Kamati hii ya kitaalamu wawe ni watendaji watupu wa Serikali wasiwemo watu binafsi na wakati watu binafsi wapo wenye uwezo. Kama alivyosema yule mwezeshaji wetu jana wa semina kwamba kunakuwa na mambo ambayo yanakuwa ni muhimu ya Serikali, tuseme kwamba kunakuwa na Sera za Serikali zisije zikatoka. Akatoa mfano kama ikiwa kutakuwa na mambo ambayo yatakuwa ni ya usalama wa Taifa au yatakuwa ni ya usalama wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kama ni mambo kama hayo basi hiyo taasisi itakayoundwa iwe ni ya Serikali peke yake isiwe ya mashirikiano, iwe ni ya Serikali peke yake wasishirikishwe watu binafsi, kwa sababu kama ni taasisi ambayo ni ya usalama wa Taifa hawawezi wakashirikishwa watu binafsi na iundwe kutokana na Serikali peke yake, lakini hizi ambazo zitakuwa ni taasisi zinazoundwa baina ya Serikali na watu binafsi, kuna haja Kamati hii ya wataalamu tuwaingize na wao watu binafsi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunapendekeza watu wawili watoke katika sekta binafsi kama tulivyopendekeza kwenye Kamati na hii itakuwa tumewatendea haki wale watu. Kama ni siri za Serikali, naamini kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge, watendaji wakuu wa Serikali wote wanalishwa yamini, wakishalishwa yamini hawatoi siri za Serikali na hawa wakishaingia kwa sababu watakuwa wamo katika Kamati hii ya wataalamu, watapigwa yamini wajumbe wote, wakishapigwa yamini watakuwa hawatoi siri ya utendaji wao wanaotenda.

Lakini ikiwa kuna siri za Serikali basi na kiundwe chombo cha Serikali peke yake, kama ni taasisi za usalama wa Taifa, kama ni taasisi ambazo kuna usalama wa nchi na wawe peke yao. Lakini hapa kwenye uwekezaji hakuna siri hapa, kwa sababu hapa siri yenyewe iliyokuwepo kwenye uwekezaji ni ipi, hakuna hapa, isipokuwa mimi namuomba sana Mhe. Waziri, akubaliane na Kamati yake, watu wawili hawa watoke sekta binafsi, wala hapataharibika kitu na

hawa watapigwa yamini, kama viongozi wengine wanavyopigwa yamini na wao watakula yamini na naamini kwamba hawataharibu kitu chochote.

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ni mzuri, Mswada huu tunaupendekeza upite mia juu ya mia upitishwe ili tuweze kupata mabadiliko ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokuambia kama mimi nitakuwa na machache kwa sababu mengi tumeyazungumza kwenye Kamati, naomba sana Mhe. Waziri au naiomba sana Serikali itukubalie Serikali yetu ni sikivu isikie na wajumbe hawa wawili wateuliwe kutoka sekta binafsi ili na wao waone kama wamo, kwa sababu wao ndio watakaokuja kusema kama serikali imejikusanyia wenyewe, kwa sababu hawa waliopo ni watendaji watupu na watajiona kama bado ni vile vile kuwa Serikali inafanya mambo yake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na namuomba Mhe. Waziri, atukubalie.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kufika hapa wote salama na kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Mswada huu muhimu sana katika nchi yetu na ambao utaleta maendeleo makubwa na ufanisi katika nchi yetu.

Mhe. Waziri, nakushukuru sana kwa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Miradi ya Maridhiano namba 1 ya 1999, Kutunga Sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu ambao sio mkubwa sana, nianze katika ukurasa wa 354, Sehemu ya Kwanza. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuamua kuleta Mswada huu katika Baraza letu kutufu hili ili kuupitisha na Waheshimiwa Wajumbe, nawaomba sana tuuchangie na tuupitishe Mswada huu wa sheria, ambayo itajulikana kama Sheria ya Mashirikiano baina ya sekta binafsi na sekta ya umma 2015.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Sehemu ya Pili 3(1) katika Wizara ya Fedha kwa aniaba ya Serikali inaweza kuingia katika mashirikiano baina ya sekta binafsi na sekta ya umma. Kwa hivyo, kwa mujibu wa sheria hii kama nilivyosema mwanzo sheria ni nzuri na mimi nampongeza sana Mhe. Waziri, kwa kutuletea Mswada huu. Naomba nimuulize Mhe. Waziri anipe kidogo uelewa zaidi mimi na wananchi kwa pamoja.

Je, unafikiri ni maeneo yepi ya sekta binafsi yataweza kuingia mkataba na Serikali katika Mswada huu au katika maendeleo yetu ambayo tunaendelea nayo, unisaidie wapi sekta binafsi ikaingia mkataba na Serikali ikaweza kutusaidia katika maendeleo haya.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kifungu cha 4. Je, wawekezaji watakaojitokeza katika sekta ya umeme ambayo ni sekta mojawapo hutumia sana mfumo wa *PPP*, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anisaidie kwa hilo kama walivyoanza wenzetu wa Tanzania Bara. Je, wawekezaji wa sekta binafsi wataweza kuingia mikataba na mashirikiano kama *ZECO* au *ZAWA* kupitia sheria hii.

Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anisaidie kwa hilo kama itawezekana au mfano nimempa kwa miradi ambayo inaweza kuingia sekta binafsi kwa kupitia mradi wetu huu na mfumo wa *PPP* pia upo kama Tanzania Bara wenzetu wameshauanza na hivi sasa wanaendelea nao.

Lakini nije katika ukurasa wa 357, Sehemu ya Pili, kifungu cha 4(1), kuhusu mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, yanaweza kutekelezwa kwa njia ya mkataba. Lakini mamlaka ya umma ichaguwe na aina ya mkataba unaofaa utaainisha kwa uwazi, dhima na majukumu kila upande, yaani sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ni mzuri na umelenga mambo mazuri kabisa na mikataba mizuri ambayo itakayofungwa baina ya sekta binafsi na sekta ya umma. Nikianzia mfano kifungu namba 4(a), kinasema;

"Kusarifu, kujenga, kuharamia ukarabati wa uendeshaji wa mradi mpya wa miundombinu wa umma".

Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu kizuri mimi sina wasi wasi nacho na nampongeza Mhe. Waziri kwa kifungu hichi kukiweka, kwa sababu kimesema wazi hapa. Lakini kifungu 4(b) pia inasema;

"Kuimarisha, kuharamia, kupanua, kutunza na kuendesha miundombinu ya umma iliopo".

Kifungu hiki Mhe. Waziri, ni kizuri na kimeeleza katika mkataba kitakuwepo, kwa hivyo, mimi sina wasi wasi nacho, nampongeza sana Waziri kwa hili.

Kifungu (c) kinasema;

"Kuongoza, kusimamia, kuendesha, kukarabati au kutoa huduma za umma au kuweka miundombinu mipya".

Mhe. Mwenyekiti, pia, kifungu hiki kizuri sana kwa sababu kimeeleza sana wazi kabisa kusaidia katika miundombinu mbali mbali na kuweka kwa huyu mwekezaji binafsi ambaye atakayekuja kuweka miundombinu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri naomba kujua, katika miradi hii mtu anaweza kuingia katika mikataba hii awe na kiasi cha kima cha shilingi ngapi, maana yake Mswada nimeuangalia sijaona. Sasa muekezaji anapokuja na mikataba kama hii imesema awe na uwezo wa kufanya, kuimarisha, kupanua na kutunza kuendesha miundombinu ya umma iliopo.

Pia, kukarabati, kusimamia, kuendesha na kutoa huduma nyengine, lakini kima cha bei gani mwekezaji huyu anaweza kuingia katika mkataba huu. Anaweza muekezaji akaja, lakini akawa mbabaishaji. Sasa naomba kujua au aonyeshe kima gani au *capital* gani aliyokuwa nayo, yaani *evaluation* yake ya kuweza kuingia mkataba na Serikali kupewa kitu kuendesha yeye ili isije kuwa mikataba kama tunavyoona mifano mengine ya mikataba inakuwa wawekezaji ni wababaishaji.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Wazirim aniambie ni bei gani hasa kiasi cha fedha ambacho awe nacho muekezaji huyo anisaidi, ili tupate kufaidika mimi na wananchi wangu wote wapate kuelewa hawa wawekezaji watakuja na *capital* yao vipi na kuweza kuendesha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niingie kwenye kifungu namba 5(1), kuhusu mkataba wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema Mswada huu naukubali ni mzuri na una nia njema kabisa kwa wananchi wetu na hasa kwa Zanzibar yetu bila wasi wasi sina mashaka nao. Nichukuwe mfano hapa kifungu (a), kinasema;

"Kinasema maridhiano kwanza yawepo, mkataba wa umma unaotolewa kwa mujibu wa mkataba huo, muekezaji binafsi atalazimika kutoa huduma kwa umma au kuweka miundombinu ya umma kwa niaba ya mamlaka ya umma, awe tayari kuwajibika kifedha, kitaalamu, ujenzi au majukumu kwa mambo haya ambayo atakayoyafanya".

Kwa hivyo, mimi hapo nampongeza sana Mhe. Waziri, kwa mkataba huu ulivyouweka wazi kabisa huyo muekezaji awe na majukumu ya aina gani.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nimalizie mchango wangu kama nilivyosema sio mkubwa sana, nilitaka nichangie kwa sababu huu Mswada ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na mimi nampongeza Mhe. Waziri tena kwa juhudi yake kubwa hii.

Lakini Mhe. Waziri, nilikuwa naomba katika sheria hii utatusaidiaje katika sekta ya uchimbaji wa mafuta na gesi pale tutakapoanza kuchimba mafuta yetu Zanzibar. Naomba kama sheria hii uliposema mwanzo kuwa wawekezaji wataingia, lakini naomba itatusaidiaje au itatuweka vipi, naomba anipe muongozo wake ili tupate ufafanuzi zaidi tupate kuelewa kuwa hii kazi kubwa ambayo tunategemea karibuni kuifanya ya uchimbaji wa mafuta na gesi, kwani wananchi wetu wengi watapata ajira na kuweza kuondosha hali zao duni za kimaisha.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anisaidie sheria hii itatusaidiaje katika uchimbaji huu wa gesi na mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia kwa mia na wananchi wangu wa Jimbo la Bububu. Ahsante sana nashukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hussein Ibrahim. Sasa ni zamu ya Mhe. Mohammedraza Hassanali. Waheshimiwa Wajumbe, kama kuna mjumbe kwa sababu tuna muda bado, kama kuna mjumbe yeyote anataka kuchangia tuchangie ili tuweze kumpa nafasi Mhe. Waziri, kesho aje kufanya majumuisho. Mhe. Raza, karibu.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa hatuna budi wote kwa pamoja kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeweza kutupa pumzi hii tukawepo *Alhamdulillah* mpaka muda huu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nichukuwe nafasi ya kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini.

Lakini vile vile, Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kushukuru kwa kuletwa hii Sheria ya *Partnership*, mbele ya Baraza la Wawakilishi na matumaini yangu ni kwamba yataweza kufanikiwa na kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nikiwa mwakilishi, lakini vile vile kwa nafasi yangu ya pili ni mfanyabiashara. Sasa na kwa bahati nzuri hiki ndio chakula chetu, maana yake unaposema *partnership*.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu wa sheria kwenye ukurasa wa 353, Mswada huu ulikuwepo ambao leo unakuja hapa kufutwa sheria namba 1 ya mwaka 1999, takriban miaka 16. Nafikiri ingekuwa busara kwa Serikali yetu na waziri angeweza kutusaidia ni kitu gani kilichoweza kukwamisha Mswada huu usiweze kutekelezwa toka mwaka 1999, ambapo leo ni miaka 16 ambapo haukuweza kutekelezwa Mswada huu.

Mimi nafikiri Mhe. Waziri kwa kupitia hili Baraza tukufu la Wawakilishi angetupa ufafanuzi wa Mswada huu ambao ulikuja mwaka 1999 ukapitishwa, leo unakuja unafutwa. Sasa nafikiri Mhe. Waziri angetupa hoja nzuri na nina imani yake kwamba nini haukuweza kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu leo tumekuja na Sheria hiyo hiyo ya *Partnership* ya mradi huu wa pamoja. Kwanza ningeiomba Serikali kweli tumechelewa sana, lakini nasema hatujachelewa, wenzetu duniani kote wameweza kuendelea kutokana na hii *partnership,* ambapo waliofaidika hasa kwa upande mfano, Bangkok, Singapore, Malaysia, Indonesia na sehemu nyengine zinazohusika.

Mhe. Mwenyekiti, tunaposema tunaingia katika nyanja hii nataka nishauri wizara inayohusika na waziri anayehusika, kwamba ni lazima Serikali iwe ina mipango maalum wa kuweza kuwa na hii *partnership* na *commitment* ya Serikali, kupitia katika taasisi zinazohusika na kuweka sasa ni kitu gani ambacho Serikali yetu imepanga kuingia kwenye *partnership*. Unaposema *partnership*, Serikali lazima iwe ina *commitment,* yaani iwe imejiandaa na mipango yake.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana kwa Serikali na wafanyabiashara kuhusu *partnership.* Unaweza kuwa na miradi mingi ikawekwa ya barabara kwa mfano, miradi ya viwanda na miradi mengineyo, lakini kubwa zaidi ni kuwepo na nia, kwa sababu "penye nia pana njia".

Kwa hivyo, mimi naunga mkono, ndio maana nikasema najiuliza kwamba vitu hivi tulikuwa navyo kwa mwaka 1999, ni jumla miaka 16, leo inakuja kufutwa hii. Sasa tuwe waangalifu na dunia ya sasa tunahitajiana, dunia nzima unaposema *partnership*, wote tunahitajiana; wafanyabiashara wanahitaji Serikali na Serikali inawahitaji wafanyabiashara, maana ya *investment.* Kwa hivyo, sehemu zote mbili tunahitajiana kwa maslahi ya Taifa letu na kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kushauri Serikali ni kwamba mikataba hii ambayo tutakwenda nayo Mwenyezi Mungu atusaidie kwa nia nzuri, lazima tuwe waangalifu katika *partnership*.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi wafanyabiashara wanakuwa wajanja na kama hatutokuwa na wataalamu ndani ya Serikali, watalaama ambao wanauelewa uchumi tunaweza tukaja tukajikuta mfanyabiashara akaifilisi Serikali nzima na kukawa hakuna pesa ya kuweza kuzilipa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nina mifano mingi ya wazi, sasa katika hili kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kupitia kwa wataalam lazima tutafute wataalam ambao wenye fani ya uchumi hasa, maana unaweza kuwa na *Certificate,* inaweza ukawa *professar, doctor* matokeo yake ndio kwanza ule mkataba unaweza kuturejesha nyuma kwa miaka hamsini.
Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nime-*experience* mambo mengi sana katika maslahi yetu haya yaliyokuwepo na tunayokwenda nayo tumejikuta Serikali yetu hii hii imeingia katika hasara ya mabilioni na nina ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi tangu kuingia kwenye Baraza nashukuru mungu nazungumza na vigezo na ushahidi, si mropokaji, lakini tangu kumekuwepo kwa wataalam kama hivi Serikali yetu imeingia kwenye mikataba ambayo leo tunalipa mabilioni ya pesa; mikataba ambayo haikuwa na manufaa kwa nchi, mikataba ambayo haikuwa na manufaa kwa Serikali, lakini kwa sababu tu ya umimi umimi na kikundi tumefika hapa tulipofika.

Mhe. Mwenyekiti, uangalifu wangu mimi kwa wenzangu Serikalini, mimi nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa heshima zake, busara zake na usikivu wake, lakini kuna vitu ambavyo kama hatukuwa makini katika hii *partnership* namna gani ya kuweza kwenda kuifanyia kazi na kukaa, tuwe waangalifu sana tusije tukabebesha mzigo wajukuu zetu, vilembwa wetu huko mbele kwa sababu tu ya maslahi ya wachache.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina zaidi ya haya lakini natoa tu hiyo kwa sababu nimesema kwamba miradi mingi iliyokuwepo sasa hivi, ambayo imefanywa, imepitiwa mikataba na watendaji, miradi ile na watendaji wale matokeo yake leo kwenye sehemu ya bilioni 10 inabidi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dk. Ali Mohammed Shein inaongezwa nyengine bilioni 20 kutokana tu na mambo ambayo hayakuwa na ufanisi, hayakuwa na uwazi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hawakuhusishwa kuna mikataba ambayo natolea mfano, ambayo Mwanasheria Mkuu alipaswa azisimamie hazipiti na hizo zipo mpaka sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, ni vitu tofauti lakini ninachopenda mimi naelezea hali halisi kwamba tunapokwenda kama hivi tuwe waangalifu na tuwe na wataalam na tujue kwamba, bora tuwakodi wataalam ambao wenye kufahamika katika dunia ya sasa wakawepo wakatusaidia ili tuje kubeba mzigo ambao utakuja kutuumiza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja na kumi kuhusu suala la *partnership,* lakini naomba Mhe. Waziri kwa heshima zote awe muangalifu, lakini vile vile namuomba atutolee ufafanuzi tu wa huu mradi, sheria hii ya miaka 16 ilishindwa kuenda hata tukafikia hapa tunakwenda na huu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia. Ahsanteni sana.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe.Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa ya kuchangia mchango wangu mdogo sana ingawaje utakuja katika mchango wa kisuala kwa jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri anayehusika na Wizara hii kwa jinsi alivyowasilisha Mswada wake huu na tumeufahamu wote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema sina tatizo la kuunga mkono Mswada huu au sheria hii kwa sababu ni muda mrefu sana tulikuwa tunalipigia kelele suala hili la kutafuta wawekezaji, ili kuja kutufanyia kila lile lenye haja ya nchi yetu kwa kutafuta maslahi ya nchi na wananchi wetu kwa jumla. Sasa nimpongeze Mhe. Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuleta sheria hii ingawaje imechelewa lakini waswahili walisema "*kawia ufike*".

Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo tofauti ambayokuwa kuna kero nyingi katika maeneo yetu tuliyokuwa tunahitaji wawekezaji, kwa hivyo, imani yangu ni kuwa kupitishwa kwa sheria hii italeta mafanikio na Serikali italisimamia kwa umuhimu sana hili ili tufanikiwe na kuondosha kero zilizomo ndani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuja ukurasa wa 360, kifungu cha 13, kwenye Kazi za Kamati ya Wataalam, hapa kwenye Kazi za Kamati za wataalam kuanzia (a) mpaka (f), zote zinaelezwa kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, aidha kutaka mashauri au kushauri au kutafuta mapendekezo na mengineyo.

Sasa hapa nilitaka niulize suala, je, huyu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na yeye ni sehemu ya Kamati ya wataalam au laa? Nauliza hivyo kwa sababu inaonekana hapa mambo mengi yanakwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kwa kutafuta mafanikio ya hili suala lenyewe.

Lakini ukija kwenye kifungu cha 14 kwenye Muundo wa Kamati ya Wataalam na Mashirikiano, kuna watu hapa wametajwa; kuna Katibu mtendaji Tume ya Mipango ambaye atakuwa Mwenyekiti, kuna Muwakilishi atakayeteuliwa kutoka Wizara ya Fedha. lakini kwa bahati mbaya hakuainishwa kama ni Katibu Mkuu au laa. Kwa hivyo. namuomba hapa Mhe. Waziri, atupe ufafanuzi kutoka huyu muwakilishi atakayetoka Wizara ya Fedha, aidha atakuwa ni huyo Katibu Mkuu mwenyewe au kuna mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 15, kuhusu Wajibu na Majukumu ya Wizara ya Fedha, wajibu na majukumu ya Wizara ya Fedha ni makubwa katika Mswada huu na inaonekana yeye ndiye mhusika mkuu katika shughuli zote. Kwa hivyo, ninaloliomba katika Wizara hii ni kuwa makini sana katika utekelezaji na ufuatiliaji wa mikataba kwani nasema hivyo kwa sababu kuna mikataba mingi iliyofungwa hapa baada ya muda mfupi mikataba ile ikakiukwa, wengine wakakimbia kwenye mikataba ile, maana yake tunatoa mifano kwa yale mambo yaliyokuwa tunayo ndani ya nchi yetu tuliyoyaona.

Kuna miradi ya ujenzi wa barabara, kuna miradi ya ujenzi wa maskuli, kuna miradi mingi tu, lakini baadae wale wawekezaji wenyewe hukimbia halafu baada ya kukimbia wakaipa Serikali hasara kubwa ya kutafuta watu wengine wa kuja kulifuatilia.

Sasa nina wasi wasi na hapa kama hakutakuwa na usimamizi mzuri wa hii Wizara ya Fedha hapa katika wajibu wake, basi yatakuja kutukuta haya. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri na Serikali kwa jumla iliangalie sana suala hili katika kufunga mikataba ili tusije tukarudi nyuma baada ya sisi kwenda mbele kwa kufanikisha, tukarudi nyuma ikawa tupo pale pale tu pa zamani.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwambia katika barua yangu nina masuala mawili tu madogo, kwa hivyo, naunga mkono asilimia mia moja na nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhanahu wataala* kwa kutujaalia kuwa hai na wazima tukiendelea na shughuli zetu katika chombo hiki cha wananchi wa Zanzibar.

Pili, nikushukuru kwa kutoa nafasi kwa baadhi yetu ambao hatukuwahi hata kuleta majina kwa kutumia muda huu uliobakia kuweza na sisi kuchangia chochote, nikushukuru sana Mwenyekiti kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, tatu, nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame na Serikali kwa ujumla kwa kuja na Mswada huu. Napongeza kwa sababu mbili; Kwanza dhana yenyewe ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta ya binafsi kwa maana ya *Public Private Partnership* katika dunia ya leo na kwa miaka mingi sasa imekuwa ndio njia ambayo inatumiwa kuendesha miradi mikubwa, ile dhana ya kuona Serikali peke yake ndio inaweza kufanya miradi mikubwa kama hii katika sehemu nyingi sana duniani imeondoka.

Na mara nyingi miradi mikubwa duniani inategemea kupatikana kwa mtaji mkubwa sana na kwa nchi masikini kama zetu mara nyingi inakuwa si rahisi kwa Serikali peke yake kuweza kushajihisha upatikanaji wa mtaji wa kutosha kufanikisha utekelezaji wa miradi kama hiyo.

Kwa hivyo, dhana ya kukaribisha mashirikiano baina ya sekta ya umma kwa maana ya Serikali kwa kiasi kikubwa na mashirika yake na taasisi zake nyengine na sekta binafsi imekuwa ikipewa umuhimu mkubwa. Kwa hivyo, napongeza nchi nyingi zilizoendelea hata tunapoangalia miji ambayo sasa imeimarika sana kwa mfano Dubai, lakini hata ukiangalia kama walivyosema wenzangu hapa nchi kama Singapore ni sehemu ya nchi, lakini kwa hadhi yake imekuwa ikihisabiwa kama vile ni eneo maalum la Hong Kong, nchi nyingi za mashariki ya mbali ambazo zinaitwa *Tiger economies* zimefanya kazi kubwa sana kwa kukaribisha dhana hii.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sasa hata nchi ambazo zimeendelea sana sasa nazo pia zinakaribisha kwa kiasi kikubwa sana uendelezaji wa miradi kwa kutumia mfumo huu wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Kwa hivyo, napongeza kwa sababu hiyo kwamba na sisi tumeingia katika duru hizo za kuwa na Mswada kama huu.

Lakini pili, napengeza vile vile kwa jinsi Mswada wenyewe ulivyoandaliwa na sikuona ajabu sana kwa sababu baada ya kupewa tu Mswada huu nilibahatika ndani ya wiki iliyopita kuona katika mitandao kwamba Kampuni inayoheshimiwa ya *NAFAL ASSOCIATES* iliandika katika mitandao kwamba imeshiriki kwa kiasi kikubwa katika kuandaa Mswada huu chini ya udhamini wa Benki ya Dunia *World Bank*.

Kwa hivyo, ndio maana ukiutizama unakuta kwamba kwa kiasi kikubwa sana umejitosheleza katika maeneo mengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa baada ya pongezi hizo, mimi sitokuwa na mengi katika suala la maudhui ya Mswada kwa maana ya vifungu, lakini kutakuwa na baadhi ya mambo ambayo ningetahadharisha na machache ningependa Mhe. Waziri anapokuja kufanya majumuisho anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza, ni suala ambalo mimi huwa silionei tabu kulisema ni suala linalohusu Zanzibar kukabwa koo na hili dudu linaloitwa "Muungano". Katika dunia ya leo sehemu kubwa ya miradi kama hii tuliyoorodhesha katika jaduwali hapa ukiangalia ukurasa wa 379 kuna jaduweli ambayo inaorodhesha miradi ya mashirikiano baina ya sekta umma na sekta binafsi chini ya kifungu cha 9(5).
Mhe. Mwenyekiti, hii inahitaji mtaji mkubwa sana na tunapoangalia mfano wa hapa hapa kwetu kwa maana ya Zanzibar na jirani zetu wa Tanganyika, miradi mikubwa kama hii imetokana na mashirikiano kupitia mara nyengine mabenki ya kimataifa na inapokuja hata kile ambacho tunatakiwa sisi kupitia sekta ya umma tuchangie katika mashirikiano hayo yanayofikiriwa ya sekta ya umma na sekta binafsi, basi mara nyingi huwa hatuna fedha tunategemea labda mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tumeshuhudia kwamba bado Zanzibar haina mamlaka katika eneo hilo na mwaka jana katika vyombo vya habari kuandikwa sana habari za jaribuo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuomba mkopo katika *Exim Bank* India ambayo wenzetu upande wa pili wa Tanganyika wakaamua kuikwamisha Zanzibar katika suala la upatikanaji wa mkopo huo, barua zilichapishwa katika vyombo vya habari, ikaonekana kwamba *Exim Bank* ya India ilitaka uhakikisho au dhamana ambayo bado ilikuwa ina matatizo makubwa kupatikana.

Kwa hivyo, suala langu kwa Mhe. Waziri, ni kwamba je, tunapojielekeza katika dhana ya mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi, katika hali ambayo nchi yetu itapokuja mfano nayo yenyewe itoe kima fulani cha mradi ule kwa maana ikiwa Serikali ndio itakuwa ndio sekta ya umma, wakati huku sisi wenyewe mapato yetu ni madogo na tunagegemea mikopo ambayo hatuna dhamana kujisimamia wenyewe chini ya mfumo huu wa Muungano ambao unaikabaa koo Zanzibar kila uchao isisogee mbele, kwamba je, sisi kiasi gani tutaweza kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii. Hilo ndio suala langu la kwanza ambalo ningeomba unisaidie.

Na bahati nzuri katika hili Mhe. Waziri mwenyewe Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame, yuko katika kumbukumbu akilalamika mwenyewe kiasi gani kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Dk. Benard Membe alivyomnyanyasa na kumwambia hana *instrument* katika kutia saini mkataba mmoja ambao ulikuwa unahusu mradi baina ya Zanzibar na kama sikosei ilikuwa na China.

Sasa najiuliza masuala kama yale bado hayajapata ufumbuzi, wala hayana mwelekeo wa kupata ufumbuzi na tusidanganye kwamba tumepata ufumbuzi katika inayoitwa Katiba pendekezwa, hakuna kitu ndani yake. Kwa hivyo, nasema tutatekeleza vipi suala hili katika Mswada huu ikiwa hali bado iko hivyo Zanzibar bado haina mamlaka kamili imebakizwa kama vile inaendeshwa kwa hewala bwana mpaka atake mwenyewe Tanganyike ndio uruhusiwe unachokitaka na asichokitaka yeye hakipatikani kitu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hilo tuwekewe wazi.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, ambalo nilitaka nitahadharishe katika utekelezaji wa Mswada ni suala zima la uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa sheria hii. Hivi sasa hatujakuwa na sheria kwa maana hii ambayo tunazungumza Mswada huu leo, lakini iko miradi mikubwa na ninapoangalia kifungu cha 14 cha Mswada huu kinachozungumzia Muundo wa Kamati ya Wataalam ya Mashirikiano baina ya Sekta ya umma na Sekta binafsi, sioni ajabu kwa nini katika wajumbe waliotajwa hapa ni Katibu Mkuu anayehusika na Miundombinu miongoni mwa Makatibu Wakuu wachache wa Wizara nyengine.

Kwa sababu Wizara ya Miundombinu ndio yenye miradi mikubwa katika nchi yetu labda ukijumuisha na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, nina bahati ya kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na uvundo ulioko katika maeneo kadhaa ya miradi ya miundombinu, nafikiri tunaujua sisi zaidi Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuliko mtu mwengine yoyote. Nitoe mfano mmoja ambao tumeuzungumza sana katika Baraza hili unaitwa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria (*Airport Terminal 2),* ni mfano hai ambapo kama hakuna uwazi na uwajibikaji kiasi gani nchi inaweza kuingizwa katika hasara kubwa sana.

Mradi ule ulipoanzia ile dhana ya mradi (*concept* ya mradi) uliambiwa ungegharimu dola milioni 57.5. Tukafika pale tukaambiwa baada ya watu kubadilisha karatasi huko na kushirikiana na hawa hawa wawekezaji uchwara ikafika dola milioni 70.Tumetoka tukaambiwa baada ya marekebisho yaliyosababishwa na...mimi sisemi uzembe nasema ulifanywa kwa makusudi na watendaji wanajua walichokifanya, ukafika mpaka tukaambiwa ungefika dola za Kimarekani milioni 110.

Mhe. Mwenyekiti, leo tunaambiwa ili mradi huu ukamilike utafikia kugharimu dola za Kimarekani 128 milioni; umeanza 57.5, tushafika dola za Kimarekani 128 milioni, ukiangalia tofauti yake ni fedha nyingi sana, zingemaliza matatizo ya elimu na matatizo ya afya na matatizo ya maji katika nchi hii. Fedha zime zimeishia mifukoni mwa watu, hakuna uwazi katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mradi huu mkubwa na utaifanya na hii itaingia katika historia nyengine kwa Zanzibar, kwamba mradi huu, hii ndio itakuwa *the most expensive air port terminal to be built in the world here Zanzibar.* Ndiyo itakuwa ya ghali zaidi kuliko zote duniani. Ukiangalia thamani ya ujenzi *per square metre* kwa fedha ambayo iliyotumika kujengea uwanja ule ambao ukubwa wake wa eneo ni kilomita za mraba 21,000.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ukitizama hapa pamepita madudu. Yote ni kwa sababu hakuna uwazi na uwajibikaji. Tukidai maelezo humu ndani tunapewa maelezo ya kuondoshwa ondoshwa njiani na

mara nyengine mijadala mengine inazimwa kwa nguvu, tumeshuhudia hapa. Kuna bajeti zinapitishwa kwa nguvu tu ya Spika. Sasa

Mhe. Mwenyekiti, haya yanapitishwa, lakini tuwe na mfano mwengine.

Mfano mwengine ni mradi wa *E-Government* ambao umeambiwa umeharimu dola za Kimarekani milioni 20, lakini wataalamu wametwambia kwa mradi ule na kwa masafa yaliyotumika haungepaswa kuzidi dola milioni sita. Nilisema sama ndani ya Baraza hili na nikataka Kamati teule iundwe, nikakataliwa katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mfano wa mwisho ingawa mifano iko mingi. Hivi karibuni ambao bahati nzuri kumeingia watu wanaoitakia heri nchi hii wameunusuru. Mradi wa kukamilisha Ujenzi wa Ukuta wa Eneo la Forodhani mpaka kuelekea Bandarini pale. Kuna kampuni nne zili-*tender*. Lakini la ajabu mradi ule ulianzia na awamu ya kwanza ambao ndio ule ustawishaji wa bustani ya Forodhani na aliyefanya kazi ile nzuri yupo.

Kuna baadhi ya mambo tukisema humu ndani huwa tunaambiwa hapa tumetafuta *Single Company* kufanya kazi kwa sababu imeshafanya hapo mapema, tungetegemea ingetumika Forodhani vile vile. Kwa sababu mtu ameshafanya kazi awali. Lakini watu waka-*tender* upya, ikawa dakika za mwisho, pemeshaamuliwa kampuni ile ile iliyofanya kazi ya ujezi wa utengenezaji wa bustari na Forodani ime-*tender* kazi ya kukamilisha ujenzi wa ukuta ule kwa shilingi ya bilioni 9 karibia.

Lakini akataka kupewa kampuni ya Kichina ambao watu huku wanamaslahi yao kwa bilioni 18, mara mbili ya fedha ambayo ingetumiwa na kampuni ile ya mwanzo, tofauti ya bilioni 9 zingemaliza kiasi gani matatizo yetu ya elimu, ya maji, ya afya kwa wananchi wetu wanyonge. Sasa hili lilipata kunusuriwa, kuna wazalendo waliingia kati kidogo likawahiwa.

Sasa nimetoa mifano hii kuonesha kwamba kiasi gani kwamba kukiwa hakuna uwazi wa uwajibikaji. Sheria hii badala ya kuwa muokozi kama Wawakilishi wenzangu wengi walivyozungumza, inaweza ikaja ikageuka laana kwa wananchi wa Zanzibar ikawa ni *instrument* ya wakubwa na watendaji kujinufaisha binafsi huku wananchi masikini wa Zanzibar wakiendelea kubebeshwa mikopo na madani ambayo inachukuliwa kugharamia miradi ambayo imefanywa kwa gharama kubwa kuliko gharama yake binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili mifano mingi niliyoitaja inahusu China na mara nyingi nimesema, tunapaswa kuwaangalia kwa macho mawili Kampuni za Kichina. China ya leo sio china ile iliyokuja hapa mwaka 1964. China ya leo inafanya biashara, mara nyingi nalisema hilo. Mara nyingi tunavutiwa kwa kuambiwa kwamba mikopo hii ni nafuu ni riba ya asilimia moja, lakini ukishapewa mkopo wa riba nafuu unalazimishwa lazima uchague *contractor* katika *list* ya *contractor* za mwenye *Exim Bank* na sheria imekuwekea na humu ndani ndimo mnamopigwa. Kwa sababu mradi unaukuta unatiliwa mara dufu ya gharama zake ambazo ungezipakwa kwa *contractor* mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, hilo ni eneo la pili ambalo nadhani ni muhimu sana tutakapopitisha sheria hii tuje tulione. Sisi wengine tunamaliza muda wetu, tukijaaliwa atakae rudi atarudi, lakini chombo hiki kitaendelea kuwepo na kuulizwa maswali ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho, kwa dakika chache naomba kidogo nizungumzie kifungu cha 3 kwa ufupi sana. Mamlaka ya kuingia mashirikiano baina ya Sekta Umma na Sekta Binafsi. Kifungu 3(1) kinasema;

Kifungu 3(1) "Wizara ya Fedha kwa niaba ya Serikali, inaweza kuingia katika mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, kwa mujibu ya masharti ya Sheria hii".

Lakini kifungu 3(2) ikasema;

"Mamlaka ya Umma inaweza kuingia Makubaliano na Mwekezaji Binafsi, iwapo Mamlaka ya Umma, inahusika kwa mujibu wa sheria, kutoa huduma za umma au miundombinu kwa umma kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii."

Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna 3(3) hicho sitaki kukisoma. Hapa nataka kutahadharisha kwa Serikali. Moja katika malalamiko ambayo tunayapata sana sisi Wajumbe wako tunapofanya kazi za Kamati. Wizara zinalalamika kwamba miradi yao ya Kisekta hawawachiwi Wizara za kisekta kuisimamia. Yote imekusanywa na Wizara ya Fedha, imekuwa kama vile pweza na mikia yake minane kila pahala yupo.

Mhe. Mwenyekiti, nafahamu kwamba Wizara ya Fedha kwa mujibu wa sheria zetu ndio msimamizi wa mitaji ya umma, nalifahamu hilo. Lakini pia, Rais akiamua kuunda Wizara akazipa kusimamia sekta mbali mbali maana yake Wizara zile zinategemewa ndio zenye utaalamu kwa sekta zile husika.

Lakini leo sio wizara tu hata maeneo ambayo tumeziundia mamlaka huru. Kwa mfano mamlaka ya viwanja vya Ndege Zanzibar. Unaendeshwa mradi wa ujenzi wa *terminal* pale na miradi mengine yote mikubwa. Mamlaka haijui chochote. Kila tukenda malalamiko yao ni hayo. Haya unayakuta katika kila Wizara ya Sekta ambapo miradi yake imesimamiwa na Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tunajiuliza miradi hii hii unapokwenda upande wa pili wa bahari tu hapo Tanganyika unakuta Wizara za Sekta ndizo zinazosimamia. Kwa nini katika Zanzibar Wizara ya Fedha imeng'ang'ania kila kitu. Halafu ingelikuwa angalau inasimamia tu tukaona uwazi, uwajibikaji, usafi na fedha inatumika inavyokusudiwa. Lakini matokeo Wizara ya Fedha kusimamia ndio huu uvundo niliouzungumza hapa miradi mingi ambayo imeitia hasara nchi hii.

Kama nilivyosema kifungu cha 3 nataka Waziri akija aje anisaidie, kwamba kipimo gani kitatumika juu ya miradi ipi isimamiwe na Wizara ya Fedha na ipi isimamiwe na mamlaka ya umma kama kilivyosema katika kifungu cha 3(2).

Mhe. Mwenyekiti, mwisho katika kifungu nilichokisema mapema cha 14 chenye Kamati ya Wataalamu ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Ningemuomba Mhe. Waziri aje anisaidie tu. Nini ilikuwa mantiki (*logic*) ya kuamua Wajumbe wa Kamati hii wawe ni

Wajumbe hawa waliotajwa hapa, ambao jumla yao ni watu saba kutoka (a) hadi (g). Kwa sababu kuna maeneo wameingizwa Makatibu Wakuu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nilikuwa nataka kuuliza swali labda *pacific* juu ya eneo moja ambalo hivi karibuni Kamati yetu ilikumbana nalo. Katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuna idara ya mipango miji na vijiji na ndio waliopewa kazi ya kusimamia kuandaa *master plan* na pengine *lands plan* ya mji na nchi kwa ujumla wake.

Moja ambalo linalolalamikiwa sana na kwamba inapokuja matumizi makubwa ya ardhi kwa miradi mikubwa wao hata kuulizwa kushauriwa hawashirikishwi, wanakuja kupewa taarifa ya maamuzi yameshafanywa. Sasa wanajiuliza kwamba katika hali kama hiyo unasimamiaje wewe matumizi bora ya ardhi ikiwa hushirikishwi.

Mhe. Mwenyekiti, hili aliuliza miradi hii inayotegemewa kufanywa na mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kama tunavyosema ni miradi mikubwa. Sasa swali langu ni kwamba, miradi yote inatumia ardhi kwa kiasi kikubwa na tafsiri ya ardhi ni pana kwa maana hii, inajumuisha hata maeneo ya bahari iliyotuzunguuka.

Sasa nauliza kwa nini hatukuona umuhimu wa kuwa mtu, nimemuona Katibu Mkuu anayehusika na ardhi. Lakini Katibu Mkuu anayehusika na ardhi siye anakuwa na dhamana yake pana. Siye ambaye atatambua kwa undani masuala yanayohusu mpango wa matumizi ya ardhi kwa maana ya *lands plan* na *master plan* ya nchi yetu na mji wetu. Sasa nikasema kwa nini hatukuona katika eneo kama hili kuwa na haja. Ndio maana nikamwambia Mhe. Waziri anisaidie kwamba nini ilikuwa mantiki ya kuwachagua hawa waliorodheshwa na wakaachwa wengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme kwa jumla kama nilivyosema, Mswada kwa maana ya uandishi umeandikwa vizuri, tatizo langu lipo katika utekelezaji kwa kuzingatia yale ambayo nimeyasema baada ya uzoefu wetu ambao tumeuona katika nchi yetu kwa kipindi hichi kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, niseme naomba kupata ufafanuzi katika maeneo hayo. Lakini kwa jumla niseme nauunga mkono Mswada huu kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi ambao nawawakilishi hapa wa Jimbo la Mjimkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tuna robo saa ambayo imebakia na nikiangalia sioni kama kuna mtu yeyote. Naam Mhe. Abdi Mosi Kombo.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho na mimi kutoa mchango wangu mdogo sana katika Mswada huu unaosema kwamba mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeingia mkakasi kidogo kutokana na ukurasa wa 360, kifungu cha 14 kinasema;

"Muundo wa Kamati ya Maridhiyano ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

Mhe. Mwenyekiti, mkakasi niliokuwa nao mimi ni kwamba Kamati nzima hii yote imewekwa watendaji wa Serikali. Hivyo, ndio hakuna mtaalamu yeyote katika sekta binafsi ambae angeingizwa hapa ili yale mashirikiano yaliyoambiwa kwamba Mswada huu unamashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Mkakasi wangu ni kwamba kama itakuwa hakuna mtaalamu yeyote katika sekta binafsi, basi itakuwa ndio yale yale kwamba watakuja wawekezaji, wataambiwa sasa tunakupeni kipande cha ardhi hichi hapa, lakini watalaamu walioamua ni upande wa Serikali.

Kwa hivyo, ningeliomba Mhe. Waziri, aje atueleweshe kwa nini hawakuingizwa wataalamu wa upande wa sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, huu ni Mswada mzuri sana ambao Mswada utakao tuinua sisi Wazanzibari, lakini kama hawakuingizwa wataalamu wa sekta binafsi itakuwa ni vigumu sana kutekelezeka. Ningelimuomba Mhe. Waziri afanye busara kama iwezekanavyo, Kamati hii iliyochaguliwa kuhusu wataalam wa sekta binafsi na wao waingizwe. Nimekumbushwa kwamba Mswada wa Mashirikiano lazima upate sekta binafsi na sekta ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdi Mosi Kombo, kwa kuwa muda wetu bado upo, kwa hiyo, ningemuomba sana na kwa kuwa Waziri sasa hivi muda uliobakia hatoweza kufanya majumuisho, kwa hivyo, ningemuomba Mwanasheria Mkuu atutengulie Kanuni ili tuweze kumaliza kikao hichi chetu cha leo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia kanuni ya 23 naomba tuitenge kando ili tuahirishe Baraza hili hadi kesho saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanasheria Mkuu, niwahoji basi wale wanaokubaliana na hilo, wanaokataa, waliokubali na hilo wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa jioni hii ya leo kwa michango pamoja na utulivu wenu, tutaendelea kesho siku ya tarehe 17/03/2015, saa 3:00 hapa hapa. Kwa hiyo, naahirisha kikao hadi hiyo kesho. Ahsanteni sana.

(Saa 1:40 Baraza liliahirishwa hadi kesho tarehe 17/03/2015, saa 3:00 asubuhi)